ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
42.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
43.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
46.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
50.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
52.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
54.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
56.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
57. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
61.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
64.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
66.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
67.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
68.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
71.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Yahya Khamis Hamad	**Kaimu Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Nne – Tarehe 23 Januari, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

TAARIFA YA WAGENI

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuanza shughuli zetu kwa mujibu wa *Order Paper*, tunao wageni ambao niliarifiwa mapema na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, naona mwenyewe hajafika. Lakini ameleta wageni, nafikiri ni wageni ambao wako katika Jimbo lake anashirikiana nao kwa kazi mbali mbali pale.

Wageni hao ni wanne waliofika leo katika ukumbi wetu huu na wageni hao wanatoka kwenye hoteli yenye jina la *Dolphin Berry Resort* hapa Zanzibar na wageni hao ni kama wafuatavyo.

Nitawaomba wale wageni ambao wapo nikiwataja wanyanyuke ili Waheshimiwa Wajumbe wawaone. Kwa hivyo, wageni waliopo ni:

1. Mr. Castern Enna – *General Manager within with wife Mrs.Brigett Enna – Assistant Manager.* Wale pale, ni Meneja Mkuu pamoja na Msaidizi Meneja wa hoteli hiyo. Wamefuatana na
2. Bwana Haroub Ali Khamis – *Human Resource and Public Relations*. Yule pale ndugu yetu. Wengine ni;
3. Bwana Haji Mwadini Haji – *Partner Officer.* Yule pale anaonekana. Huyo sio katika mheshimiwa. Mwengine ni;
4. Dr. Said Mohammed Said – huyu ni daktari ay eye yupo pale juu.

Hao ndio wageni wetu waliofika leo, naomba nichukuwe nafasi hii kuwakaribisha sana katika ukumbi wetu huu. *Mr. Castern and your wife and all team, your most welcome in our chamber here in this morning to see how we are moving on with our session, we most welcome*. Tunawakaribisha sana.

Waheshimiwa Wajumbe, hao ndio wageni wetu naomba nichukuwe nafasi hii kukushukuruni na kuwashukuru wao, ahsanteni sana. Katibu.

TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wajumbe, taarifa ya Spika kwa asubuhi ya leo, inahusu suala la kukamatwa mheshimiwa wetu wa Baraza hili. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka Jimbo la Muyuni, taarifa inaeleza kama ifuatavyo.

Kwa masikitiko makubwa Ofisi yangu imepokea taarifa kutoka kwa Kamishna wa Polisi Zanzibar inayohusiana na kukamatwa na Jeshi hilo Mjumbe wetu wa Baraza la Wawakilishi kutoka Jimbo la Muyuni Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Mhe. Jaku Hashim Ayoub alikamatwa na Jeshi la Polisi siku ya tarehe 18/01/2012 majira ya saa 11 jioni, kwa tuhuma za tukio la kuzama kwa Meli ya MV *Spaice Islander One*, iliyotokea mwaka jana 2011. Jeshi la Polisi lilifanya mahojiano naye na baadae kumwachia kwa dhamana. Hata hivyo, taarifa iliyotolewa kwangu inaonesha kuwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub anatarajiwa kufikishwa mahakamani pamoja na wenzake mara tu hatua za kisheria zitakapokamilika.

Taarifa hii Waheshimiwa Wajumbe, naileta kwenu mbele ya Baraza hili kwa mujibu wa kifungu cha 38(1) na (2) cha Sheria ya Kinga, Uwezo na Fursa za Baraza, sheria nambari 4 ya mwaka 2007. Taarifa ambayo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar wana haki ya kuielewa kupitia kwangu, chini ya kifungu cha 38(3) cha sheria hiyo hiyo nambari 4 ya mwaka 2007.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba kutoa taarifa hiyo kwenu, na mheshimiwa mwenyewe yupo hapa ambaye aliachiwa kwa dhamana kusubiri hatua nyengine za sheria. Nashukuru kutoa taarifa hiyo, ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe wote. Tunaendelea.

MASWALI NA MAJIBU
Nam. 27
Ujenzi Holela wa Hoteli za Kitalii Katika Maeneo ya Fukwe

Mhe. Mtumwa Kheir Mbaraka (Kny: Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi) – Aliuliza:-

Ujenzi holela wa hoteli za Kitalii ambazo hujengwa hadi kwenye fukwe, huwa ni chanzo cha maji ya bahari kupanda juu, Mfano kwenye kisiwa cha Kisiwapanza maji sasa yamepanda hadi kwenye maua.

(a) Mhe. Waziri anaifahamu hali hiyo.
(b) Ni hatua gani ambazo Serikali itachukua angalau kupunguza hali hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu :-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo. Mhe. Spika, nchi yetu imeingia katika biashara ya utalii kwa lengo jema la kukuza uchumi wake ili kuboresha maisha ya Wazanzibari wote. Katika kufanikisha uwekezaji wa shughuli mbali mbali za sekta ya utalii taratibu za kisheria na miongozo mbali mbali imewekwa ili pamoja na mambo mengine kudhibiti uwekezaji utakaoleta athari za kimazingira na kijamii.

Kwa mfano, Kanuni za kudhibiti matumizi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji za mwaka 2006, katika Kanuni ya 9 inayohusu Ujenzi wa Hoteli inaeleza kuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuruhusiwa kujenga hoteli ndani ya mita 30 kutoka alama ya maji kujaa kwa fukwe zenye mchanga; au ndani ya mita 10 kwa fukwe zenye mawe au majabali. Sambamba na Kanuni hiyo, mpango wa ugawaji wa maeneno ya utalii (*Tourism Zoning Plan*) wa mwaka 1993 nao umeelekeza maeneo ya fukwe ya mita hizo kuachwa bila kujengwa.

Mhe. Spika, ujenzi holela wa hoteli za kitalii ambao hujengwa hadi kufika kwenye fukwe huchangia kwa kiasi kikubwa mmong'onyoko wa fukwe na kuleta uharibifu mkubwa kwa mazingira.

Hata hivyo, chanzo cha kupanda kwa maji ya bahari huko Kisiwa Panza, hakitokani na ujenzi wa hoteli kwa kuwa hakuna hoteli yoyote ya kitalii iliyojengwa humo Kisiwa Panza hadi hivi sasa. Miongoni mwa sababu zinazokisiwa kuwa zimepelekea kupanda kwa maji ya bahari katika Kisiwa Panza ni pamoja na mabadiliko ya tabia nchi yanayoendelea duniani kote, ukataji wa mikoko na misitu kwenye fukwe na ukanda wa pwani, miti hiyo imekatwa kwa ajili ya kuni, ujenzi na uchomaji wa chokaa. Uharibifu wa matumbawe na miamba ya bahari, na pia uchukuaji wa mchanga wa pwani ambao wananchi wanauchukua kwa shughuli za ujenzi wa nyumba za kuishi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 27 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ninaifahamu vyema hali ya ujenzi wa hoteli hadi katika fukwe. Miongoni mwa maeneo ambayo hoteli zimejengwa hadi kwenye fukwe ni pamoja na Ukanda wa Nungwi, Kiwengwa, Matemwe na Uroa.

(b) Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, inaendelea kushirikiana kwa karibu zaidi na idara zinazohusika. Kama vile Idara ya Ardhi, Uwekezaji na Idara yna Utalii ili kuona kwamba

hali hiyo inapungua kwa kiasi kikubwa au kuondoka kabisa. Pia kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya kutunza mazingira.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza yenye vifungu (a) na (b), pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri.

(a) Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba vipo baadhi ya visiwa kwa Unguja na Pemba kikiwemo Kisiwa Panza, vimo katika hatari ya kuzama, Mwenyezi Mungu apishe mbali, iwapo wizara pamoja na serikali haitochukua hatua za kushughulikiwa tatizo hili.

(b) Je, Mhe. Waziri huoni itakuwa ni vizuri wizara ikishirikiana na serikali kwenda kuona eneo hilo kama ikiwezekana ikawa ni siku ya upandaji wa miti ya mwitu ambayo ndio inayoota katika fukwe hizo kulikoni mikoko ambayo huota kwa kusuasua, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

(a) Mhe. Spika, naomba niwe mkweli kabisa kwamba sina tafiti za uhakika ambazo zinaniambia kwamba baada ya kipindi fulani visiwa kama Kisiwa Panza na vingine vinaweza kutoweka katika ramani. Lakini kutokana na hali ya kawaida tu ya mabadiliko ya tabia nchi, tayari katika ulimwengu huu kuna baadhi ya visiwa vinavyofanana na vyetu vinasemekana kwamba vitatoweka katika ramani ya dunia kutokana na kuzama. Kwa hivyo, huwenda na sisi pia baadhi ya visiwa vyetu vikawa katika hatari hiyo, lakini bado hatuna utafiti unaothibitisha hayo.

(b) Mhe. Spika, napenda sana nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba serikali haikukaa tuli kuiangalia hali ya Kisiwa Panza. Ofisi yangu ilipeleka ujumbe mkubwa ukiongozwa na mimi mwenyewe na viongozi wa idara zote kutembelea kisiwa hicho, ambako hakuna eneo ambalo tuliliacha kulitembelea. Tumeiona hali ilivyo na ofisi inajipanga pamoja na shughuli za kuweza kuanzisha vikundi ambavyo vitapanda miti ya mikoko basi kuweza kuangalia pia ni jinsi gani tunaweza kukabiliana na uharibifu huo.

Mhe. Spika, nakubaliana kabisa na ushauri wa Mhe. Mjumbe wa kwamba tuendelee kukaa na wananchi na viongozi wa maeneo hayo, ili kuona ni njia gani bora au kama kuna miti ambayo ni bora zaidi katika kuhifadhi mazingira. Kwa sababu kwa mujibu

wa ofisi yangu, miti ya mikoko ndio ambayo inachukua muda mfupi sana kuota katika maeneo hayo na ingekuwa busara kuendelea kuipanda hiyo. Lakini hata hivyo, ushauri wake tunaupokea.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuniruhusu kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba kuna baadhi ya wawekezaji kwa upande wa Nungwi hawakufuata zile taratibu zilizowekwa za kuwacha mita 10 au 20 kutoka katika kima cha maji yanapojaa kuanza kujenga hoteli zao.

Je, ni lini serikali itawalazimisha wawekezaji hawa kujenga kuta za uhakika kusudi kuzuwia maji ya bahari yanayopanda juu kuharibu mazingira.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, naomba kwanza nimfahamishe Mhe. Mjumbe kwamba kanuni ambayo inatakiwa kufuatwa na wawekezaji ya kuwacha mita 30 kwa *send beach* na mita 10 kwenye maeneo ya miamba, ni kanuni ambayo iko chini ya Idara ya Mipango Miji na Vijiji katika Wizara ya Ardhi. Ofisi yangu ni kwamba inaipenda sana sheria hii tukiunganisha kwamba inatusaidia sana katika shughuli nzima ya kuhakikisha mazingira yetu yanatunzwa. Ofisi yangu inachofanya kikubwa ni kushirikiana na Idara hii ya Ardhi ambayo ni Idara ya Mipango Miji na Vijiji, ambayo ndio yenye kanuni hiyo inayotaka matakwa hayo, kuweza kuipa taarifa kila wakati uharibifu unapotokea, ili iweze kuchukua hatua za kusimamia kanuni hiyo.

Nam. 59

Matengenezo ya Msingi Shehia ya Msingini

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman – Aliuliza:-

Katika Shehia ya Msingini – Wilaya ya Chake-Chake kuna msingi unaopitisha maji machafu kuelekea Bandataka.

Msingi huo badala ya kumwaga maji baharini unakusanya maji na kuleta usumbufu kwa wananchi. Kwa kuwa maji yanayokusanyika hutoa harufu mbaya na kuna uwezekano wa kusababisha wananchi kuugua maradhi ya mripuko.

Je, Mhe. Waziri, Serikali ina mpango gani wa kuufanyia matengenezo msingi huo.

Mhe. Waziri Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, serikali imepanga kukamilisha mradi wa ujenzi wa msingi unaopitisha maji machafu uliopo katika Wilaya ya Chake-Chake kuelekea Bandataka kupitia msingini na Mtoni ifikapo, au ndani ya mwaka huu wa fedha wa 2012.

Mhe. Spika, serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeshatenga jumla ya TZS 30 millioni. Kati ya fedha hizo ambazo zinatarajiwa kutumika katika kukamilisha mradi huo. Hadi hivi sasa, jumla ya TZS 20 millioni zimeshatolewa na kazi zinatarajiwa kuanza mara moja kukamilisha kazi hiyo. Ahsante.

Nam. 100

Kukataliwa Baadhi ya Sarafu Madukani

Mhe. Rufai Said Rufai – Aliuliza :-

Utaratibu wa matumizi ya fedha halali katika nchi nyingi Duniani uko katika hali mbili yaani Noti na Sarafu. Nchi yetu Tanzania inao utaratibu kama huo na tunazo sarafu za shilingi tano, kumi, ishirini, ishirini na tano, khamsini, mia na mia mbili.

Je, ni kwanini sarafu za shilingi tano, kumi, ishirini na ishirini na tano zinakataliwa na wafanyabiashara pale wananchi wanapohitaji huduma zao mbali mbali madukani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na kwa ridhaa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 100 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006 kifungu cha 26, Benki Kuu ya Tanzania ndicho chombo pekee chenye mamlaka na haki ya kutoa na kusambaza noti na sarafu kwa malipo nchini Tanzania. Vile vile, Benki Kuu ndiyo iliyopewa dhamana ya kuziondoa noti au sarafu katika mzunguko wa fedha. Inapofikia kutaka kuziondoa sarafu au noti, Benki Kuu

hupaswa kutoa taarifa rasmi katika gazeti la serikali ili kuufahamisha umma juu ya azma ya kuziondoa noti au sarafu katika mzunguko kama kifungu cha 28 (2) cha Sheria ya Benki Kuu kinavyoeleza.

Mhe. Spika, kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kwamba sarafu alizozitaja Mhe. Mwakilishi hazijaondoshwa katika mzunguko wa fedha, hivyo bado ni halali kutumika na nawaomba wafanyabiashara na wananchi wasizikatae.

Aidha, zipo sababu tatu za binafsi zinazowafanya baadhi ya wafanyabiashara kuzikataa sarafu hizo.

1. Biashara zao hazina mauzo ya sarafu.
2. Kuona tabu kuzikusanya sarafu hizo na kuziwasilisha benki.
3. Kuona kwamba fedha kwao ni noti na sio sarafu.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kuwa hizo sio sababu za msingi, bali ni sababu binafsi. Nawaomba wafanyabiashara wazikubali sarafu kama ni fedha halali kwa matumizi halali.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, nashukuru kwa majibu ya Mhe.Waziri. naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri je, ni lini serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu, kwa kuwa hizi serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu, kwa kuwa hizi sarafu imekuwa ni mzigo kwa wafanyabiashara. Je, hatuoni kama ni vyema kubadilisha hizi sarafu pakaundwa sarafu moja tu ambayo itakuwa inaletwa kwa wafanyabiashara.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, hoja yake ni ya msingi na kwa utaratibu wa sheria ya Benki Kuu, mimi sina mamlaka ya kusema lini ziondoshwe, lakini nimeupokea ushauri wake na nitaufikisha kwa Gavana wa Benki Kuu, ili tuone nini tunafanya katika sarafu hizi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri kakiri kwamba sababu hizi zinazotolewa sio sababu za msingi ni sababu za binafsi, na kwa kuwa fedha hizi ni halali na wafanyabiashara sasa hivi, hata kama ni duka ambalo linatumia sarafu hizo ndogo wanazikataa na kuwasababisha wananchi usumbufu.

Je, ni lini hasa serikali kwa kupitia wizara yake itatoa tamko rasmi na kuwaita wafanyabiashara kuwaelimisha kwamba fedha hizi ni halali na kupunguza usumbufu wa wananchi. Endapo watakuwa na ukaidi je, wizara yake itachukua hatua gani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka nimwambie tu kwamba kutoa tamko linapaswa litolewe na Gavana wa Benki Kuu kwa mujibu wa sheria. Nitafikisha taarifa hii kwa Gavana wa Benki Kuu ili aweze kutoa tamko hilo.

Lakini kwa upande wa kuwaita wafanyabiashara walioko Zanzibar, kwa upande wangu kama waziri mwenye dhamana ya fedha na kwa kushirikiana na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko huwa tunakutana mara kwa mara na wafanyabiashara, basi tutafikisha haya maelezo kwa wafanyabiashara, ili kuwaeleza hali halisi kwamba fedha hizi ni halali na waendelee kuzipokea na kuwaomba waendelee kuzipokea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, naomba nimuulize swahib yangu Mhe. Waziri swali langu dogo tu la nyongeza. Mhe. Spika, mbali ya kuzikataa sarafu zilizotajwa, lakini pia kumeibuka mfumo au utaratibu katika nchi yetu, ambapo wafanyabiashara wamekuwa wakitoza tozo mbali mbali kutokana na huduma au vitu wanavyoviuza kwa kutumia sarafu ya kigeni hasa dola ya Kimarekani, na kwa sababu sarafu inayotambulikana Tanzania ni shilingi ya Tanzania.

Je, Mhe. Waziri ana kauli gani juu ya suala hili na je, ina uhalali ikizingatiwa kwamba fedha ambayo imekubalika kutumika Tanzania ni shilingi ya Tanzania.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza fedha halali kwa matumizi halali ndani ya Tanzania ni shilingi ya Tanzania na sio fedha ya aina nyengine yoyote ile. Wafanyabiashara wa aina yoyote ile ambao wanapokea au wanatoa fedha ambayo sio shilingi ya Tanzania basi wanakwenda kinyume na taratibu na sheria za nchi. Hivyo, hawapaswi kufanya hivyo na ninawaomba sana wasifanye hivyo. Isipokuwa katika maeneo ya hoteli, mtalii anaweza akatumia fedha ya kigeni yoyote ile katika kulipia bili zake katika hoteli.

Nam. 108
Marekebisho ya Mishahara

Mhe. Jabu Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mhe. Spika, mwanzo kabla ya yote sina budi kukushukuru kwa kunitolea taarifa muhimu, ambayo imenihusu mimi mwenyewe nikiwa ni mjumbe wa Baraza lako hili tukufu katika pahala panapostahiki.

Vile vile Mhe. Spika, nataka nikutowe wasi wasi wewe mwenyewe pamoja na wajumbe wa Baraza lako hili na wananchi wa Jimbo la Muyuni pamoja na maswahiba wangu wanaonitakia kheri. Sitakiwi kujibu swali hili wakati liko mahakamani, kama kanuni zako zinavyosema Mhe. Spika. Mimi sio mmiliki wa Meli ya MV Spice Islander wala sio Mmiliki wa Kampuni ya Visiwani.

Hii ni kwa baadhi tu ya wajumbe walioteuliwa kutaka kunichafulia jina langu na kunivunjia heshima yangu Mhe. Spika. Baada ya maelezo hayo naomba swali langu nambari 108 lijibiwe.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imerekebisha mishahara ya watumizi wa umma kwa lengo la kuwaongezea maslahi yao. Lakini marekebisho hayo yameleta malalamiko mengi miongoni mwa walengwa.

(a) Mhe. Waziri, inakuwaje watumishi wenye sifa zinazolingana kitaaluma na muda wa utumishi wao watafautiane kimaslahi kwa sababu ya tafauti ya Ofisi wanazofanya kazi. Mfano wanasheria wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutafautiana na mtumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Mahakimu wa Wilaya.

(b) Vigezo gani vimetumika kuwapandisha watumishi wa ngazi ya chini ya mshahara kutoka 100,000/= hadi 125,000/= wakati Zanzibar hivi sasa inakabiliwa na mfumko mkubwa wa bei za chakula ambao umewaumiza watu wa chini.

(c) Kwa kuwa watumishi wote wanatumia soko moja la chakula, serikali imetumia vigezo gani vya kupanga mishahara kwa sababu wafanyakazi kuanzia ngazi ya Wakurugenzi, Makatibu Wakuu ndio wamenufaika zaidi.

Mhe. Spika: Maswali yote mengine mheshimiwa, yanahusu kwenye vyombo vya sheria. Haya Mhe Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora karibu kujibu swali.

Mhe Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 108 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo. Kwanza kabisa Mhe. Spika, napenda kukubaliana na Mhe. Mjumbe kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imerekebisha mishahara ya watumishi wa umma kwa lengo la kuwaongezea maslahi yao kwa nia ya kuwawezesha kufanya kazi zao kifanisi.

Hata hivyo, sikubaliani na kauli ya kwamba marekebisho haya yameleta malalamiko mengi miongoni mwa walengwa. Taarifa tulizokuwanazo ni kwamba kwa mara ya kwanza serikali imechukua juhudi za kutosha katika kuwajali watumishi wake. Hata hivyo, yapo matatizo madogo madogo yaliyojitokeza kutokana na taarifa za wafanyakazi kutokuwa sahihi. Matatizo haya yamesababi

(c) Mhe. Spika, kama nilivyokwisha kueleza katika swali (b) kigezo kikubwa kilichotumika ni jinsi ya hali ya fedha ilivyoruhusu. Kwa kutumia kigezo hicho serikali imeongeza mshahara wa kima cha chini kwa asilimia 25, kima ambacho watumishi wengi wamefaidika nacho.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake muafaka tena mwanana kabisa.

(a) Hivi Mhe. Waziri anayo taarifa kuwa wafanyakazi wa Mahakama wa Unguja na Pemba wameshatoa tahadhari kwa kugoma, iwapo nyongeza zao mishahara hazitoongezwa upya hasa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo pamoja na wafanyakazi wake?

(b) Mhe. Waziri, naomba kufahamu ni mazingira gani ya kazi tofauti kati ya Mahakimu wa Wilaya na Waendesha Mashtaka ya Serikali wakati wote wanatumia soko moja la chakula, viwango vya taaluma vyao vyote vinafanana. Vile vile inaonesha *experience* zaidi huwa baadhi ya Waendesha Mashtaka kutoka Afisi ya *DPP* wanao uzoefu zaidi kuliko Mahakimu?

(c) Hivi sasa serikali inafikiria kurekebisha mafao ya Viongozi wa Kisiasa kabla ya kumaliza matatizo yaliyojitokeza kuhusu marekebisho ya mishahara, ambayo yameibua kilio kikubwa kwa watumishi wa umma mbali mbali?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza kabisa Mahakimu wa Wilaya wamelipwa mafao au mishahara yao kulingana na hadhi ya nafasi zao. Vile vile hawa wamelipwa mafao kama wanavyolipwa Makadhi wa Wilaya na wanalipwa sawa na Manaibu Wakurugenzi.

Tatizo lilikuwa ni Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo. Kwa kweli Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo tofauti yao na hawa Mahakimu wengine, kwanza viwango vyao vya elimu havilingani kabisa na viwango vya elimu vya Mahakimu wa Wilaya na wengine.

Hata hivyo, napenda kumhakikishia Mhe. Mjumbe kuwa suala la Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo wizara yangu tayari imeshalishughulikia kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria, hivyo kuanzia mwezi huu Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo watafaidika na nyongeza kuanzia asilimia 35 mpaka 45. Hilo moja.

Mhe. Spika, ni mazingira yepi yanayowatofautisha Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo na hizo afisi nyengine. Kwa kweli hapa jambo liko wapi ni kwamba unapozungumzia mtu mwenye ngazi ya *degree* ya kwanza na yule mwenye *certificate* na hayo ndio mazingira yanayotofautisha hivi viwango. Lakini mazingira gani aliyoyakusudia kati ya watu wa Mahakamani, watu wa Mwanasheria Mkuu na wale watu wa *DPP*, hizi ni kazi tofauti.

Kwa hivyo, hiyo ndio sababu iliyosabisha tuweze kutofautisha kati ya mishahara ya Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo na Mahakimu wa Wilaya kama nilivyosema mwanzo. Lakini Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo, Wanasheria wa Serikali pamoja na Waendesha Mashtaka katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kuhusu suala la kutoa indhari nalijua au silijui. Mhe. Spika, najua kwamba Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo kupitia chama chao walikuja rasmi ofisini kwangu kwa ajili ya kueleza malalamiko yao. Kutokana na hali hiyo, ndio maana wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria tumeweza kuyafanyiakazi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, miongoni mwa vigezo ambavyo serikali ilitumia kwa ajili ya kupandisha mishahara ni elimu pamoja na uzoefu.

(a) Je, ni kwa nini Wahasibu wenye uzoefu na kiwango cha elimu sawa kwa Pemba na Unguja ni tofauti, yaani Wahasibu wa Unguja wanaofanyakazi katika Makao Makuu ya Wizara wanayo maslahi zaidi ya mishahara kuliko wahasibu kama hao, ambao wenye kiwango sawa cha elimu na wanafanyakazi Pemba?

(b) Je, unaweza kututhibitishia kwamba Wahasibu wa Baraza la Wawakilishi wanapata mshahara sawa na mshahara wa Mhasibu Mkuu wa Serikali au afisi yako?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, Mhasibu Mkuu wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu ana-*Vote* analipwa sawa na Mhasibu Mkuu mwengine yeyote ambaye anashughulikia *Vote* kama Mhasibu Mkuu wa Wizara na zile taasisi zinazojitegemea.

Kigezo kilichotumika kwa nini Wahasibu wa Pemba na wale wa Unguja. Kwanza ieleweke wanaolipwa kiwango cha mshahara wa Mkurugenzi, unapolipwa mafao yako kuna tofauti ya kiwango vya malipo, yaani kuna mshahara na maposho.

Kwa hivyo, Wahasibu Wakuu wanaoshughulikia *Vote* wanalipwa viwango vya mshahara wa Mkurugenzi na *Internal Auditor* analipwa mshahara na Naibu Mkurugenzi. Lakini hawalipwi mafao mengine kama maposho na mambo mengine, yaani wao wanacholipwa ni mshahara tu.

Sasa ni kitu gani kilichotofautisha kati ya Wahasibu walioko Pemba na wale wa Unguja. Jibu ni kwamba Mhasibu analipwa yule anayesimamia *Vote*. Kwa maana hiyo, suala la Wahasibu wa Pemba wanalipwa tofauti na wale wa Unguja hilo sina hakika nalo. Lakini nitalifanyiakazi, ili nijue kwa maana ya wale wahasibu wanaoshughulikia *Department* nyengine ndogo ndogo. Ikiwa ni Mhasibu ambaye anayeshughulikia *Vote* awe Pemba au Unguja, basi huyo atakuwa analipwa kima cha mshahara cha Mkurugenzi. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, miongoni mwa marekebisho yaliyofanywa na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni maposho kwa watumishi, ambapo madereva wanaowaendesha viongozi pamoja na makarani wameongezwa maposho kwa mujibu wa toleo lililotolewa na wizara hii. Kwa kweli nyongeza ambazo zimeelekeza zitaanzia mwezi wa Disemba 2011.

(a) Je, Mhe. Waziri atakubaliana nami kwamba baadhi ya wizara na taasisi za serikali bado hazijalipa nyongeza hizo za posho katika mwezi huo?

(b) Ni sababu zipi zilizowafanya washindwe kulipa posho hizo kwa wakati, ambapo tayari wamepokea matoleo kutoka katika wizara yako?

(c) Ni hatua zipi atazichukua Mhe. Waziri, ili kuhakikisha watumishi hao wanalipwa posho zao pamoja na *arrears* zao za mwezi wa Disemba?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ninayo taarifa kwamba baadhi ya wizara pamoja na taasisi bado hazijawalipa watumishi hawa kama toleo lilivyoagiza. Kwa hivyo, wizara yangu imeshachukua hatua ya kuwakumbusha kwamba wawalipe watumishi hawa maposho yanayostahiki kuanzia mwezi ule ambao serikali imeamua.

Kuhusu tutawachukulia hatua gani, kwa kweli hatua ni hizo za kuwakumbusha na watakapokuwa hawatekelezi, basi nadhani ni suala la kujua kwa nini hawatekelezi. Lakini nia ni kuwaongezea wafanyakazi hawa maposho, ili kuwawekea mazingira maalum ya kuweza kufanyakazi zao kwa ufanisi zaidi.

Nam. 12

Uundaji wa *SACCOS*

Mhe. Salma Mussa Bilali – Aliuliza:-

Katika jitihada za kuwahamasisha wananchi kujiunga na kuunda Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*), ili waweze kujikimu na kujipunguzia ukali wa maisha.

(a) Je, Mhe. Waziri hivi sasa zimeshaandikishwa *SACCOS* ngapi Unguja na Pemba na ni za ngazi gani?

(b) Kwa vile *SACCOS* nyingi tayari zimeshasajiliwa wizara yako haioni umuhimu wa *SACCOS* hizo kuunda muungano wao, ili ziweze kuutumia muungano huo kupata mahitaji yake, ikiwa ni pamoja na mitaji, badala ya kila *SACCOS* kutafuta mikopo kupitia Benki au Taasisi nyengine za fedha katika kupunguza gharama za uendeshaji?

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 12 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara yangu ni kweli imefanyakazi kubwa ya kuanzisha na kusajili *SACCOS*. Hadi hivi sasa jumla ya *SACCOS* 463 zimesajiliwa, ambapo kati ya hizo 291 ni Unguja na 172 ni kutoka Pemba.

(b) Mhe. Spika, kuhusu suala la kuunda umoja wa *SACCOS*, wazo hili ni la msingi na ninaungana naye kwenye hilo. Kutokana na hali hiyo,

naomba kutoa taarifa rasmi kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwamba tayari tumeshaunda Muungano huo ambao unaitwa Chama Kikuu cha Vyama vya Akiba na Mikopo Zanzibar (*Zanzibar Saving and Credit Cooperative Union – ZASCU*).

(c) Hata hivyo, changamoto iliopo mbele yetu ni kuijengea uwezo, ili iweze kutekeleza majukumu yake pamoja na kuhudumia wanachama wake kwa ufanisi pamoja na kuhamasisha *SACCOS* zilizopo zijiunge na Chama hicho Kikuu cha Akiba na Mikopo.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyonge.

(a) Namuomba Mhe. Waziri alieleze Baraza hili tukufu Muungano huo wa Vyama vya Ushirika umeanzishwa mwaka gani na ofisi yake iko wapi?
(b) Wizara imejipanga vipi katika kukabiliana na changamoto zilizopo, ili muungano huu uweze kusimama na kuzisaidia *SACCOS*, kwa lengo la kusaidia wanachama wake kulingana na dira pamoja na malengo yao waliyojiwekea?

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kwanza napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Mjumbe tokea tumeanza kikao hiki Mhe. Mwakilishi amekuwa ni muulizaji mzuri sana wa maswali na hili likiwa ni swali lake na nne kwa wizara yangu. Kwa hivyo, ninampongeza sana. Nadhani tutakapotoa zawadi wa kwa wale wanaoumwa na *SACCOS* zetu pamoja na Vikundi vya Ushirika, basi Mhe. Mjumbe naye tunaweza kumfikiria. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimesema kwamba umoja huu umeanzishwa hivi karibuni. Kwa hivyo, tumekusudia kuiwezesha hii *SACCOS* moja kubwa kabisa ambayo itakuwa na uwezo wa kuzishawishi *SACCOS* nyengine ndogo ndogo kujiunga pale. Faida inayopatikana kwa *SACCOS* ndogo ndogo ni shida kupata dhamana ya kibenki, lakini kila *SACCOS* ikiwa kubwa. Kwa mfano, hivi karibuni Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni alinialika na nilikwenda kule, basi alivikusanya vikundi vyote vya pale na mimi nilikwenda kusema maneno tu. Kwa hivyo, utaratibu kama ule ndio unaokubalika.

Kwa kweli hivi sasa ninahakika wako kwenye hatua nzuri hivi sasa na natarajia *SACCOS* ile itakuwa ni moja ya *SACCOS* zenye nguvu kabisa kama zilivyo za Mwanakwerekwe na maeneo mengine. Kwa maana hiyo, Mhe. Mjumbe wahamasishe wananchi wako wajiunge na *SACCOS* kubwa na kama nilivyosema tutaziimarisha pamoja na kuziendeleza.

Nam. 29

Utaratibu wa Kuingia Skuli Mikondo Miwili (Asubuhi/Jioni)

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Ubora wa Elimu unategemea sana namna ya ufundishaji, walimu wenyewe na muda wa kufundisha.

(a) Je, utaratibu wa kuwafundisha wanafunzi kwa mikondo miwili (asubuhi na jioni) unatoa muda muafaka wa kufundisha?

(b) Ili kuokoa maendeleo ya vijana wetu, serikali inachukua jitihada gani kuondoa utaratibu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 29 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa ubora wa elimu unategemea kuwepo kwa walimu waliomahiri, mbinu bora za kufundishia pamoja na muda wa kutosha wa kufundishia katika skuli zetu. Mchanganyiko wa mambo hayo ndio unaoleta ufanisi katika elimu na upatikanaji wa elimu bora.

Baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, utaratibu wa kufundisha kwa mikondo miwili asubuhi na jioni katika skuli zetu umeanza tokea mwaka 1980, umesaidia sana katika kuwezesha nchi yetu kupanua kwa kasi huduma ya elimu na hatimaye wanafunzi wengi kupata nafasi ya kufundishwa katika skuli zetu. Hata hivyo, ni kweli kuwa utaratibu huu umechangia sana katika kupunguza muda wa kufundishia katika skuli zetu.

Kwa hivi sasa ni skuli za Wilaya ya Kusini Unguja tu, ndizo zinazofanya kazi kwa mkondo mmoja kutokana na kuwepo kwa wanafunzi wachache na kuwepo madarasa ya kutosha.

Aidha pamoja na kuwa na skuli nyingi zetu zinafundisha katika mikondo miwili, walimu wetu wanafanya jitihada kubwa kuhakikisha kuwa muhtasari inafundishwa kikamilifu.

Miongoni mwa mbinu wanazotumia ni pamoja na kufundisha masomo ya ziada katika siku za mapumziko. Hadi sasa hakujaonesha tofauti ya maendeleo ya mwanafunzi baina ya skuli zinazofundisha kwa mikondo miwili na zile zinazofundisha kwa mkono mmoja. Utaratibu wa kufundisha kwa mikondo miwili utaendelea kutumika kwa sasa, kutokana na skuli zetu nyingi kuwa na uhaba wa madarasa ukilinganisha na idadi kubwa ya wanafunzi tulionao.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada kubwa zinazochukuliwa na wananchi pamoja na wizara katika kujenga na kukamilisha ujenzi wa madarasa mapya na skuli mpya za kisasa bado mahitaji ya madarasa ni makubwa mno. Kutokana na hali hiyo, wizara inakusudia ifikapo mwaka 2015/2016 idadi ya wanafunzi katika madarasa ipungue hadi kufikia idadi ya wanafunzi 40 kwa darasa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa maendeleo ya vijana wetu yanategemea na ufundishaji wa walimu madarasani.

Je, Mhe. Waziri kuna tathmini gani inayofanyika mara baada ya matokeo ya mitihani?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, sijamfahamu swali lake namuomba arudie tena.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa maendeleo ya vijana wetu yanategemea na ufundishaji wa walimu madarasani. Je, Mhe. Waziri kuna tathmini gani inayofanyika mara baada ya matokeo ya mitihani?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Spika, baada ya matokeo ya mtihani wizara huwa tunakaa na kufanya tathmini. Kwa hivyo, mpaka hivi sasa katika tathmini zetu hatujaona kama nilivyojibu kama swali langu la msingi tofauti ambayo imeonesha kama wanafunzi wanaosoma kwa mkondo mmoja wanapasi zaidi kuliko wale wanafunzi ambao wanaosoma kwa mikondo miwili.

Kwa mfano, Mhe. Spika Skuli za Kusini Unguja ambao nimeeleza ndio wanaosoma kwa mkondo mmoja, kwa kweli hawana tofauti na skuli nyengine ambao wanaosoma kwa mikondo miwili, yaani matokeo yao huwa ni sawa. Kwa maana hiyo, mpaka hivi sasa katika tathmini zetu bado hazijaonesha tofauti yoyote.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuongeza jibu la Mhe. Naibu Waziri kuhusu tathmini kama alivyosema kwamba tukimaliza mitihani huwa tunakaa kitako kwa ajili ya kufanya tathmini.

Sasa kwenye tathmini yetu katika skuli zinazofanya vibaya huwa inagundua kwamba kuna hitajika msaada mkubwa wa wazee, lakini sio tatizo la maskuli yenyewe, isipokuwa ni msaada wa wazee unatakiwa mkubwa.

Kwa mfano, hivi sasa katika skuli zetu kuna mambo yanatendeka ambayo yanapunguza sana uwezo na wazee wayatizame na watayaona kuwa mtoto anayetokea wakwanza katika darasa, wakwanza katika darasa la pili na haya yanatokea kwenye *position* nzuri baina ya wakwanza, wapili na watatu.

Sasa anapofika katika *standard* 5 na 6 matokeo yake yanashuka na wala si kwa sababu ya walimu, isipokuwa anaanza kuingia katika mambo ya ajabu. Kwa hivyo, hili ndilo tatizo linalotokea sana katika maskuli yetu Mhe. Spika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri wakati alipokuwa akijibu swali hili alisema kwamba kwa zile skuli ambazo zinaingia kwa mikondo miwili walimu wanajitahidi kuzipa mapengo yaliomo kwenye *Syllabus* kwa kufundisha wakati wa ziada.

(a) Ikiwa skuli wanafunzi wanakwenda mikondo miwili, yaani asubuhi na jioni wakati huo wa ziada wanaupata vipi?

(b) Skuli nyingi hizi ziko mashamba hazina umeme *boarding* na wala watu hawawezi kwenda kusoma usiku. Kwa hivyo wanapata vipi wakati wa kuongeza masomo ya ziada?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nilizungumza katika jibu langu la msingi kama ambavyo ameeleza Mhe. Mjumbe kuwa walimu wanajitahidi katika kusomesha masomo ya ziada.

Ni kweli na nilieleza jitihada wanayoifanya na hili nataka kuchanganya na swali lake la pili, kwa kweli wanatumia zile siku ambazo hawaendi skuli. Mhe. Spika, nilisema kwa mfano, siku za Jumamosi na Jumapili kwa kawaida hakuna skuli. Kwa hivyo, zile siku za mwisho wa wiki ndizo ambazo walimu wanakaa na wanafunzi na kuchukua nafasi hii ya kuhakikisha kuwa wanatumia muda ule wa siku za *weekend*.

Nam. 89

Maadhimisho ya Mwaka wa Kiislamu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Katika Vikao vya Baraza vilivyopita tuliuliza suala la Kuadhimisha Kuanza kwa Mwaka wa Kiisalmu. Mara zote serikali imekuwa ikiwaeleza wananchi kuwa suala hili linafanyiwa kazi, lakini uhalisia wa hali hiyo hauonekani.

(a) Je, Mhe. Waziri anaweza kutueleza ni vipi umakini wa serikali unaonekana katika suala hili?

(b) Kama umakini wa serikali katika hili hauwezi kuelezwa, serikali iwajulishe wananchi tatizo gani limepelekea hali ya serikali kutoeleweka katika suala hili?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali leke Nam. 89 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, suala la Kuadhimisha Kuanza kwa Mwaka Mpya wa Kiislamu lina umuhimu mkubwa sana hasa kwa kuzingatia ukweli kwamba wananchi wengi wa visiwa hivi, ambao ni Waislamu wanalidai kwa muda mrefu sana.

Mhe. Spika, kama nilivyojibu swali hili katika maswali mawili yaliyopita swali Nam. 121 na Nam. 31 ya vikao viwili vya Baraza vilivyopita vya mwezi wa Aprili, 2011 na mwezi wa Oktoba, 2011. Wizara yangu ililitizama suala hili lakini kwa mapana yake. Kwa hivyo, baada ya kukamilisha hatua hizo kwa upande wetu, basi maoni yetu tayari tumeshayapeleka katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa hatua zake. Mhe. Spika, tulipeleka maoni hayo kwa barua kumbukumbu Nam. WKSW/19VOL.I/11 ya tarehe 5 mwezi wa Januari, 2012.

Mhe. Spika, tumefanya hivyo kwa sababu hii inatokana na kuwa sheria inayohusiana na shughuli za Mapumziko (*holidays*) ziko chini ya dhamana ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Sheria hii ni Sheria ya Tafsiri Nam. 7 ya mwaka 1984 na chini ya kifungu cha 4 kumpa uwezo Mhe. Rais baada ya kupata ushauri kutoka kwa Makamu wa Pili na kuukubali na kutangaza siku yoyote kuwa ni ya mapumziko. Mchakato huu hivi sasa ndio unaendelea.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe astahamili hadi matakwa ya hiyo sheria yakamilike na kupata maamuzi kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuwa mstahamilivu kwamba suala hili limekuja zaidi ya mara tatu mpaka hii leo na inaonesha anayo nia ya kuleta mashirikiano juu ya suala hili.

(a) Mhe. Waziri, Kwa sababu watu wote wapo, ikiwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ipo pamoja na wewe mwenyewe upo. Hivi kuna sababu gani inayofanya msishauriane, ili tupate jibu?

(b) Nimezoea katika Baraza hili kusikia mara tu, wakati wowote, matunda yake, serikali imo mbioni na leo Mhe. Waziri unaniambia hivi nistahamili mpaka lini? *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, serikali haiendeshwi kama Shirika Binafsi, isipokuwa serikali inaendeshwa kwa utaratibu wake. Kwa mfano, tulisema hapa tunapitia katika utaratibu uliowekwa na utaratibu wa aina moja tayari umeshakamilika.

Sasa tumepeleka kwa Makamu wa Pili wa Rais, ili na yeye afuate utaratibu kama sheria inavyotaka. Kwa hivyo, hatuwezi kwa pamoja tukaka na kusema tuamue bila ya kufuata utaratibu wa kisheria kama ulivyo. Kwa maana hiyo, tutaendelea kufuata sheria, ili maamuzi yatakayotoka yawe yametoka kwa mujibu wa sheria zetu, ambapo na wewe ni Mhe. Mjumbe ambaye tumetunga sheria hizo.

Nam. 33

Uanzishwaji wa Hospitali za Mikoa

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Aliuliza:

Serikali ilikuwa na nia safi ilipoanzisha hospitali za Mkoa kama vile Micheweni na Vitongoji kwa upande wa Pemba, Kivunge na Makunduchi kwa upande wa Unguja, lengo ni kuwasogezea wananchi huduma za afya. Kwa vile hospitali ya Makunduchi iko mbali katika Mkoa wa Kusini na hivyo kusababisha vijiji vengine kutofaidika na huduma za hospitali hiyo.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kujenga hospitali kubwa ya Mkoa wa Kusini katika eneo la Tunguu ambayo itanufaisha vijiji vyote vya Mkoa huo badala ya kuitegemea hospitali ya Makunduchi ambayo ipo mbali kwa baadhi ya vijiji vya Mkoa huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Afya, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Baraza lako Tukufu suala lake Nam. 33, kama ifuatavyo;-
Mhe. Spika napenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba serikali yake bado ina nia hiyo hiyo ya kuhakikisha kwamba inawasogezea huduma za afya wananchi wake. Ndio mana inajitahidi kuimarisha vituo vyake vya afya, na hospitali hizo za Wilaya kwa kuongeza huduma kama kuwekewa damu wagonjwa, kufanyiwa opersheni za uzazi katika hospitali hizo.

Pia serikali katika ilani yake ya uchaguzi imeelekeza kuwa na hospitali hizo kwa kila Wilaya. Si hivyo tu ili kufikia huduma hizo pia serikali imeimarisha miundo mbinu ya barabara ili wananchi wake waweze kufika katika hospitali na vituo hivyo. Kwa Makunduchi, sasa kuna barabara ya mzunguko ambapo wagonjwa kutoka katika vijiji vingi vya Wilaya ya Kati, Kusini ukanda wa pwani na juu wanaweza kufika Makunduchi bila ya matatizo.

Mhe Spika, Serikali tayari imeshatenga eneo huko Binguni kwa ajili ya ujenzi wa hospitali kubwa mpya wakati utakapowadia na michoro ya hospitali hiyo ipo tayari. Tatizo linalokwamisha ujenzi huo ni ukosefu wa raslimali fedha na wafanyakazi wakati itakapomalizika

Ila wazo la Mwakilishi la kutaka Serikali ifikirie kujenga hospitali kubwa katika eneo la Tunguu, kwa kweli ipo haja hiyo na hasa ukitilia maanani kwamba mji wa Tunguu unakua na utahitaji hospitali kubwa kwa ajili ya mji huo na pia vile vijiji vya Mkoa wa Kusini ambavyo haviko karibú na Makunduchi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Waziri kwanza nikushukuru kwa majibu yako mazuri.

(a) Kwa kuwa silka kuwa ni mama na wajawazito ambao wanaishi mbali na hospital ya Makunduchi. Je, serikali ina mpango gani wa kuomba mkopo kutoka taasisi yoyote ya fedha ili hospital hiyo iweze kujengwa haraka.

(b) Kwa kuwa kuna vituo vijijini katika baadhi ya vijijini, serikali ina mpango gani wa kupeleka gari mfano kama aina ya *ambulancia* ili kupeleka wagonjwa wanapozidiwa kwa haraka na kwa wakati muafaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika,

(a) Hospital ya Makunduchi sasa hivi najengwa. Kuna wafadhili ambao wanaifanyia kazi na inamabadiliko kama anaifahamu hospital ya Makunduchi ilivyokuwa na sasa hivi ilivyo. Na inaendelea kwa sababu haijamalizika. Kwa hiyo hakuna haja ya serikali kuchukua mkopo mwengie kujenga hospital hiyo hiyo. Tuwaachie wanayoijenga waimalizikie.

(b) Kwa kawaida *Ambulanci* zinakuwa katika hospitali ya za Wilaya, na kijiji ambacho kinatatizo kinatakiwa kipige simu katika hospital ile ili *ambulanci* iwafuate. Kwa upande huo wa Makunduchi wao wanafanya hivyo. Kwa upande wa Kivunge watu kwa kawaida huwa wanachukua wagonjwa wanawapeleka Kivunge. Kama Kivunge wakihisi kwamba limeshindikana ndipo ambulanci inapotumika kumchukua mgonjwa yule na kumpeleka hospital ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo huo ndio utaratibu uliopo

Nam. 20
Maeneo ya Wazi Kuzuiliwa Kujengwa

Mhe. Mohammed Haji Khalid - Aliuliza:

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mara baada ya kuteuliwa kushika wadhifa huo alifanya ziara katika sehemu mbali mbali za Mkoa wa Mjini/Magharibi kuona hali ya ujenzi katika sehemu za wazi ambazo haziruhusiwi kisheria kujengwa. Katika eneo la Mombasa aliona sehemu ya wazi imejengwa na akatoa tamko kuwa ujenzi huo usimamishwe.

(a) Je, tamko hilo la Serikali limetekelezwa.
(b) Kama halikutekelezwa kwa nini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Spika kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam**.** 20 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kufuatia tamko la serikali, wizara yangu imetekeleza kwa kuzifuta hati zote zilizohusika katika eneo hilo na nakala za barua hizo zimepelekwa katika Afisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi pamoja na Baraza la Manispaa, kwa kuwa taasisi hizo ndizo zenye mamlaka ya kutoa vibali vya ujenzi na kuzuwia ujenzi kisheria.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya swahiba wangu, naomba kumuuliza suala dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, ni hatua gani za kinidhamu zimechukuliwa kwa wafanyakazi waliosababisha kadhia hiyo katika eneo lile.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kujibu suala la nyongeza na kumsaidia Mhe. Naibu Waziri wangu kama alivyojibu suala mama.

Hatua za kinidhamu zilizochukuliwa baadhi ya wafanyakazi wamehamishwa na baadhi ya wafanyakazi wamepwa onyo la maandishi. Kwa kosa la kutoa viwanja maeneo ambayo yasingepaswa kutoa viwanja.

Nam. 57

Uchakavu wa Bandari ya Mkoani

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Aliuliza:

Bandari ya Mkoani ndio Bandari Kuu kwa Kisiwa cha Pemba kwa shughuli za usafiri. Lakini sehemu kubwa ya gati ya Mkoani inakaa maji ambayo ni machafu na hupelekea usumbufu mkubwa kwa watumiaji hasa tukizingatia kuwa zile sehemu ambazo ni kavu huwekwa gari.

Je, Mhe. Waziri, Wizara yako ina mpango gani wa kulitatua tatizo hili ili kuwaondoshea usumbufu watumiaji wa Bandari hii ikiwemo pia kulinda afya zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 57 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa kipindi kirefu gati ya Mkoani – Pemba imekuwa ikikabiliwa na tatizo la kutuama kwa maji wakati wa mvua zinaponyesha. Hali hiyo imetokana na kudidimia sehemu ya katikati ya gati hiyo, ambapo imekua akilileta usumbufu kwa kipindi kirefu.

Mhe. Spika, katika jitihada za kuliondosha tatizo hilo, Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari hivi sasa inaendelea na kazi ya matengenezo makubwa ya

gati hiyo ili kurekebisha hali hiyo na kuondoa kabisa tatizo la kutuama kwa maji bandarini hapo. Kazi hiyo ilianza katika mwezi wa Septemba, 2011 na inahusisha ukataji wa zege katika eneo lililodidimia na baada ya kukamilisha ukataji kuweka ujazo mpya wa zege ili kusawazisha eneo lote. Kazi hiyo inategemewa kukamilika katikati ya mwezi wa Februari, mwaka huu wa 2012.

Mhe. Spika, wakati matengenezo hayo yakiendelea tunaomba kutoa wito kwa watumiaji wote wa bandari ya Mkoani kutoa mashirikiano yanayohitajika hasa kwa wakati huu wa matengenezo ili kuondoa usumbufu na kuweka mazingira ya usalama kwa watumiaji wa bandari na wafanyakazi wanaoendelea na shughuli hiyowote

Nam. 40

Ufinyu wa Posho la Kuzuia Magendo

Mhe. Hamza Hassan Juma - Aliuliza:

Katika kupambana na magendo ya karafuu Serikali imeamua kutoa posho askari wanaofanya kazi ya ulinzi wa zao hilo, lakini kuna malalamiko kwa Askari kwamba posho waliopangiwa ya kujikimu ni ndogo sana hailingani na ugumu wa kazi wanayoifanya.

(a) Je, Wizara yako imewahi kupokea malalamiko hayo.
(b) Kama imewahi, Je, imechukua hatua gani.
(c) Kwani hiyo posho inayolalamikiwa ni kiasi gani kwa siku kwa mtu mmoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 40 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba serikali iliamua kuweka ulinzi katika maeneo ambayo kwa uzoefu yalikuwa ndio njia kuu ya Magendo ya karafuu, kwa lengo la kudhibiti zoezi hilo haramu ambayo iliathiri uchumi wa nchi yetu kwa kiasi kikubwa na askari walioteuliwa kufanya kazi hiyo hupewa posho maalum ya kujikimu.

(a) Mhe. Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, imewahi kupokea malalamiko kwamba posho wanayolipwa askari hao ni ndogo ukilinganisha na kazi yenyewe.

(b) Mhe. Spika, Wizara yangu baada ya kupokea malalamiko hayo iliyalepeleka katika vikao vya Kamati ya Vikosi Kazi yaani *(Task Force)* kwa mazingatio ambapo wakuu wote wa vikosi vya ulinzi vya hapa Zanzibar ni wajumbe, kwa pamoja walikubaliana kwamba posho hiyo ibaki kama ilivyo. Kwa kuwa ni kwa ajili ya kujikimu tu, huduma nyengine kama vile matibabu wanahudumiwa.

(c) Mhe. Spika, posho linalolalamikiwa ni Tshs. 5,000/= kwa chakula kwa siku na Tshs. 1,000/= kwa huduma ndogo ndogo, kwa jumla kwa siku wanalipwa Tshs. 6,000/= kwa kila askari.

Nam. 43

Maghala ya Serikali

Mhe. Hamza Hassan Juma - Aliuliza:

Serikali yetu ilikuwa ina miliki maghala mengi ya Akiba ya Chakula pamoja na yale ya kuhifadhia karafuu na bidhaa nyengine. Kwa muda mrefu sasa maghala hayo yamekuwa yakitumiwa na Matajiri au Wafanyabiashara binafsi. Katika hali hiyo tunashindwa kujua ni maghala mangapi bado yanamilikiwa na Serikali ya Mapunduzi Zanzibar na mangapi yameuzwa.

(a) Je, Serikali ilikuwa na maghala mangapi kabla ya kuanza kuyauza.
(b) Tangu harakati za kuyatoa kwa watu binafsi zianze yameuzwa maghala mangapi.
(c) Hayo yaliyouzwa yameuzwa kiasi gani na wameuziwa akina nani (watu au Kampuni).

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 43, lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nikubaliane naye tena na Mhe. Mwakilishi kuwa ni kweli serikali ilikuwa inamiliki maghala mengi ya hakiba ya chakula pamoja nay ale ya kuhifadhia karafuu na bidhaa nyenginezo

(a) Serikali ilikuwa ina maghala 49 kati ya hayo 24 yanamilikiwa na Shirika la ZSTC hadi leo hayajauzwa. Kwa upande wa maghala ya hakiba ya chakula jumla yalikuwa 7, kati ya hayo maghala 4 yapo Unguja na maghala 3 yapo Pemba.
Maghala ya Unguja yalikuwa yanatumika na yapo Saateni ambayo ni mali ya ZSTC nayo ni 2 na hadi sasa ni mali ya ZSTC. Maghala

mawili yapo Bandarini ambayo yaliazimwa kutoka Zanzibar Worfeg kwa ajili ya chakula kinachokuwa kinasafirishwa kupelekwa Pemba. Baada ya Shirika la Bizanje kusimamisha huduma zake maghala hayo yamerejeshwa Shirika la Bandari ambao ndio wamiliki.

Kwa upande wa Pemba Mhe. Spika, Maghala tatuzo yaani ghala la hakiba Mkoani na maghala mawili ya hakiba yaliyokuwepo Kizimbani Wete bado ni mali ya serikali. Sasa maghala hayo yanatumika kama Afisi ya Vitega Uchumi Zanzibar chini ya Afisi ya Raisi, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

(b) Mhe. Spika, naomba kumjibu suala lake hilikama ifuatavyo. Tangu Shirika la Bizanje kusimamisha biashara zake kwa wananchi, maduka na maghala madogo saba yameuzwa. Pia maduka mengine yaliyobaki yametolewa kwa makubaliano ya kujenga maghalal mengine ya chakula cha hakiba hapo Maruhubi ambapo hivi sasa kwa nia njema serikali inapatumia kuwa ni Afisi ya Mamlaka ya Vitega Uchumi yaani (ZIPA).

(c) Mhe. Spika, ambayo yameuzwa kwa watu binafsi kwa jumla ya shilingi milioni 80 na laki 5 ni kama haya yafuatayo.

1. Ghala iliyokuwepo Konde Pemba, ameuziwa ndugu Ibrahim Shaib Khamis kwa barua yenye kumbukumbu Nam. WUBU/P4/3/3/VOL 11/172007 ya tarehe 21 mwezi wa 6 mwaka 2007 kwa jumla ya shilingi milioni 8 za kitanzania.

2. Ghala nyengine lililokuwa Chake Chake Pemba limeuzwa kwa barua yenye kumbukumbu Nam. WBVM/P4/5/11/23 ya mwaka 2004 tarehe 24 mwezi wa 12 na ameuziwa ndugu Mohammed Ali Aboud wa Chakechake Pemba kwa jumla ya fedha za kitanzania shilingi milioni 27.

3. Ghala Nam. 1214A na nambari 1213A yaliopo Kokoni Wilaya ya Mjini Unguja yameuzwa kwa thamani ya Shilingi milioni 25 za Kitanzania kwa mkataba wa *saled* yenye *registration* Nam. 248 ya mwaka 1997 ambayo imesajiliwa kwa *Volume* 1 ndani ya kitabu (a)(b) ya mwaka 1997 na ameuziwa ndugu Mohamme Hemed Mohammed wa sanduku la posta 177, Zanzibar.

4. Maghala mengine ni pamoja na *plot* Nam. 889 na 888 lililokuwepo Malindu Unguja ambayo aliuziwa kwa *saled* nyengine yenye usajili Nam. 68 ya mwaka 2004, volume 1 kitabu

A2 ya terehe 10 Machi 2004 ambayo *plot* hizi ziliuzwa kwa jumla shilingi milioni 10 na laki 5 za Kitanzania na aliyeuziwa ni ndugu Abul-latif Jussa Sadiq wa Zanzibar.

5. Ghala nyengine Mhe. Spika, kauziwa ndugu Mohammed Said Mahfoudh wa Zanzibar kwa *saled* ya tarehe 19 Oktoba mwaka 2000 yenye *registration* Nam. 382, Vole 11 tarehe 19 Oktoba mwaka 2000 kwa thamani ya shilingi milioni 10 za Kitanzania. Ghala hilo lilikuwa na vitu vya ujenzi hapo malindi.

Mhe. Spika, kwa ujumla baada ya Shirika la Bizanje kusimamisha huduma za kuwauzia wananchi mahitaji muhimu kwa kufuatia sera ya Biashara Huria iliamua kutoa yaliyokuwa maduka na maghala yake 15 ili kujengewa maghala mengine 4 ya hakiba ya chakula huko Maruhubi. Ambayo kama niliposema hapo awali maghala hayo hivi sasa yanatumika na Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar. Aidha maghala mengine 10 bado ni mali ya serikali kati ya hayo maghala matatu yapo Unguja na maghala 7 yapo kisiwani Pemba.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kuweza kujibu suala langu kwa ufasaha mkubwa sana na nadhani waheshimiwa wengi wameridhika na majibu aliyoyatoa Mheshimiwa.

(1) Mhe. Spika, kwanza nilikuwa nataka nijue haya maghala ambayo mpaka sasa hivi bado yamo mikononi kwa serikali yamekodishwa na yanaendelea kukodishwa. Nilikuwa nataka nijue kwamba yamekodishwa kwa mkataba wa miaka mingapi mingapi na ni mwaka gani ambao yamekodishwa na hiyo kodi kwa thamani gani, aidha kwa mwezi au kwa mwaka.

(2) Mhe. Spika, ameeleza Mheshimiwa haya maghala ambayo yameuzwa milioni 8, milioni 27, milioni 25, milioni 10, nilikuwa vile vile nataka nijue haya maghala ambayo yaliuzwa, yaliuzwa mwaka gani.

(3) Je, serikali haiyoni kwamba kuuza maghala ni kujipunguzia uwezo pale inapohitaji kuweka hakiba zake au kuweka mali zake, sasa itabidi wakodi kwa watu binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante Mhe. Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Masoko naomba nimjibu Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura aliyechaguliwa kwa kura nyingi sana masuala yake mawili ya nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, suala la kukodishwa kwa mahala halijakuwepo katika suala la msingi. Na kwa kuwa ametaka kujibiwa kwa kina kama nilivyojibu haya yaliyouzwa basi nitamletea kwa maandishi.

(b) Ametaka kujua kwanini maghala haya yameuzwa. Mhe. Spika, katika jibu langu nimesema kwamba kuuzwa kwa maghala haya imefuatia kusitishwa kwa shughuli za kuleta bidhaa hapa nchini na Shirika la bidhaa nnje. Kwa maana hiyo kubinafsishwa kwa watu binafsi biashara yote ya chakula. Hiyo ndiyo iliyokuwa sababu ya msingi.

(c) Lakini katika majibu yangu kila ghala lililouzwa nimetaja barua na mwaka wa kuuzwa pamoja na kumbukumbu ya barua iliyotumika katika kuuza kila ghala.

Mhe. Omar Ali Shehe: Nashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, nina taarifa kwamba ghala kubwa la ZSTC lililokuwepo Kibirinzi/ Chake Chake kauziwa mfanyabiashara kwa ajili ya kuweka ghala ya pombe katika kisiwa cha Pemba na ndio ghala kuu la Pombe katika kisiwa cha Pemba.

(a) Sasa wakati serikali ina tatizo kubwa la maghala na inatatizo kubwa la majumba, maana yake yale yale maghala tunaweza tukayageuza majumba kuwa ni Ofisi. Ni sababu zipi hasa za msingi zilizopelekea serikali kuyauza maghala haya kwa watu binafsi.

(b) Uuzaji si barua tu uuzaji wa mali za umma unatakiwa ufuate taratibu pamoja na sheria zilizowekwa. Je, itakapobainika kwamba uuzaji huu haukuata sheria na haukufuata maslahi ya umma, Je, wahusika watakuwa tayari kuwajibika.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, suala la kwamba ghala kubwa lililokuwepo Tibirinzi Pemba limeuzwa kwa mfanyabiashara ili liwe ghala kubwa la kuweka Pombe, taarifa hiyo Wizara hatuna na kwa hiyo nitamuomba Mhe. Mwakilishi tushirikiane kwenye kulifanyia kazi hilo. Lakini Mhe. Spika, sababu ya kimsingi kama nilivyojibu kwenye suala langu mama. Ni pale serikali ilipoamua Bizanje ijitoe kwenye masuala ya biashara, ndio sababu iliyopelekea baadhi ya maghala kuuzwa. Yapo maghala ambayo yamebaki kwenye mikono ya serikali, yakiwemo yale ya ZSTC na mengine ambayo kwa sasa yanatumika kama ofisi za vitega uchumi na ZIPA.

Mhe. Spika, uuzaji umefuata sheria na tutakumbuka Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wakati anajibu suala lake, utaratibuu

unaofuatwa na serikali kwenye kuuza mali zake wakati anajibu uuzwaji wa nyumba za serikali alisema kuna taratibu zimewekwa katika mifumo mitatu. Namuomba Mhe. Mwakilishi arejee *hansard* ile na atajua utaratibu upi hasa uliofuatwa katika kuuza maghala haya..

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri suala la nyongeza. Katika azma ya serikali ya kujenga maghala ili kuondoa matatizo wananchi wake.

Micheweni kulijengwa ghala kwa nguvu za wananchi kwa kushirikiana na serikali. Lakini kwanza ghala lile Mhe. Waziri kalisahau hakulitaja. Ghala lile sasa hivi lipo na linafaitika nguvu za wananchi pamoja na serikali, sasa hivi linatumika kwa kuwekea vifaa vya Tume ya Uchaguzi masanduku na madude mengine. Ghala hili linatumika miaka mitano mpaka miaka mitano.

(a) Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kama zile nguvu za serikali na wananchi zinafaitika?

(b) Na je, wale Tume ya Uchaguzi wanaopewa kuweka yale masanduku wamekodishwa na Serikali, wameuziwa au wamepewa tu.

(c) Na je, ghala lile ili kuliokoa nguvu za wananchi ili zisipotee anashauri vipi na litatumika vipi ili lisitumike miaka mitano mpaka miaka mitano.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, nimesema katika jibu kwamba maghala mengine yamebaki kwa kazi za serikali, likiwemo hili ghala la Micheweni. Kama wanaweka vifaa vya uchaguzi basi ni miongoni mwa vifaa vya shughuli za kiserikali kwa ajili ya kumbukumbu zisije sikapotea Mhe. Spika, nakushukuru.

Nam. 34

Upandaji wa Miti ya Mivinje na Mikaratusi

Mhe. Salma Mussa Bilali (Kny: Mhe. Salma Moh'd Ali) - Aliuliza:

Kuna taarifa kwamba miti ya Mivinje na Mikaratusi inapoteza maji kwa kiwango kikubwa kutoka ardhini na kuyaingiza katika mkondo wa hewa na kuifanya ardhi kupoteza maji mengi na kukosa rutba, na hivyo kurudisha nyuma maendeleo ya kilimo katika maeneo inayopandwa miti hiyo.

Kutokana na matatizo hayo baadhi za Wilaya za Tanzania Bara zimeanza kupiga marufuku upandaji wa miti hiyo na kuikata katika maeneo iliyopandwa.

(a) Mhe. Waziri, Wizara yako imefanya utafiti wowote ili kuthibitisha dhana hiyo.

(b) Kwa kuwa miti hiyo inapopandwa kwa wingi katika maeneo mbali mbali hasa mivinje, kwa ajili ya biashara ya miti na mikaratusi kwa kutengenezea arki, huoni kwamba hilo ni tatizo kwa ardhi na mazingira yetu.

(c) Je, serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwaelekeza wananchi kupanda miti mingine badala ya hiyo, itakayowafanya kufikia malengo yao ya kujikimu kimaisha bila ya kuleta uharibifu wa mazingira.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili) - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili naomba kumjibu Mhe. Salma Mohammed Ali, Nafasi Maalum za Wanawake, swali lake Nambari 34 lenye kipengele (a,b, na c) kama ifuatvo:-

Miti ya mivinje na mikaratusi asili yake nchini Australia. Miti hii imeletwa katika maeneo ya Afrika mwishoni mwa karne ya karne ya 19. Kuna aina kumi na saba (17) za miti ya mivinje na aina zaidi ya mia saba (700) za miti ya mikaratusi duniani ambayo inaota katika mazingira tafauti. Kwa hapa Zanzibar mivinje aina ya *Csuarina equisetifolia* na mikaratusi aina ya *Eacalyptus* ndio inayopandwa zaidi.

Mhe. Spika, miti ya mivinje na mikaratusi inafaida kubwa za kijamii, kiuchumi na hata kimazingira. Miti hii imekuwa ni vyanzo vikubwa vya mapato kwa wakulima hapa nchini. Mazao yanayotokana na miti hii yanasaidia kuinua mapato ya wakulima vijijini. Ujenzi wa mahoteli ya Kitalii umefaidika sana kutokana na mazao yanayotokana na miti hii.

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi kuhusiana na miti hii, sasa naomba kumjibu Mwakilishi masuala yake kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna manung'uniko mengi kuhusiana na miti ya kigeni katika suala la uhifadhi wa mazingira kwa ukanda wetu huu wa joto. Miti ya mikaratusi imekuwa ikipigiwa kelele sana

kwamba inaharibu mazingira kwa kunyonya maji na kukausha ardhi na wakati mwengine kuzuia baadhi ya kuota.

Mhe. Spika, wizara yangu bado haijafanya utafiti wa kutosha kuhusiana na suala hili hapa nchini kwetu, lakini kutokana na uzoefu tulionao baadhi ya miti ya mikaratusi ina tabia ya kuota na kukua haraka sana, hivyo kutumia kiwango kikubwa cha maji. Mfano mikaratusi aina ya *Eucaltyptus grandis* inakuwa haraka sana na kunywa maji mengi, hivyo hata wenzetu wa Kenya hawapendelei kuipanda miti hii katika maeneo yenye vyanzo vya maji. Ni jambo zuri kuelewa kwamba, aina ya mikaratusi ambayo hapa nchini kwetu tunapanda haina tabia ya kunywa maji mengi na ndio maana inaweza kuota haata katika maeneo ya ukame (uwandaji maweni). Wizara yangu inajipanga kuweza kufanya utafiti wa kina kuhusiana na suala hili.

Mhe. Spika, aina ya miti ya mivinje haina athari kabisa na wala hausababishi kukauka kwa vyanzo vya maji. Kwa kawaida, mti wa mvinje ni mkavu na pia hauhitaji maji mengi wala chakula kingi kwa ajili ya kumea. Hivyo basi hauna tabia ya kufyonza maji mengi ardhini. Unaweza kustahamili mazingira ya ukame. Hii ni kutokana na maumbile yake ya ukavu kawaida mivinje hauwezi kumea vizuri katika maeneo yenye maji mengi.

a) Mhe. Spika, dhana ya kwamba miti ya mvinje na mikaratusi ambayo imekuwa ikipandwa kwa wingi kwa ajili ya biashara na utoaji wa mafuta (arki) hupelekea matatizo ya kimazingira. Dhana hii ni kweli katika mtizamo wa kimazingira kwani aina yoyote ya kiumbe hai ambacho kitaingizwa kutoka nje ya eneo lake la asili kinaweza kuleta taathira za kimazingira. Hii ni kwa sababu ili kiweze kuishi sehemu hiyo ni lazima kikabiliane na mazingira ya pahala hapo, na pia kujitengenezea mazingira yatakayokiwezesha kuishi. Hivyo basi, katika kufanya hivyo kuna uwezekano mkubwa wa kujijengea nguvu za ziada ili kupambana na mazingira halisi ya eneo hilo. Lakini katika kufanya hivyo na viumbe viliopo hapo navyo vinajenga uwezo wa kupambana na hali ya mazingira hayo.

b) Mhe. Spika, wizara yangu haiwashurutishi wananchi kupanda miti ambayo wao wenyewe hawaipendelei. Kwa maana hiyo wizara yangu inawashajiisha na kuwashauri wananchi kuzalisha na kupanda miti tofauti kulingana na nahitaji yao, ikiwemo ya matunda, kivuli, mapambo, viungo, kuni, majengo na malisho.

Mhe. Spika, kwa wale ambao watakaopenda kuipanda miti hii ya mivinje na mikaratusi kwa sababu za kibiashara ili kujikimu kimaisha wataendelea kupatiwa ushauri wa kitaalam juu ya maana ya kuendeleza upandaji wa miti kwa faida za kijamii na kimazingira**.**

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Kwa kuwa nchi yetu ni ndogo na ardhi kubwa sasa hivi inatumika kwa ujenzi na kuna ardhi zinazobaki kwa kilimo Mhe. Waziri katika jibu lake amekiri kwamba haujafanyika utafiti. Je, haoni haja sasa ya kufanyika utafiti huu ili kuzuia madhara makubwa ya baadae ya kuja kukosa chakula kwani wataalamu wengi wanasema kwamba maji chini ya ardhi yanapungua na kwa hivyo kadri ya miti hiyo itakavyokuwa tunaizoea ndivyo itakavyochukua maji chini ya ardhi na mazao yakawa yanakosekana.

b) Mhe. Waziri ulikiri kwamba Kenya wao wameipiga marufuku hiyo miti ya mikaratusi ya aina fulani. Je, wataalamu wetu wamewahi kupelekwa huko Kenya ili kujifunza na wao ni mikaratusi ya aina gani na njia gani wanazotumia ili kuweza kupata utaalamu huo ili kuweza kunufaisha nchi yetu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kwamba nchi yetu ni ndogo lakini nataka kusema pamoja na kuwa haujafanyika huo utafiti alioushauri ni kwamba kuna maeneo ambayo zamani yalikuwa hayawezi kutumika kwa kilimo kwa sababu ya ukosefu wa mvua. Lakini wenyeji wa pale wakapanda mivinje ile kazi ya miti ya kuhakikisha kwamba inasaidia kutoa *carbondioxide* yakutosha na kuifanya ile miti iweze kuja mvua katika maeneo yale. Kwa hivyo, sehemu hizo sasa hivi mvua zinapatikana na mvua zikipatikana maana yake ndio kilimo kinaweza kuendelea katika maeneo yale. Utafiti huu upo ushaonekana kabisa kwamba ukipanda miti mvua inakuja, kwa hiyo katika baadhi ya maeneo mvua zinapatikana kwa sababu kumepandwa miti tena miti ya mivinje.

Mhe. Spika, kwa hivyo nakubaliana na yeye kwamba utafiti tutauendeleza nitafanya utafiti zaidi ili kujua madhara yake tusije tukaingia katika hiyo hasara ambayo ameizungumza.

Mhe. Spika, Kenya wamepiga mapiga marufuku kupanda mikaratusi, lakini nilimwambia kwamba mikaratusi iliyopo duniani ni aina 700 kwa hivyo

mikaratusi maalum ambayo wamepiga marufuku Kenya ni kweli inasababisha ukame kwa haraka, lakini mikaratusi tunayotumia sisi hapa haisababishi ukame kwa haraka kwa sababu kuna aina nyingi ya mikaratusi katika dunia, mengine ndio ile inayotoa arki na mengine ni ile ambayo tunaitumia kwa mbao na mambo mengineyo.

Mhe. Seleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kukiri kwamba haujafanyika utafiti kwa hivyo hawezi kutoa fatwa kwamba mikaratusi hii inayofyoza na mikaratusi hii haijafyoza kwa sababu hawajafanya utafiti.

Mhe. Spika, kwa kuwa taaluma katika mambo ya miti inaonesha wazi kwamba mivinje pamoja na mikaratusi inakuwa na uwezo wa kufyoza maji katika ardhi na kupeleka katika majani na halafu tunayamwaga katika hewa aidha kupitia katika tundu zinazoitwa stomata au katika magome. Sasa Mhe. Waziri kwa kuwa serikali ilihamasisha mambo ya *transpiration*, serikali ilihamasisha suala la upandaji miti bila ya kufanya utafiti.

a) Je, atakubaliana na mimi kwamba sasa serikali ilifanya makosa kuwahamasisha wananchi kupanda miti bila ya kufanya utafiti.

b) Kwa kuwa miti hii ni tatizo je serikali ni lini itawahamasisha wananchi kupanda miti yenye asili ya kunde kwa sababu hii ina uwezo wa kufyoza *nitrogen* iliyoko katika hewa na kupeleka katika ardhi na hatimae kupatikana rutba.

c) Kuendelea wananchi kuwaruhusu kupanda mivinje na mikaratusi ambayo inapoteza mbolea na kufanya ardhi kuwa kame, haitorudisha nyuma ile adhma ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuboresha kilimo pamoja na ile SMT ya Kilimo Kwanza.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, katika jibu langu la msingi nilisema kwamba mikaratusi inafyoza maji, lakini mivinje haifyozi maji mengi kiasi hicho na kwa ushahidi uliopo katika baadhi ya maeneo watu wanapovuna mivinje wakapanda mahindi basi yanakuja kwa *speed* kubwa sana.

Kwa sababu *nitrogen* inakuwa inapatikana pale kutokana na majani yake, kwa hivyo inasaidia kwa upande mmoja hii mivinje, hii mikaratusi najua ina matatizo ya kufyoza maji mengi. Lakini mikaratusi tunayoipanda sisi haina uwezo mkubwa kama ile ambayo imekuwa ikipandwa kule Kenya. Kwa hivyo,

mimi sikubaliani kwamba serikali imefanya makosa kwa sababu jambo lolote ni vizuri kwanza ulijaribu halafu ndio utajua tatizo liko wapi.

Mhe. Spika, kwa hivyo, serikali haikufanya makosa imelijaribu na imeona kwamba itahitaji kufanya utafiti wa kina, lakini walioileta miti hii ambao sisi tumerithi hapa tangu wakati wa ukoloni walioileta bila shaka walifanya utafiti mdogo, sisi sasa hivi tutafanya utafiti mkubwa.

Mhe. Spika, vile vile sikubaliani na yeye kwamba tutakwenda kinyume na hili suala la Mapinduzi ya Kilimo, ni kwamba hatwendi kinyume tunajitahidi kuwafundisha wakulima wetu kilimo na kwa kweli wakitekeleza tunavyotaka tunawasaidia kuwapatia pembejeo na mambo mengineo ili tuweze kuendeleza kilimo na mwaka huu kidogo tumepata athari hizi mvua zilizokuja kati kati, lakini vyenginevyo yangelikuwa mabonde yote sasa hivi tushamaliza kuyachimbua.

Nam. 7

Watu Wenye Ulemavu wa Uziwi Kufaidika na Taarifa za Habari

Mhe. Raya Suleiman Hamad - Aliuliza:-

Mhe. Waziri unaelewa kwamba watu wenye ulemavu wa uziwi hawafaidiki na taarifa za habari zinazotolewa na *ZBC*. Kama ni hivyo Wizara yako ina mpango gani wa kuwafanya wafaidike sawa na watu wengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 7 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli watu wenye ulemavu wa uziwi hawafaidiki na taarifa za habari zinazotolewa na *ZBC*, hiyo ni kwa sababu ya kutopatikana hadi hivi sasa Mtaalamu mwenye kupasha habari kwa njia ya ishara. Mhe. Spika, katika kuona upungufu huo Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo mwaka huu wa fedha Shilingi 3,000,000/= zimetengwa maalum kwa ajili ya mtaalam huyo. Lengo ni kuwawezesha watu wasiosikia na wasioweza kusema wafaidike na baadhi ya vipindi vinavyotolewa na *ZBC*. Lakini hadi hivi sasa tunaendelea kumtafuta mtaalamu huyo, namuomba Mhe. Mwakilishi ikiwa anamfahamu mtaalamu wa aina hiyo atuarifu ili hatua za kumpata zianze kuchukuliwa.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Je, Mhe. Naibu Waziri huoni dunia sasa inaendelea na utandawazi na watu hawa nao ni watu wenye haki na fursa katika nchi hii, katika chombo hiki kitukufu tunachokijadili hapa wenzetu hawa na wao wana haki kama watu wote, lakini bado hatujapata mtaalamu huyu wa lugha ya alama katika chombo hiki. Je, ni lini utaweza kutufanyia jitihada ya kuweza kutuletea mwandishi wa habari anayetumia lugha ya alama ili kufaidika wananchi hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nasema kwamba maelezo yote niliyoyaeleza humu ni ya uhakika na nakuomba Mhe. Mwakilishi ukiwa ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia ulemavu basi tushirikiane mimi na wewe na wizara yetu ili kumtafuta mtaalamu huyu wakati wowote ule unapohitajika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa muda mrefu sasa tangu baada ya mapinduzi na kabla ya hapo dunia ilikuwa inatumia teknolojia ya *analogy* katika kutupatia habari na ni dhahiri kwamba walemavu wa aina hii hawakufaidika na teknolojia hiyo kwa miaka yote hiyo. Na kwa kuwa Katiba ya Zanzibar inasema wazi kwamba miongoni mwa haki za msingi ni watu kupata habari na kwa sasa dunia inaingia teknolojia mpya *digital*.

Je, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba kama itafika 2015 dunia ikiwa imeingia kwenye teknolojia hii ya *digital* ikiwa hawana wataalamu wa kuwapasha habari walemavu wasiosikia si itakuwa wanaendelea kuvunja Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kwamba juzi tu tulikuwa na semina tena semina imefahamisha vizuri sana na kuhusu mtaalamu wa ishara Mhe. Mwakilishi tunakuhakikishia inapofika 2015 mtaalamu huyo itakuwa ameshapatikana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa hawa walemavu wasiosikia ni miongoni mwa Wazanzibari na wana haki ya kufaidi na haki na mapendeleo ya serikali hii sawa sawa na walipa kodi wengine, na kwa kuwa haki ikichelewa kutolewa ni sawa na kwamba haikutolewa kabisa.

a) Je, kuendelea kuchelewa kuwapatia wataalamu wa mambo haya ya lugha za ishara si kuwanyima haki zao Wazanzibari hawa.

b) Na kwa kuwa wataalamu wa lugha za ishara wapo tele hapo Bara je isingekuwa vyema kwa wizara hii ikenda ikatafuta kijana hapo Bara angalau ule wakati wa taarifa ya habari katika *ZBC* angalau na hawa wenzetu wakaweza kusikia hiyo taarifa ya habari ya televisheni kwa kupitia wataalamu wa hapa hapa nchini ambao wanapatikana kwa wingi hapo Bara.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli nimetoa ufafanuzi mzuri kwenye swali mama na kwa kweli wizara yangu kama nilivyosema mwanzo nilipomjibu Mhe. Mwakilishi kuwa amtafute mtaalamu huyo na sisi tukiwa tuko mbioni kufanya juhudi hiyo.

HOJA ZA SERIKALI

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba kutumia Kanuni ya 42 (1) na 42 (3) na (5) ili uniruhusu kuwasilisha hoja ya kujadili jambo la dharura kuhusiana na maombi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kudai ukanda wa bahari kuu kama ambavyo tulikuwa tumelizungumza siku ya Ijumaa kabla ya kuahirisha kikao chako. Mhe. Spika, naomba ruhusa yako.

Mhe. Spika: Ni sawa lakini tutakwenda vizuri zaidi tukimaliza hili suala ambalo lipo ndani ya *order paper* la kumaliza hii hoja ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuna hatua fulani ambazo wizara wanataka kuchukua na kwa hiyo nilitaka tuondoe hilo alitochukua muda mkubwa, mara baada ya hilo basi hoja yako hii tutaruhusu sasa uiweke ili tupate muendeleo mwengine.

Kwa hiyo nikuombe tumalize hili suala la wizara kwa sababu nalo limechukua muda mrefu kidogo na kulikuwa na ahadi ambayo wananchi wanaisubiri kwa hiyo tujue tunaendaje juu ya hili halafu tena tutakwenda na hilo jengine.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Maslahi ya Viongozi wa Kisiasa ya 2011

(Kusoma kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, siku ya Jumatano tarehe 18/01/2012 niliwasilisha kwa mara ya kwanza Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kitaifa Nam. 4 ya mwaka 1988 na Sheria ya Viongozi wa Kisiasa

Nam. 6 ya mwaka 1999 na kutunga Sheria mpya ya Maslahi na Mafao ya Viongozi wa Kisiasa baada ya kustaafu pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, baada ya kuwasilisha mswada huu michango ya Waheshimiwa Wajumbe ilifuata kuanzia Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura na baadae Waheshimiwa wengine walifuata.

Mhe. Spika, michango iliendelea takriban kwa siku mbili, siku ya Jumatano yenyewe ya tarehe 18/01/2012 na Alhamis ya tarehe 19/01/2012.

Mhe. Spika, kwa ujumla kulikuwa na michango 37, michango 11 kutoka kwa Waheshimiwa Wawakilishi ambao ni Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na michango 26 kutoka kwa Waheshimiwa wengine Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi maarufu kwa jina la *backbenchers.*

Mhe. Spika, sote tunakumbuka *backbenchers* wote waliochangia walieleza kutoridhika kwao na vifungu mbali mbali vilivyomo katika mswada niliowasilisha na kushauri kwamba serikali ifanye marekebisho katika vifungu hivyo kama ilivyoshauriwa katika ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu hapo ndipo watakapoweza kupitisha mswada huu. Waheshimiwa Mawaziri kama serikali walijitahidi kutoa ufafanuzi mwingi katika vifungu mbali mbali, lakini bado ufafanuzi huo ulionekana kutofahamika barabara na kuweza kukubalika kwa Waheshimiwa Wawakilishi wengi wa *backbenchers*.

Kwa mantiki hii Mhe. Spika, ni busara na hekima lazima zitumike katika kuchambua tena mswada wangu na kurejesha maelewano na maafahamiano mazuri yaliyojengeka siku zote katika Baraza letu wakati wa kupitisha mswada.

Mhe. Spika, kwa kuwa lengo letu sote nikufanikisha suala hili basi Mhe. Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi kifungu Nam. 85 (1) naomba kuahirisha kutoa majumuisho yangu ya mswada huu hii leo mpaka katika kipindi kijacho cha Baraza.

Mhe. Spika, naomba kusisitiza kwamba mswada hauondoshwi ila ninachofanya nikuahirisha kutoa majumuisho hii leo ili kupata fursa ya kuwasilisha mabadiliko ya mswada kwenye kamati iliyopitia mswada huu kwa lengo ambalo kwa pamoja serikali na Waheshimiwa Wawakilishi wapate kuelewana zaidi na kukubaliana katika mapendekezo yao kwa faida ya nchi yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nafikiri Mhe. Waziri amefahamika vizuri makofi haya na dalili hii inaonekana kuunga mkono jambo hili kwamba mswada huu urejeshwe kwenye kamati kwa sababu hapo nyuma tukikumbuka kwamba kulikuwa na maombi kwamba serikali ingeondoa mswada huu, lakini kuundoa mswada maana yake umefuta mazungumzo yote yale yaliyokwishatolewa na wajumbe kama 37 pamoja na taratibu nyengine zote za kuwasilisha hati na kuwasilisha mswada huu inakuwa unaziondoa.

Kwa hivyo, nadhani wananchi wanaweza wakauliza hivi imekuaje mswada huu uliwasilishwa watu wakazungumza pale kwa mapana na marefu halafu leo unaondolewa wanaanza tena, hii nini hii.

Kwa hivyo, kuondoa hiyo mashauri aliyokuja nayo ni hayo kwamba jambo hili lirejeshwe kwenye kamati, najua Kamati za Baraza zinasaidia kuweza kufanya kazi kwa karibu zaidi kuliko kwenye sura za Baraza namna hii, ili kile ambacho kitazungumzwa huko wakaelewana huko baadae kinaweza kikawekwa katika utaratibu baadae yakaja haya majumuisho. Nadhani fikra nzuri kama mlivyopiga makofi na hiyo moja kwa moja kuwa hili jambo mnaliunga mkono.

Lakini pili, kuna ndugu yetu hapa *camera man* mpya ameingia wa *Channel Ten* ambaye anaonekana yupo. Ameomba ruhusa na nimemruhusu, ndio maana nikamwambia Mhe. Ismail Jussa asubiri kidogo kwa sababu hili suala huko nje wananchi wanalisubiri sana. Mwandishi wa habari huyu ameomba ili atoe taarifa hii kwa wananchi kuwa limefikia wapi kwa vizuri na kwa maelewano kiasi gani aingie asikie hili pamoja na hilo jambo jengine ambalo tumeahirisha kidogo mpaka baada ya shughuli hii.

Masuala hayo yote ni muhimu na anapopata matangazo mazuri, narejea, matangazo mazuri kwa wananchi maana yake wananchi watakuwa wanaelewa zaidi nini tulichofikia. Kwa hivyo, ndugu yangu huyu aliomba na nimemruhusu aingie kwa sababu ya mtazamo huo.

Baada ya hayo nadhani *actually* hii ni taarifa na wala sio hoja, kwa hivyo ni kutoa *ruling* tu, na kwa mwelekeo huu nadhani hakuna tatizo.

Kwa hivyo, nakubali kwamba jambao hili lirudi kwenye kamati na kule mtaangalia kwa ukaribu pamoja na serikali ili hatimaye kikao kijacho iwe ni shughuli ya kwanza kumaliza jambo hili kabla ya shughuli nyengine ambazo zitakuwemo katika orodha yetu wakati huo.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kuonesha mwelekeo mzuri na njia ya kuendelea mbele ili kumaliza shughuli zetu kwa pamoja na kwa maelewano makubwa nanma hii.

Wakati wa mjadala wa jambo hili nilitumia neno kisaidieni kiti, msaada kama huu ni mzuri nawashukuru sana. Baada ya hayo niseme tu kwamba mswada unarudi katika kamati inayohusika ili kumaliza masuala hayo na hatimaye kuletwa kwenye mkutano ujao. Nashukuru.

Sasa tunaendelea, niliahirisha kidogo suala la Mhe. Ismail Jussa lakini sasa Mhe. Jussa wakati ni wako karibu.

HOJA YA KUJADILI JAMBO LA DHARURA

(CHINI YA KANUNI YA 42 (1), (4), (5), (9) na (10) YA KANUNI ZA BARAZA LA WAWAKILISHI, TOLEO LA MWAKA 2011)

KUHUSIANA NA HATUA YA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUWASILISHA MAOMBI KWENYE UMOJA WA MATAIFA (*UN*) YA KUTAKA KUONGEZEWA UKANDA WA BAHARI KUU *(EXTENDED CONTINENTAL SHELF)* IKIWA NI NYONGEZA YA ENEO LA UKANDA WA UCHUMI BAHARINI *(EXCLUSIVE ECONOMIC ZONE - EEZ)* KWA ZIADA YA MAILI ZA BAHARINI *(NAUTICAL MILES)* 150 BILA YA KUZINGATIA MAAZIMIO YA BARAZA LA WAWAKILISHI YA MWAKA 2009

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kutupa neema yake ya uhai na afya tukaweza kuendelea na shughuli zetu muhimu zinazogusa maisha ya nchi yetu ya Zanzibar na watu wake.

Mhe. Spika, kwa kutumia Kanuni ya 42 (1), (4), (5), (9) na (10) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2011, na kufuatia ruhusa ulioitoa katika kikao cha tarehe 20 Januari, 2012, nina heshima kubwa kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar tunaowawakilisha hapa, lakini nitoe heshima maalum kwa wananchi wa Jimbo la Mjimkongwe walionipa heshima ya kuingia katika chombo hiki na kuwawakilisha katika chombo chao hiki kitukufu kuwasilisha hoja hii ya kujadili jambo la dharura kuhusiana na hatua ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwasilisha maombi kwenye Umoja wa Mataifa ya kutaka iongezewe eneo la ukanda wa Bahari Kuu, *(Extended Contintental Shelf)* kwa ziada ya maili za baharini *(nautical miles)* 150 ikiwa ni nyongeza ya ziada ya eneo la maili za baharini *(nautical miles)* 200 za *Exclusive Economic Zone* (*EEZ*) zilizokwisha tolewa katika mwaka 1989.

Mhe. Spika, kanuni ya 42, fasili ya (10) inaeleza kwamba, “Kwa madhumuni ya Kanuni hii jambo lolote litahesabiwa ni muhimu kwa umma iwapo litagusia

maslahi ya nchi au wananchi wake na utatuzi wake utategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kiutawala peke yake".

Mhe. Spika, kwa maoni yangu na naamini maoni ya Waheshimiwa Wajumbe wengi wa Baraza hili tunaamini jambo hili linatimiza masharti hayo.

Mhe. Spika, taarifa za kuwepo maombi haya tulizipata tarehe 16 Januari, 2012 pale Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Prof. Anna Tibaijuka, alipofanya mkutano na waandishi wa habari mjini Dar es Salaam na kueleza dhamira hiyo. Likiandika taarifa za mkutano huo, gazeti la Nipashe la mjini Dar es Salaam la tarehe 17 Januari, 2012, lilieleza:

> "Tanzania imetangaza kuwasilisha maombi Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa (*UN*), jijini New York, nchini Marekani, kudai umiliki wa eneo la ziada nje ya maili 200 za Ukanda wa Kiuchumi Baharini (*EEZ*) katika Bahari Kuu ya Hindi, ili iweze kulifanyia utafiti zaidi kuhusu rasilimali zilizoko chini ya bahari kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi".
>
> Kwa mujibu wa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Profesa Anna Tibaijuka, rasilimali hizo ni pamoja na mafuta, gesi na madini.
>
> Eneo hilo linatokana na ongezeko lingine tena la maili 150 na hivyo kufanya jumla ya mpaka hadi maili 350, ambazo ni sawa na kilomita 560 kutoka kwenye '*baseline'*. Waziri Tibaijuka alisema, "Maombi hayo yanatarajiwa kupelekwa na jopo la wataalamu kutoka Tanzania Bara na Zanzibar na wajumbe wawili kutoka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, litaongozwa na Waziri Tibaijuka."

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Andiko la Kitaalamu lililowasilishwa Umoja wa Mataifa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusiana na maombi hayo na ambalo liliwasilishwa rasmi tarehe 18 Januari, 2012 na ambalo nimebahatika kupata nakala yake, eneo hilo la ziada lililoombwa litakuwa sawa na kilomita za mraba 61,000 katika ukanda wa Bahari Kuu. Aliyewasilisha si waziri anayesimamia mambo ya Muungano kwa sababu ardhi, nyumba na maendeleo ya makaazi, vyote si mambo ya Muungano.

Mhe. Spika, ukiangalia ramani ya eneo lililoombwa ambayo inapatikana kwenye ukurasa wa 13 wa Muhtasari (*Executive Summary*) ya andiko hilo. Mhe. Spika, nitaomba baadae nikukabidhi hii *executive summary* uipate, na

ambayo kwa faida ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu, nimeiambatanisha pamoja na maelezo ya hoja hii, utagundua kuwa sehemu kubwa mno iliyoombwa ni eneo la bahari kuu ambalo kimsingi liko upande wa mashariki wa visiwa vya Unguja na Pemba. Ndiyo kusema mwenye haki ya kuomba eneo hili na kufaidi rasilimali zilizomo (ikiwa zimo alizozitaja Mhe. Tibaijuka za mafuta, gesi na madini) ni nchi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Katiba ya Zanzibar Ibara ya 1 inaeleza na naomba kunukuu:-

"Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vilivyoizunguka na bahari yake, ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar"

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu katika kikao chake cha tarehe 08 Aprili, 2009, (Baraza la Saba, Mkutano wa Kumi na Tano), lilikuwa na mjadala mzito wa siku tatu mfululizo kuhusu ***'Taarifa ya Mapendekezo ya Serikali kuhusu Ripoti ya Mshauri Mwelekezi juu ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia'*** *ambapo kutokana na uzito wake, wajumbe 49 wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri wengi wa wakati ule na pia Waheshimiwa Mawaziri wengi tulio nao sasa walichangia mjadala huo, tena kwa hisia kali za kizalendo na mapenzi ya kweli kwa nchi yetu tukufu. Baada ya mjadala huo, hatimaye wewe Mhe. Spika uliingia katika historia kwa kuwahoji Wajumbe kuhusiana na maazimio matatu yaliyowasilishwa na serikali.*

Azimio la tatu lilikuwa la aina yake na ili tujikumbushe hali ilivyokuwa naomba uniruhusu ninukuu moja kwa moja kutoka kwenye Taarifa Rasmi (Hansard) ya Baraza kwa siku hiyo ya tarehe 08 Aprili, 2009, ukurasa 71 – 72 kuhusu suala hilo kama ifuatavyo:-

Mazungumzo haya ulikuwa unayazungumza wewe Mhe. Spika.

"<u>Pendekezo la Tatu:</u>
Waheshimiwa Wajumbe naomba niwahoji wale wanaokubaliana na pendekezo la EEZ sehemu ya Bahari Kuu, serikali inashauri kwamba Wajumbe wakubali kwamba suala hili liende kwa mashirikiano ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wale wanaokubali pendekezo hilo wanyanyue mikono.

Wanaokubali pendekezo hilo…
Wanaokubali pendekezo hilo…

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kukataliwa)

Kwa hivyo, pendekezo hili lisahihishwe na inavyoonekana kufuatana na michango ya WaheshimiwaWajumbe kwamba eneo hili pia liwe katika mikono ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ni sawa ndio tunachokubali hicho?

Wajumbe: *Sawa.*

Mhe. Spika: *Wanyanyue mikono basi Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubali na wale wanaokataa.*

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: *Mhe. Spika naafiki.*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika kwa hivyo, pendekezo la eneo la Bahari Kuu katika suala zima la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi liwe katika mikono ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hayo ndio mapendekezo ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, yaliyopitishwa leo hii tarehe 08/04/2009 saa 7:00 mchana."

Mwisho wa kunukuu Mhe. Spika,

Mhe. Spika, nimekuomba ruhusa yako ninukuu sehemu hiyo ili Waheshimiwa Wajumbe tuelewe kilichoamuliwa na Baraza lako tukufu, na maamuzi hayo ni halali hadi wakati huu, kwa sababu hakujatolewa azimio jengine la Baraza la kuyafuta au kuyabadilisha.

Mhe. Spika, inaeleweka kwamba baada ya Baraza kupitisha azimio hilo na yale mengine mawili yaliyolitanguliaazimio hilo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kwa aliyekuwa Waziri Kiongozi wakati huo, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, iliiandikia rasmi Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Pinda, kuiarifu juu ya msimamo wa Zanzibar na kutaka hatua zichukuliwe kuyaondoa masuala hayo katika orodha ya mambo ya Muungano. Hilo halijatekelezwa hadi sasa ingawa kutokutekelezwa kwake hakubatilishi maamuzi ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, suala la kuihoji Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya hatua ilizofikia katika kusimamia utekelezaji wa maazimio hayo limekuwa likiibuliwa mara kwa mara katika mikutano ya Baraza lako hili. Mara ya mwisho wakati wa kikao cha Bajeti cha mwaka 2011, serikali iliwataka Waheshimiwa Wajumbe wawe wavumilivu na kuliacha suala hilo lije

litekelezwe wakati wa mjadala wa kupata Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hii nikumbushe Mhe. Spika, ilikuwa ni pamoja na pia kutwambia kwamba tuwape mwaka mmoja ili katika bajeti itakayokuja mwaka huu pia tutapata majibu ya kuridhisha juu ya suala hili.

Mhe. Spika, kwa msingi huo ingetegemewa basi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano isichukue hatua zozote zitakazopelekea kuyafanya maazimio haya ya Baraza la Wawakilishi niliyoyazungumza ambayo sasa ndiyo msimamo rasmi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yakawa hayana maana tena. Kitendo cha kupeleka maombi Umoja wa Mataifa kutaka kuongezewa ukanda wa bahari kuu ambao tayari Zanzibar ilishaamua kila upande isimamie wenyewe, ni kwenda kinyume na dhamira (*spirit*) hiyo na hakiashirii kuwepo kwa nia njema kwa upande huo.

Mhe. Spika, mimi binafsi na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu, tumeshtushwa sana na kauli ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Mhe. Ali Juma Shamuhuna, aliyoitoa kwenye Baraza hili siku ya Ijumaa ya tarehe 20 Januari, 2012 kwamba yeye hafahamu kuwepo kwa azimio hili, na kwamba yeye na wizara yake imeshirikishwa na imeshiriki kikamilifu katika kuandaa andiko lililofikishwa Umoja wa Mataifa. Bahati nzuri amekiri kwamba suala hilo amelifanya bila ya kulitaarifu Baraza la Mapinduzi ambalo kikatiba ndilo msimamizi mkuu wa maamuzi ya kisera kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, aliliomba Baraza kwamba suala hili ilivyokuwa halijafikishwa kwenye Baraza la Mapinduzi basi waachiwe serikali wakalijadili na halafu wataleta taarifa mbele ya Baraza hili katika kikao kijacho.

Kimsingi tulikubaliana na ombi hilo, isipokuwa kutokana na uzito wa suala lenyewe na jinsi lilivyogusa hisia za wananchi wa Zanzibar ambao ndiyo tunaowawakilisha hapa, tukaomba tupewe nafasi ya kulijadili kupitia hoja hii ya kujadili jambo la dharura na kupata fursa ya kutoa mapendekezo yetu ambayo tungependa Baraza la Mapinduzi liyazingatie wakati wanatafakari hatua za kuchukua.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa basi, nipendekeze kwa Baraza lako tukufu kwamba lilitake Baraza la Mapinduzi wakati wa kujadili suala hili lizingatie mambo yafuatayo:

1. Kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iiandikie rasmi Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitaka isimamishe mchakato wote wa maombi ya kutaka kuongezewa eneo la ukanda wa bahari kuu yaani (*Extended Continental Shelf*) kwa ziada ya maili za baharini (*nautical miles*) 150 ikiwa ni nyongeza ya ziada ya eneo la maili za baharini (*nautical miles*) 200 za *Exclusive Economic Zone* (*EEZ*) hadi hapo suala hilo litakapopatiwa ufumbuzi wakati wa mjadala wa Katiba Mpya.

2. Kwamba iwapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitochukua hatua za kusimamisha mchakato huo, hapa Mhe. Spika, naomba kidogo nirejee maneno ya Mzee wangu Mhe. Ali Mzee Ali aliyosema juzi kwam,ba, mara nyengine hujitokeza dharau ya kutotekelezwa maazimio yanayotoka hapa. Kwa hivyo nirejee Mhe. Spika, kwamba iwapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitochukua hatua za kusimamisha mchakato huo, basi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipeleke ujumbe wake na barua rasmi Umoja wa Mataifa kuutaka usimamishe kushughulikia maombi hayo hadi hapo suala la mchakato wa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano utakapomalizika na kukubaliana maeneo ya ushirikiano na maeneo ambayo kila upande utayasimamia wenyewe.

3. Kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iitake Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusitisha shughuli zote ambazo zinahusiana na kutumia rasilimali zilizomo eneo la ukanda wa bahari kuu (*EEZ*) hadi hapo suala hili litakapomalizwa baina ya pande mbili, na

4. Kwamba iwapo hatua hazitochukuliwa kuhusiana na mambo hayo, basi Zanzibar haitofungika na chochote kitakachoamuliwa kuhusiana na mambo hayo ambayo hayakushughulikiwa na Zanzibar yenyewe.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imewasilishwa na imeungwa mkono hiyo ikiwa na maana kwamba ijadiliwe. Kanuni inatuelekeza chini ya kifungu hicho hicho kwamba muda wa kujadili hoja kama hii ya dharura ni muda usiozidi saa moja. Tulikubaliana mapema kwamba hatutegemei kwamba serikali itoe majibu hivi sasa na ndio hata hoja yenyewe inavyoelekeza kwamba ikayafanyie kazi maombi haya ya mtoa hoja na tulijielekeza mapema kwamba ni vizuri basi tukajadili kwa kifupi kufuatana na taratibu za kanuni ili tujue *concern* za wajumbe ili zichanganywe pamoja na haya ambayo yameletwa

katika hoja hii ili iweze kuyafanyia kazi kwa pamoja na hatimaye huko mbele ndio ilete hiyo taarifa rasmi. Hiyo ndio *spirit* iliyokuwepo na ndio makubaliano yaliopo.

Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kwamba muda wa jambo hili uliowekwa kwa mujibu wa kanuni ni mfupi sana na kwa hiyo hivi sasa nina maombi ya wajumbe watatu, tutoe dakika zisizozidi kumi tukipunguza zidi ya hapo itakuwa vizuri na tusirejee rejee ili tupate mawazo zaidi ya kuichangia serikali ya kwenda kuyafikiria huko siku za usoni jambo hili litapofikishwa rasmi na serikali katika mikutano ya Baraza la Mapinduzi ambayo ndio utaratibu halisi.

Kwa hiyo, tujadili na naomba nimkaribishe Mhe. Hamza Hassan Juma kwa dakika kumi, hivyo tutakwenda kwa dakika kumi kumi.

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kunipa nafasi hii kuweza kuwa mchangiaji wa mwanzo wa hoja aliyoiwasilisha Mhe. Ismail Jussa kuhusu suala zima la Serikali ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuomba kuongezwa Maili 200 za ziada katika ukanda wa Bahari Kuu.

Mhe. Spika, kwanza nataka niseme kitu kimoja kabla sijaendelea na mchango wangu. Hivi karibuni wakati ulipotutuma kufanya shughuli za Kamati za Baraza nilikuandikia barua rasmi ya kukuomba kwamba kamati yangu iende Tanzania Bara na kutaka kuonana na uongozi wa *TPDC* kwa ajili ya kuangalia hatua au maendeleo ya uchimbaji wa mafuta hasa katika ukanda wa Tanzania.

Mhe. Spika, ulinileta tabu kidogo, lakini niliendelea kukuomba kwa sababu nilikuwa na hoja za msingi. Sasa hoja yangu ile Mhe. Spika, nilipokuwa mkaidi ulipokuwa unataka kujua nini tunataka kwenda kufanya *TPDC*, Mhe. Spika, suala hili ndilo ambalo tulikuwa tunataka kulifuatilia.

Kwa sababu tayari wenzetu kila walivyokuwa wakitafuta wakifanya utafiti wa uchimbaji wa mafuta ambapo kwa ile meli iliyokuweko katika ukanda wa Lindi na Mtwara tayari walikwishaanza kufanya huu utafiti na walikwishafika karibu mita 3500 bado mafuta hayajapatikana lakini dalili zilikuwa zinaonekana.

Kwa taarifa tulizokuwa tunazipata kupitia vyombo mbali mbali, kila wanapojaribu kufanya utafiti wenzetu wamegundua kwamba ukanda wa Bahari Kuu hasa ukanda ambao umepakana na mpaka wa Mombasa na visiwa vya Pemba imeonekana kwamba maeneo hayo kuna kiasi kikubwa cha mafuta

ambayo huenda yakapatikana. Sasa Mhe. Spika, ule ukaidi wangu kutaka lazima mimi niende kule nilikuwa nakwenda kuitafuta taarifa hii.

Mhe. Spika, hivi juzi baada ya sakata hili niliwaona Mhe. Waziri Mkuu akazungumzia dalili zilizojitokeza za upatikanaji wa mafuta katika ukanda wa bahari kuu hasa katika eneo lile nililolitaja mwanzo la baina ya Mombasa na visiwa vya Pemba na Unguja, Mhe. Spika, inaonesha huu ndio utaratibu wa kwenda kutafuta hiyo rasilimali.

Nakuja katika hoja yenyewe. Mhe. Spika, mimi juzi nilishangaa sana Mhe. Jussa alipouliza kuhusu suala la Tanzania kwenda kuomba kuongezewa maili zaidi ya maili 200, kama tunavyojua maili zile zinazokwenda kuombwa kuongezwa sio kama itakuwa umiliki wa moja kwa moja wa ardhi kwa ajili ya eneo la baharini, lakini eneo lile tunalokwenda kuongezewa kwa ajili ya kuweza kumiliki zile rasilimali zitakazopatikana katika eneo lile.

Mhe. Spika, nilishangaa sana serikali hasa kupitia Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais iliposema kwamba hawajui suala hilo wakati tayari kuna magazeti yameshatoa taarifa na mawaziri wananunuliwa magazeti kila siku, lakini kwa bahati mbaya inaonesha magazeti yale yananunuliwa lakini hayasomwi.

Waziri alipoulizwa akasema yeye haya taarifa na Mhe. Spika, ukatoa muongozo hatuwezi kujadili kitu ambacho hatuna uhakika nacho. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri siku ile ile usiku wake tulimuona kwenye televisheni ya *TBC* Waziri wa Ardhi na Makazi wa Tanzania Baraza, Mhe. Anna Tibaijuka na jopo lake akifuatana na wabunge wawili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakenda kuwasilisha ombi lao Umoja wa Mataifa na ombi lile wameliwasilisha kwa msaidizi wa Katibu Mkuu ambaye ni Mama Asha Rose Migiro. Yeye alieleza kwamba suala lile hivi karibuni kutakuwa na kikao cha Umoja wa Mataifa kitakachoweza kujadili.

Sasa Mhe. Spika, sisi tulishangaa kwamba serikali haijui, lakini kitu kilichonishangaza zaidi Mhe. Waziri wa Ardhi, Makazi, Maji na Nishati siku ya pili yake alipotakiwa kutoa ufafanuzi kwa kweli taarifa ya Mhe. Waziri huyo imeniweka njia panda. Kwa sababu inaonesha yeye mwenyewe hajijui dhamana yake wala haijui mamlaka yake, wala hajui nani kiongozi wake.

Mhe. Spika, maneno haya sio ya kwangu maneno haya ni yake mwenyewe katika *paper* hii ambayo nimeichukua *hansard* leo asubuhi maneno aliyoyaeleza juzi. Kwa sababu yeye mwenyewe alieleza suala hili kama serikali haijui, lakini yeye kama waziri anajua.

Mimi nakuuliza Mhe. Spika, hapa Zanzibar tuna serikali ngapi? Kama tuna serikali moja basi Baraza la Mapinduzi ndio serikali, kama tuna serikali mbili basi Baraza la Mapinduzi lina serikali yake na Mhe. Waziri wa Ardhi na Makaazi naye ana serikali yake. Sasa Mhe. Spika, mimi nilikuwa naomba katika maazimio aliyotoa Mhe. Jussa mimi naona maazimio yake haya bado hayajatosheleza.

Mhe. Spika, mimi naomba Baraza lako lituruhusu tuongeze azimio la tano katika Baraza la Mapinduzi. Baraza la Mapinduzi lichukue hatua kali za kinidhamu kwa waziri aliyekiuka mamlaka ya wizara, aliyekiuka mamlaka ya serikali ili iwe fundisho kwa waziri mwengine yeyote asije akafanya jambo kama hili.

Mhe. Spika, kwa nini nikasema jambo kama hilo? Hapa tulipitisha azimio la Baraza la Wawakilishi, azimio lile tuliiagiza serikali na serikali ikakubali na ndio maana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikapeleka barua kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuondoa suala la mafuta na gesi kua la Muungano. Lakini vile vile ushughulikiaji wa suala la *EEZ*

Mhe. Spika tulilipigia kura, ulituuliza katika Baraza lililopita na kwa bahati nzuri Mhe. Waziri kipindi kile alikuwa ni Naibu Waziri Kiongozi, yeye alikuwa ni msaidizi wa shughuli za serikali na aliunga mkono kwamba masuala ya *EEZ* kila serikali ishughulike na masuala yake. Sasa leo seuze, mimi nashangaa! Mhe. Waziri katika maelezo yake ya juzi anasema hata ilo azimio yeye halijui kalisikia kwa Mhe. Ali Mzee, Mhe. Spika, kweli tuko makini?

Mhe. Spika, sasa hivi tunataka serikali iwajibike. Namalizia Mhe. Spika, najua unataka kunambia nimalizie. Naomba tuangalia Katiba ya Zanzibar kifungu cha 9(2)(a) naomba nikinukuu.

Kifungu 9(2)(a) kinasema kwamba:

> "Mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa serikali kufuatana na katiba utatokana kwa wananchi wenyewe", sisi ndio wawakilishi wa hao wananchi wenyewe.

(b) Kifungu cha 43(5) cha Katiba ya Zanzibar naomba kunukuu. "Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za serikali kwa jumla na Mawaziri chini ya uongozi wa Makamo wa Pili wa Rais, watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar."

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atakuwa ndio kiongozi wa shughuli za Serikali lakini serikali itawajibika kwa Baraza la Wawakilishi. Sasa kwa kuwa Baraza la Wawakilishi lilikwisha kupitisha azimio masuala haya kila nchi ishughulikie yake, sasa kama atakuwepo mtu yeyote ikiwa Waziri au mtu mwengine yeyote atakayekiuka mamlaka hii basi Baraza la Wawakilishi litatakiwa liwawajibishe.

Mhe. Spika, mwisho kabisa namuomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atakapoitisha kikao chake cha Baraza la Mapinduzi afanye maamuzi ya busara ambayo tunawashauri kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili tusije tukatumia kifungu cha kanuni cha 41. Mhe. Spika, kifungu cha 41 cha Katiba ya Zanzibar hatupendi tukitumie hapa, lakini serikali ikishindwa kuchukua hatua za kinidhamu tutatumia kifungu cha 41 cha Katiba ya Zanzibar naomba nikinukuu.

Kifungu cha 41:

"Mhe. Spika, bila ya kujali masharti ya katiba hii, Baraza la Wawakilishi linaweza kupitisha azimio la kupiga kura ya kutokuwa na imani na Makamo wa Kwanza wa Rais au Makamo wa Pili wa Rais endapo itatolewa hoja ya pendekezo litakalopitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu hichi."

Mhe. Spika, baada ya kunukuu katiba hii halali ya Zanzibar tuliyoipitisha sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nakuomba nikushukuru lakini mwisho nataka nitoe indhari. Mhe. Spika, hoja hii isije ikachukuliwa kwamba ameitoa Naibu Katibu Mkuu wa chama cha CUF. Mhe. Spika, hoja hii ameitoa Mhe. Ismail Jussa Ladhu Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe, mwakilishi halali. Tunaomba hoja hii isichukuliwe kisiasa, hoja hii ikichukuliwa kisiasa itatugawa na tutaweza kupoteza rasilimali na uwezo wa Baraza la Wawakilishi katika kuisimamia serikali. Mhe. Spika, baada ya hayo machache naomba nikushukuru. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba nikushukuru na wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache katika jambo hili muhimu na nyeti katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kutokana na utafiti na umahiri wake katika kuibua mambo muhimu na mambo nyeti katika taifa letu. Mhe. Jussa tunakushukuru sana kwa sababu kama si utafiti wako basi suala hili lingekuwa ndio limeshayeyuka kinyemela

nyemela. Kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu na kwa kweli nadhani na Wazanzibari wote tunakupongeza katika hili.

Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa katika taarifa kwamba suala hili si suala geni, ni suala ambalo mwaka 2009 tulilijadili sana, ni suala ambalo kwa kweli wananchi wote wa Zanzibar kwa mara ya kwanza katika hali ile tuliyokuwanayo liliwaunganisha Wazanzibari na bila ya kujali tofauti zao tuliungana na kuwa kitu kimoja. Katika mambo yaliyotuunganisha Wazanzibari hii ni agenda ya kwanza.

Mhe. Spika, wakati ule nakumbuka kwamba Baraza lako hili kama ilivyoelezwa katika taarifa, hili ndio Baraza la Wawakilishi na ndio chombo cha wananchi. Kwa taarifa tulizozipata Baraza la Mapinduzi nalo lilitoa msimamo mmoja juu ya suala hili na tangu kipindi kile hadi sasa kama ilivyoelezwa ni kwamba hakuna chombo chochote kilichobadilisha maamuzi yale na kilichokuwa kinatakiwa sasa kwa kweli ni utekelezaji wa kile ambacho tulikiagiza Baraza hili pamoja na Serikali.

Sasa kilichotokea miaka miwili baadae tumeshuhudia kwamba wenzetu walioko Bara katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wameanza tena tatizo lao bila ya kushauriana nasi na bila ya kukumbuka yale ambayo tuliyaagiza, wamekwenda Umoja wa Taifa kama hadithi ambazo tulizipata ili kwenda kuongezewa masafa hayo ambayo ni ya ukanda wa bahari.

Hivyo hivyo, imeelezwa juzi kwamba serikali haina taarifa kwa mujibu wa maelezo ya Waziri wa Nchi. Lakini vile vile na sisi kama Baraza la Wawakilishi chombo ambacho ni cha wananchi kwa niaba ya wananchi hatuna taarifa. Sasa tujiulize kilichotokea ni kitu gani, kilichojitokeza ni taarifa kupitia magazeti na jinsi ambavyo Mhe. Waziri alikiri kwamba yeye kama yeye analifahamu suala hili.

Sasa kwa kweli kile ni kitendo kibaya sana, ikiwa Baraza la Wawakilishi tuliagiza, ikiwa Baraza la Mapinduzi liliagiza, lakini yeye binafsi akachukua hatua. Mimi nasema kwa lugha za watoto wa mijini ile tunasema ni dili iliyochezwa baina ya Waziri na wenzetu wa Jamhuri ya Muungano, au ile ni michongo iliyochezwa baina ya Waziri wetu pamoja na wenzetu walioko Bara ndugu zetu wa damu.

Mhe. Spika, mengi yameshaelezwa na mengi yataelezwa, katika hili kitendo hichi kimeaibisha sana taifa letu, kimeliaibisha Baraza letu na kuwaaibisha wananchi. Sasa kwa kuwa suala hili limegusa hisia za wananchi Mhe. Spika, tangu jana kwa kweli huko mijini unapotembea kunakuwa na matatizo makubwa juu ya suala hili. Kwa kuwa suala hili limegusa hisia za wananchi na

kwa kuwa suala hili limehatarisha maslahi ya nchi yetu, lakini vile vile kwa kuwa suala hili limekiuka maadili ya utendaji kazi wa Baraza la Mapinduzi.

Baraza la Mapinduzi ambacho ndio chombo cha serikali tunachokitegemea, Mhe. Hamza Hassan Juma kasoma hapa Katiba ya Zanzibar kifungu cha 43(5), pale ndio penye mjumuiko baina ya Baraza la Mapinduzi, Mawaziri pamoja na Baraza hili, yale kwa kweli Mhe. Waziri ameyakiuka. Sasa kwa maana hiyo, kwa ustaarabu kabisa kwa kweli namuomba sana Mhe. Waziri kabla ya kufika kwenye Baraza la Mapinduzi awajibike. Mhe. Waziri awe muungwana katika hili achukue hatua za kuwajibika yeye binafsi, achukue dhamana hiyo ya kuwajibika yeye binafsi, huo ndio uungwana.

La atakaposhindwa basi tunamuomba Mhe. Rais achukue hatua za kumfuta kazi Mhe. Waziri, kama Mhe. Rais nae hatochukua hatua hizo kwa kweli Baraza letu nalo lina mamlaka yake. Tunaweza tukaitumia katiba kifungu cha 37(1) ambacho kinasema hivi naomba kunukuu.

Kifungu cha 37(1):

> "Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 36 cha katiba hii, Baraza la Wawakilishi linaweza kupitisha azimio la kumuondoa Rais madarakani endapo itatolewa hoja ya kumshtaki Rais na ikipitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu hichi."

Mhe. Spika, hatutaki tufike huko na wala hatuombi tufike huko. Tunaamini kwamba cheo ni dhamana na lazima kila mtu awajibike kwa matendo yake. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache. Mhe. Spika, nchi yoyote duniani huongozwa kwa misingi ya katiba na sheria. Katika uislamu Mhe. Spika, ukimuona mtu amekiuka msahafu maana yake amekasirika na katika dunia yeyote ambaye anakiuka katiba maana yake amekiuka mipaka ya nchi.

Mhe. Spika, mwaka 2009 Mhe. Mansoor Yussuf Himid alikuja na hoja na waraka wa Baraza la Mapinduzi. Ninavyoamini mimi ni waraka wa Baraza la Mapinduzi si waraka wake hakuandika yeye na watoto wake. Kwa mujibu wa *hansard* hii alitwambia alikaa Baraza la Mapinduzi wakaupitia na hatimae akaridhiwa aulete mbele ya Baraza ya Wawakilishi. Kwa msingi huo, ni waraka wa Baraza la Mapinduzi chini ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati huo Mhe. Dk. Amani Abeid Karume.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba juzi nilipochangia katika mswada nilisema kwamba kuna watu hawaipendi Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Mawaziri walikuwa wakali sana. Leo inakuwaje Mhe. Spika, Waziri ndani ya serikali hii kwa niaba ya Baraza la Mapinduzi chini ya Rais analeta hoja Waziri mwengine anaipinga wazi wazi. Ni aibu kubwa sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa mchango wangu na kwa umakini mkubwa, kwa busara kubwa na heshima kubwa, Mhe. Ali Juma Shamuhuna amevunja Katiba ya Zanzibar na kwa hivyo kwa hiari yake apumzike. Najua Mhe. Spika, ni jambo gumu sana kwa Waafrika kujiuzulu lakini hii ni sheria, hiki si chama cha ngoma, lazima Katiba ya Zanzibar ifuatwe mwenzetu ameshindwa kazi inawezekana kwa uzee, inawezekana kwa makusudi apumzike awaachie wengine wafanye kazi yao.

Mhe. Spika, hili limekuwa ni jambo la tatu kwa ushahidi wangu. Baraza hili chini ya Mhe. Mansoor Yussuf Himid alituletea Sera ya Nishati na akatwambia kwamba hakuna mkataba ambao utapitishwa hapa Zanzibar bila ya idhini ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, sera imeletwa Baraza hili tukairidhia, miezi michache Mhe. Ali Juma Shamuhuna akatia saini na Ras Al Khaima mkataba wa utafiti wa mafuta. Kwa hivyo, nitarudia hapo Mhe. Shamuhuna kukiuka maagizo ya Baraza la Mapinduzi, kukiuka maagizo ya Baraza la Wawakilishi ni aibu.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa sisi Baraza la Wawakilishi tunamheshimu Rais wetu, tunamheshimu Balozi Seif Ali Iddi na kamwe hatuko tayari kumtia aibu. Lakini ukiacha mwana kulia ndugu yangu utalia wewe. Hutaki kumuondosha kwa aibu hii aibu itakufika.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa namuomba sana kaka yangu, mzee wangu mimi ananizaa Balozi Seif Ali Iddi namheshimu sana na ninaamini ni kiongozi makini na ninatarajia baada ya Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein awe refa Zanzibar ajenge heshima yake kumuondosha Mhe. Ali Juma Shamuhuna kwa busara, kwa heshima na kwa unyenyekevu mkubwa.

Mhe. Spika, nasema kwamba katiba imevunjwa, Mhe. Ali Juma Shamuhuna haheshimu Baraza la Mapinduzi, haheshimu Baraza la Wawakilishi, Mawaziri wenziwe hawaheshimu na kwa hivyo aachie madaraka kwa hiari yake ili wale Wazanzibari waishi salama. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku ya leo kufika katika Baraza hili tukufu na afya njema.

Mhe. Spika, mimi kwanza ninajiuliza kweli tuko tahadhari na mambo ya kuongoza nchi. Kama tuko tahadhari kwa nini mazungumzo tunayozungumza kwenye Baraza la Wawakilishi maazimio, matakwa ya Wajumbe wa Baraza, lakini nani hasa anayehusika kuyapeleka huko kwa kujadiliwa tukishakuzungumza hapa Mhe. Spika. Ni imani yangu kwamba lazima kuna mtu anaorodhesha na kama ni Waziri wa Wizara husika anaangalia *hansard* ya kila kipindi cha Baraza la Wawakilishi kuhakikisha yale maamuzi au maagizo yanayotolewa kwenye Baraza la Wawakilishi kuyachukulia hatua.

Mhe. Spika, wenzangu wametaja vifungu mbali mbali kuhusu suala hili sitaki nirejee. Naiomba sana Serikali kuu chini ya utawala wa Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein tumedhamiria Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunaowawakilisha wananchi kuiweka sawa serikali yetu ili kuwapa matumaini wananchi wetu hatutokuwa legelege.

Mhe. Spika, mimi namsikitikia sana ndugu yangu Mhe. Ali Juma Shamuhuna kwa sababu ni mtu mwenye uzoefu wa hali ya juu. Sasa nashangaa juzi tulipouliza suala hili *hansard* hii hata ukampa mtoto kwa kweli amejikanyaga mwenyewe humu. Mara anajua, mara kasoma kwenye magazeti, mara hajui. Mhe. Spika, hivyo kweli tutafika nchi hii, mtu mwenye dhamana ambayo Rais amemteua kwa kuona kwamba atamsaidia. Naungana mkono na wenzangu yote yale waliyoyazungumza.

Mhe. Spika, namuomba sana ndugu yangu Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tuna tegemeo kubwa sana kwako wewe, tunakuomba sana yanayozungumzwa humu Waziri wako achukue kama Mawaziri wengine hawawezi kuchukua mambo yao wakenda wakayafanyia kazi kwa sababu wewe ndio kiunganishi. Mimi niliuliza swali hilo nani hasa anayechukua matokeo yake ndio haya Mhe. Spika. Kwa vile nimeshasema haya tena nasema kwa nia safi kwa kusaidia wananchi ambao wana matumaini na Waheshimiwa Wawakilishi wao wanaowawakilisha.

Mhe. Spika, narudia tena ili niwape wenzangu nafasi. Hatutokuwa tayari serikali hii ya Umoja wa Kitaifa kila mmoja akalinda upande wake. Naunga mkono maneno yaliyosemwa si Naibu wa CUF ni mjumbe ambaye amechaguliwa na wananchi. Sisi hatutokuwa tayari kumlinda mtu kwa sababu ni CCM kwa maslahi yake mwenyewe. Mimi nasema kweli sitokuwa tayari kumlinda mtu kwa sababu ni CCM kwa maslahi yake si kwa maslahi ya umma. Tunataka kuliweka Baraza na Serikali yetu iende vizuri ili wananchi wawe na matumaini na serikali hii. Mhe. Spika, nakushukuru, ahsante sana.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii. Mhe. Spika, nilipotoa hoja kwa kuwa yale maazimio wapewe Wajumbe wa Baraza ili

wayapitie wayajue kwa sababu wengi hapa ni wepya. Hata Baraza la Mawaziri kuanzia Makamo wa Kwanza wa Rais hajakuwepo azimio hili lilipopitishwa na baadhi ya Mawaziri na leo wameona faida yake.

Lakini Mhe. Spika, niruhusu ninukuu wakati Baraza la Wawakishi Katiba inapitishwa na Rais Ali Hassan Mwinyi. Anasema "Mhe. Spika, kwa Katiba yetu mpya Baraza la Wawakilishi limeimarika, Baraza sasa limekuwa kweli ni ngome ya wananchi. Sauti ya wananchi katika Baraza ni kubwa kuliko sauti ya Serikali na ukiacha Wakuu wa Mikoa watano na Wajumbe kumi walioteuliwa na Rais, Wajumbe wote waliosalia ama wanachaguliwa moja kwa moja na wananchi au wanachaguliwa na Wawakilishi wenyewe."

Kwa hivyo, Baraza la Wawakilishi ni sauti ya wananchi, ni ngome ya wananchi, wala hakuna zaidi ya Baraza la Wawakilishi. Sasa hoja hii Mhe. Spika, siku ya Alkhamis usiku tarehe 2 ulinambia Mhe. Ali Mzee Ali nenda ukaongoze Baraza kuna ile hoja kidogo hali yangu si nzuri. Magazeti yakaandikwa, *hansard* Hamad Masoud Hamad hivi, lakini mimi ndio niliyeongoza kikao cha mwanzo. Hoja iliyokuja mezani *hansard* ya tarehe 3 hati ya kuwasilisha mezani Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi naomba kunukuu.

"Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani inayohusu Taarifa ya Mapendekezo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu Ripoti ya Mshauri Mwelekezi juu ya Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia."

Mhe. Spika, hoja si ya Wizara, hoja ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo ilikuwa awamu ya sita na sasa hivi ya saba. Kama kuna mabadiliko tutaambiwa kwamba hoja ile imefutwa, lakini ilikuwa hoja ya Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, Mhe. Salmin Awadh Salmin anasema "Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana sana na mapendekezo ya Serikali. Mapendekezo ya
Serikali si Mhe. Mansoor Yussuf Himid yote matatu yaliyowasilishwa. Mapendekezo haya si ya Mhe. Waziri isipokuwa ni mapendekezo ya Serikali na maamuzi yake yatolewe hapa katika Baraza la Wawakilishi. Maamuzi yatakapotolewa hapa ni ya wananchi wenyewe yaani Wazanzibari sio ya mtu."

Mhe. Spika, maneno haya amesema Mhe. Salmin Awadh Salmin. Sasa imekuja hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu kasoma kwenye magazeti kasikia kaleta hoja yake.

Mhe. Spika, hii si mara ya kwanza, mwaka 1984 Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban alikuwa Mjumbe wa Baraza hili Jimbo la Bumbwini alileta hoja kutokana na gazeti nililosema Mhe. Edward Moringe Sokoine alifanya semina

Bagamoyo akasema *supremacy* ya chama ikaja hoja ndani ya Baraza hili. Katika Wajumbe wa siku ile waliokuwepo humu ndani ni Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban wengine wote walikuwa hawapo hapa na yeye alichangia sana juu ya *party supremacy*. Kwa kusema kweli hoja ile Baraza likaahirishwa mpaka kikao kilichofuata matokeo yake tarehe 31 Januari, 1984 Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi na Mhe. Waziri Kiongozi wote walijiuzulu. Huu ni ushahidi.

Sasa Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi linapotoa maazimio yake lazima yaheshimiwe. Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi tulitoa maazimio kwenye katiba hii. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kila azimio la Baraza inalitekeleza, wenzetu hawatekelezi. Mhe. Spika, azimio la Baraza lilisema hivi kuanzisha katiba. "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Baraza la Wawakilishi linaanzisha Katiba ya Zanzibar."

Hii hapa Katiba ya Zanzibar kuna azimio la Baraza limetekelezwa. Katika Wajumbe waliokuwepo siku ile kupitisha azimio hili humu ndani mote aliyekuwepo siku ile mwezi Oktoba, 1984 ni Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, lakini azimio lilipitisha mwaka 1985 waliokuwemo humu ndani ni Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban alikuwa Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi na Mhe. Asha Bakari Makame alikuwa Naibu Waziri ndio waliopitisha azimio historia haitowasahau. Ukipenda ndio hivyo, hupendi ni ukweli.

Lakini Baraza hili hili Mhe. Spika, tulipitisha azimio katika Katiba hii ya Zanzibar linasema hivi. "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa na uwezo wa kuweka kitu chochote kitakachokuwa kielelezo cha serikali kama itakavyoamuliwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi."

Mhe. Spika, tumekaa miaka 20 kipengele hichi tulishindwa kukitekeleza lakini awamu ya sita ilipoingia tukaweka Azimio la Baraza. Azimio gani Mhe. Spika, Kauli ya Serikali kuhusu kuanzisha bendera ya Zanzibar. Baraza la Wawakilishi lilipitisha bendera baada ya miaka 20 tukatukanwa tukaambiwa bendera ya Simba na Yanga, bendera ya dhikiri, lakini tukaipepea bendera pale na sasa leo bendera hiyo hapo.

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi tulitoa azimio kuahirisha uchaguzi uwe mapema Jimbo la Mkanyageni. Mhe. Spika, unakumbuka azimio lilikuja uchaguzi wa Jimbo la Mkanyageni tukatoa Azimio la Baraza tukatekeleza. Mhe. Spika, natoa mifano hii kujenga hoja kama Baraza hili lina nguvu.

Mhe. Spika, Mhe. Abubakar Khamis Bakary alileta hoja yake Baraza la Wawakilishi likaijadili tukaondosha mengine tukaweka mengine lakini hatimae Baraza la Wawakilishi likapitisha hoja ya Baraza ambayo ni maarufu. Hoja

hiyo ya Baraza ndio iliyozaa Katiba hii ya Zanzibar. Mabadiliko haya yametoka kutokana na hoja ile. Kwa hivyo, Baraza la Wawakilishi ni chombo chenye mamlaka ya juu ndani ya nchi hii na Wajumbe wake ndio wenye maamuzi ya mwisho kabisa.

Mhe. Spika, naeleza mambo muhimu, Baraza la Wawakilishi liliweza kupitisha jambo kubwa sana. Baada ya Mapinduzi kilitangazwa chama kimoja mwaka 1991. Lakini Mhe. Spika, wewe ulikuwa ni mwakilishi 1992 Baraza la Wawakilishi kwa shingo upande na kwa tabu. Lakini kwa sababu ni maslahi ya wananchi tukapitisha mswada wa sheria marekebisho ya 5 ya katiba ya Zanzibar 1984, tuliyapitisha. Spika alikuwa bwana Ali Khamis na wewe ulikuwa mjumbe na ulichangia.

Mhe. Spika, jambo lile lilipitishwa na wajumbe 70 walisema kwa pamoja tuanzishe mfumo wa vyama vingi, kwa bahati mbaya wajumbe 5, hakuna mjumbe aliyekataa, wajumbe 5 walikuwa hawako. Mhe. Ali Ameir, Mhe. Adam Mwakanjuki, *Major General* Bakar Wakati, Mhe. Pandu Ameir Kificho na Ali Mzee Ali. Sio mimi, Kificho mimi Ali Mzee Ali yule pale, hawa ndio walikuwa hawapo. Kwa hivyo, tukaanzisha mfumo wa vyama vingi kwa azimio la Baraza.

Sasa yale maazimio tuliyoyatoa Barazani ambayo sisi tumeunga maazimio ya Serikali ya Mapinduzi, tumeletewa na Baraza la Mapinduzi, tukaunga mkono na suala hili la *zone*, tulilisema liwe letu. Sasa hoja inasema Baraza la Mapinduzi litowe maelezo, sawa. Lakini Baraza la Mapinduzi na mimi naomba lisimamie matakwa ya Wazanzibari. Sasa hivi tuna Serikali ya Mapinduzi yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa inayosimamia haki na usawa, ndio katiba inavyosema. Katiba hii ina mambo ya kusimamia kwenye hiyo Serikali ya Umoja wa Kitaifa yenye mfumo, mfumo gani. Kuna mfumo Mhe. Spika, lazima tuukubali kuwa ni mfumo muhimu katika nchi yetu wa kujenga umoja wetu na kujenga nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa sababu nimejaribu kueleza haya yalivyo, naomba tuelewane. Hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa imechaguliwa na nani, tumetengeneza *referendum*, tumekwenda kwa wananchi, tumewauliza na wananchi walikuwa na haki ya kutoa maoni yao, wako waliosema wanaitaka na wako waliosema hawaitaki na wote tuliwashukuru wametumia haki yao ya demokrasi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa watu wengi wanaizungumza. Serikali ya Umoja wa Kitaifa imefungwa katika kifungu cha 1980 ina utaratibu wake. Zamani Mhe. Spika, tulikuwa tunakaa upande huu wa kulia na upande ule wa kushoto. Mfumo huu tulipokwenda Ulaya, Ujerumani na Uingereza Mhe. Haji Omar Kheir yule pale, Mhe. Ali Abdalla Ali yule pale,

Mhe. Abubakar Khamis Bakary na Mhe. Ali Mzee Ali, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, Katibu Kiongozi, Katibu Mkuu Fedha, na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwenda kujifunza serikali za wenzetu. Tulipokwenda Uingereza serikali sio ya Umoja wa Kitaifa ni ya mseto na Ujerumani serikali ya mseto, hawana serikali ya umoja wa kitaifa. Lakini tulikaa na ripoti tukaiandika na tukaikabidhi serikali. Hiyo tume Mhe Spika, uliichagua wewe kamati ya watu sita.

Mhe Spika: Ahsante mheshimiwa muda.

Mhe. Ali Mzee Ali: Namalizia Mhe. Spika. Kwa hivyo, ipo haja tuelewane, huu mfumo wa *backbenchers* na *front* sio ule uliopita hapana, huu ni mfumo wa pamoja Mhe. Hamza Hassan Juma anasema *hot dog*, sisi tuko nyuma na wao wako mbele, hakuna mbabe, hakuna mtu ana haki peke yake sote ni wamoja. Mimi nimeingia humu ndani nimechaguliwa na Rais na Balozi Seif Iddi. Sisi tuko watu tisa Rais katuchagua, wanane ni mawaziri na mimi mmoja niko huku *backbenchers.* Lakini sote ni wamoja.

Mhe. Spika, nakupa pongezi za dhati kwa busara ulizopitisha kwa maamuzi tuliyopitisha leo juu ya mswada wa mafao. Hiyo ndio *sprit* ya umoja, mheshimiwa nakushukuru sana. Mhe. Hamza Hassan Juma kama Mwenyekiti na wewe nakushukuru sana kwa kazi nzuri uliyoifanya na tutaendelea kufanya kazi nzuri zaidi Mhe. Abubakar Khamis Bakary tuendelee kuijenga nchi yetu.

Mhe. Mjumbe mmoja kasema hii hoja sio ya CUF, hamna CUF. Hii hoja ni ya *backbenchers* mwakilishi na sisi tunaunga mkono. Hii serikali ichukuwe hoja hizi isijibu, tusilete malumbano, tusitukanane wala tusibeze. Mhe. Rais kasema juzi, wale wenye tabia ya kuwabeza wenzao wanapotoa maoni yao waache. Kwa hivyo, tuache tabia ya kubeza michango ya wenzetu, tuheshimu michango, tuheshimiane na tuijenge nchi yetu kwa manufaa ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, kwa hayo mafupi nakushukuru sana. *(Makofi).*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa na mimi nafasi nichangie kidogo, kwa sababu unasema muda. Mimi nakubali, muda unakwenda na mimi wala sitokwenda mbali sana nitachangia kidogo sana, kwa sababu wenzangu waliotangulia kuchangia wamezungumza mengi sana, wamenukuu vipengele na mambo mengine. Kwa hivyo, na mimi natia nyama kidogo hapo hapo palipobakia ili nimpe muda mwenzangu naye ili aweze kuchangia.

Kwanza Mhe. Spika, mimi nianze kwa kumshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa kutuletea hoja hii. Lakini niwashukuru wenzangu waliotangulia kwa michango yao mizuri kabisa ambayo imenifanya na mimi nikose kabisa la

kusema, maana yake yale niliyoyapanga mengi wameshayazungumza, sasa nikiendelea kuzungumza nitakuwa narejearejea, lakini mimi nikazie pahala pamoja tu kidogo kwenye uwajibikaji, maana mambo haya bwana ndivyo yanavyokwenda hivi.

Mhe. Spika, tukiiangalia hoja hii aliyoiwasilisha Mhe. Ismail Jussa Ladhu hapa ina maelezo mengi sana, lakini cha kusikitisha kabisa ni ule uwamuzi wa Mhe. Waziri wa kudharau kabisa mapendekezo au maazimio ya Baraza. Kwa kweli hichi mimi kinanisikitisha sana na mimi niungane na wenzangu wote ambao walimtaka Mhe. Waziri akae pembeni ili kuweka nidhamu ya chombo hiki. Mimi sina hoja zaidi ya hili Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Namuomba Mhe. Waziri awajibike, ahsante sana. *(Makofi)*.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa fursa ndogo ya kutoa mchango wangu mdogo katika suala hili. Kwanza tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzinduzi huu aliotuletea Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ni taufiki ya Mwenyezi Mungu uzinduzi huu ukatukuta kwa sababu ya nia zetu nzuri za kukaa na wenzetu katika Muungano huu.

Mhe. Spika, pamoja na kuyaunga mkono yale yaliyozungumzwa katika waraka huu na yale waliozungumza wenzangu kuhusu mengi ya umuhimu wa maazimio ya Baraza, lakini napenda nisisitize mambo mawili.

Mhe. Spika, mara tatu nimeshawahi kuuliza katika Baraza hili ni nani mwenye kuhusika moja kwa moja Zanzibar kuwasilisha matakwa yetu kikatiba katika Jamhuri ya Muungano. Majibu huwa yanakuja hivi hivi ya kubabaisha. Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, kwa sababu wenzetu hawana nia safi katika Jamhuri ya Muungano na mambo wanatuendea kinyemela, Baraza hili lipitishe azimio la kuwa mara moja Bunge la Jamuhuri ya Muungano lirudishe kiti cha Rais wa Zanzibar kuwa ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Muungano. Kwa sababu yote haya ni kwamba Rais wetu anakwenda kupembejea kule, lipeni ngoja kidogo. Lakini kama angekwenda kama vile alivyokwenda Rais Karume wa mwanzo alipokuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, mimi naamini mafuta yetu tungeshachimba, wala ingekuwa hakuna zone ya kuongezwa wala nini.

Mhe. Spika, mambo haya ni kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar hana mamlaka ya kikatiba katika Jamhuri ya Muungano tokea alipotolewa kama ni Makamu wa Rais wa Tanzania. Kwa hivyo, Baraza lipitishe azimio la kuwa Bunge lirudishe na Wazanzibari wote waungane kwamba Rais wa Zanzibar kabla hiyo katiba mpya itakapotajwa baadae haidhuru. Lakini kwanza katika kipindi hiki cha mpito, Rais wa Zanzibar arudi kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, sio achukuliwe Mzanzibari tu waseme huyu ndiye Mzanzibari, lakini hawakilishi chochote Zanzibar. Hilo la kwanza.

La pili Mhe Spika, ni kwamba mawaziri wanawajibika kwa Baraza la Wawakilishi kwa pamoja. Kwa hivyo, ikiwa mheshimiwa huyu huyu alituahidi kwamba kipindi sio kirefu tutaona hatua gani alizochukua katika suala hili la mafuta na yuko mbioni na safari hizi. Lakini sasa hivi baada ya kutangazwa ile kuja kwa meli kutoka Korea, meli yenye uzito sijui gani, ukubwa gani siju na yenye gharama kiasi gani, ndio matokeo yanakuja haya. Ramani hii tuliyopewa Mhe. Spika, walituambia wale Wa-Norway na Wa-Finland walipotupa semina siku ile, kwamba mafuta Pemba Tundauwa hayana mjadala yapo, hili halitaki utafiti wala halitaki chochote, mafuta Pemba Tundauwa yapo na hivi sasa athari zipo wataalamu wanaokwenda wanaziona.

Sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hii kungoja ngoja utamkuta ……. Naomba wajaze wenyewe. Hii kungoja ngoja hii ndio inayotuuwa. Kwa hivyo, pamoja na haya basi yatakuja mengine makubwa zaidi kuliko haya. Likishapatikana hili eneo basi tutaingiliwa na mameli hapa yatakuja kuchimba mafuta kwa sababu siku hizi mirija inaunganishika huko huko nje kwa nje. Ikiwa meli zinakuja hapa zikapakia mafuta meli kwa meli halafu ndio yasiwezekane kuchimbwa huko chini kwa chini. Umeme tunaoutumia unatoka wapi huu, unatoka Tanganyika, kwa nini tukautumia sisi, utaalamu. Kwa hivyo, utaalamu huo upo sisi tungoje tu.

Lakini la mwisho kabisa Mhe. Spika, kuna jambo ambalo linataka kutokea, sisi hatulijui Zanzibar inafutwa na hili lilianza baada ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanganyika. Nyinyi mlisikia wapi katika historia ya ulimwengu kwamba kuna nchi 1961 iitwayo Tanzania Bara ikapata uhuru. Mimi sijawahi kusoma kitabu chochote kwamba kuna nchi iitwayo Tanzania Bara imepata uhuru mwaka 1961. Kwa hvyo, ilipofika mwaka 2011 ikawa inasherehekea miaka 50. Ilikuwa ikiitwa Tanganyika, lakini hawataki wao wenyewe kusema kuwa ilikuwa inaitwa Tanganyika. Katika uhuru mabango yote yaliandikwa Tanzania Bara, ili ionekane kuwa wangetaja wao Tanganyika basi Zanzibar ingejitokeza, kwa nini wanasherehekea uhuru wa Tanganyika hawa, lakini ile ni *stomataisacion* MMMMMya brain kuwafanya wale watoto wao wasijuwe kwamba kuna Zanzibar huku, wafahamu kwamba kuna Tanzania tu. Kwa hivyo, na sisi tuzinduke tusikurupuke tu ni lazima tuchukuwe hatua za haraka. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri hapo awajibike, ahsante sana. *(Makofi)*.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa hii kuchangia kidogo katika hoja ambayo ameileta Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Nimeshawishika kuchangia kwa sababu yaliyosemwa katika kuchangia hoja hii Waheshimiwa Wajumbe wanaweza wakayafahamu vizuri sana, lakini sina hakika wale walioko nje ya Baraza hili wanaweza wakayafahamu vizuri kama ambavyo tunapenda tuyafahamu. Mhe.

Spika, ndio maana nikasimama nikasema labda kuna jambo dogo, nijaribu na mimi kutoa mchango ili litusaidie kufahamu vizuri zaidi madhumuni ya hoja hii.

Pili na mimi niungane na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kumshukuru Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Nimshukuru kwa sababu alichofanya ni kututanabahisha kwamba jamani kuna jambo la namna hii linaendelea na serikali ni vyema kama vile ambavyo ilikwishaahidi italifanyia kazi basi ni vyema mambo haya ikaweza kuyaangalia. Nikiri kwamba sio kila mtu ndani ya serikali au wajumbe wengine au hata nje ya serikali, ambaye anaweza pengine akatanabahi kuhusu suala hili na akaona pengine linawezekana likawa lina madhara huko mbele kwa nchi yetu.

Sasa Mhe. Ismail Jussa Ladhu kutokana na umahiri wake wa utafiti hili ameliona na baada ya kuliona akaona ni vyema aitanabahishe serikali kwa sababu ndio inayosimamia maslahi ya nchi yetu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hata haki zake nyengine nje ya Tanzania.

Kwa hivyo, mimi nilipoisoma hii hoja ya Mhe Jussa, Mhe. Spika, kwa kweli nilichoona ni kwamba ameeleza kitu *very straight forward*, kwamba Baraza la Mapinduzi litakapojadili suala hili ni vyema na mambo haya ikayazingatia. Mhe. Spika, kwa maana hiyo Mhe. Jussa mwenyewe hoja yake alivyoileta ni kwamba bado amekubali kwamba serikali ilizingatie jambo hili, amekubaliana na ile ahadi ya serikali kwamba jambo hili ilizingatie, lakini katika kuyazingatia na yeye ametoa, sikuizi tunaita maangalizo. Sasa kama aliyotoa ni maangalizo kwa ajili ya kuipa fursa serikali ilijadili na ilete taarifa yake hapa mbele ya Baraza hili tukufu. Mimi nadhani tungeyachukulia kama ni maangalizo na serikali iende ikayafanyie kazi.

Mhe. Spika, mengine tuliyoyasema mimi yananipa wasi wasi. Kwa sababu hoja za hapa Mhe. Spika, ni mbili. Katika suala la *EEZ* kuna mambo mawili kwa ujumla. Jambo la kwanza ni suala la kuomba utambuliwe kama wewe ndio mwenye haki ya kulitumia hilo eneo, kama ambavyo lilitolewa kwa mara ya mwanzo katika miaka ya 1980 zikatolewa kilomita 200.

Lakini mkataba huo huo ukaruhusu kwamba basi kama kuna nchi ambayo inahisi mbele ya hii *continental shape* kuna eneo la ziada ambalo inaweza ikapinga kulitumia basi ilete ushahidi kwamba inauwezo wa kulitumia, lakini na kwamba eneo hilo haitogombana na nchi nyengine. Sasa kupinga huku kwanza kuna muda maalum katika kupeleka, lakini mbali ya kwamba ina muda maalum, ina mambo ambayo ni lazima uweze kuyathibitisha kwamba yapo na yametimiza hivyo vigezo ndio unaweza ukapewa hili eneo.

Mhe. Spika, ndio maana tunajiuliza kwa nini serikali yetu idai kilomita 61. Ziko nchi ambazo zimedai zaidi ya kilomita 61, lakini ni kwa kufuata vile vigezo ambavyo vimewekwa. Kwa hivyo, suala la kupinga ni suala moja, lakini suala la pili ni kwamba Baraza lilipitisha azimio hapa kwamba suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta, iwe ni *on show*. Maana serikali ilileta azimio hapa au pendekezo kwamba katika *on show* tu ndio lisiwe jambo la Muungano. Lakini Baraza ilichosema ni kwamba hapana, iwe katika *on show* ama katika *off show* kwa maana eneo la *EEZ*.

Sasa suala linakuja kwamba je, kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kudai hilo eneo la ziada la *EEZ*, je kunapingana na hili suala la hili azimio la Baraza. Sasa hayo majibu mimi sidhani kama tunaweza tukayapata kwenye kikao hiki kwa sababu kuna masuala mengi ya kisheria ya kuweza kujiuliza na kuyatafakari. Baraza la Mapinduzi litakapokaa na kutafakari suala hili ndio litakapokuja na maelezo ya kilichotokea na kama kweli kinachofanywa na Serikali ya Muungano kinapingana na azimio la Baraza au hakipingani na azimio la Baraza. Kama kinapingana na azimio la Baraza basi serikali itachukua hatua gani. Hayo ni maelezo ambayo yatakuja wakati serikali itakapoleta maelezo yake na baada ya kutafakari, kwa sababu sidhani kama kuna mtu yeyote humu ndani, ukimuuliza hili atakupa jibu la moja kwa moja kwamba hiki kilichotokea ni kosa au si kosa.

Kwa hivyo, nadhani haujafika wakati wa kusema nani mkosa, wa kusema nani kakosea na wa kusema nani mchawi. Hayo yatakuja itakapokuja taarifa ya serikali ambayo Mhe. Ismail Jussa namshukuru sana kwamba ameiongezea taarifa zaidi ya kuweza kuijadili. Lakini hili suala lina mambo mengi ya kisheria ambayo yanahitaji yafanyiwe kazi, naamini kwenye hilo Mhe. Jussa atakubaliana na mimi kwamba hakuna jibu la moja kwa moja kwa sasa hivi, mpaka tutakapolifanyia kazi na kulifanyia utafiti na hiyo taarifa itakapokuja ndio itakapokuja kutoa jibu. Hapo kama ni mashtaka yatakuwa wakati huo, kama ni hukumu itakuwa ni wakati huo. Lakini nadhani kwa sasa hivi kumshtaki mtu tukamuhukumu hapa hapa nadhani sio sahihi.

Mimi nilikuwa napendekeza sana Mhe. Jussa labda a-*stick* labda na haya mapendekezo aliyoyatoa, serikali iende ikayafanyie kazi haya na baadae tutakapokuja tutakuja kuyajadili. Sasa anayesema Mwanasheria Mkuu ndio mkosa. Maana inawezekana kuna wengine ndio wakosa lakini humu hamjawajua, basi wakati huo ndio tutakuja kusema nani ni mkosa na hatua gani zichukuliwe, kama kuna mkosa kwa kweli na kama hii hatua kweli itakuwa imepingana na mapendekezo au maazimio ya Baraza. Lakini sasa hivi Mhe. Spika, kwa kweli hiki ni chombo kikubwa. Huko nje watu wanaweza wakafikiria kwamba Rais keshaagizwa amuondowe Mhe. Shamuhuna na asipomuondoa Mhe. Shamuhuna basi ataondolewa yeye, maana ndio

tuliyoyasema humu ndani. Sasa hayo ni mambo ambayo ni lazima tuwe na maelezo sahihi na tuyaseme wakati muafaka. Inawezekana ni maneno mazuri lakini yatakaposemwa wakati muafaka.

Mhe. Spika, ndio hilo ambalo nilisema ni vizuri tuliweke sawa jambo hili ili watu wasipate tafsiri ambayo sio sahihi katika suala hili. Nakushukuru sana Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu. Sasa ilivyo ni zamu yake Mhe. Ismail Jussa Ladhu, lakini nataka nitowe maelekezo mawili makubwa, kwamba hoja iliyopo ni suala la maombi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo ambalo serikali kwa maana ya Baraza la Mapinduzi ilikuwa haijataarifiwa rasmi. Hiyo ndi hoja iliopo mbele yetu. Hakuna hoja hivi sasa ya kutoa humu kwa mtu yeyote, hivyo ndivyo ilivyo.

Kwa hivyo, namruhusu mtoa hoja hii afanye majumuisho na kama vile ilivyokuwa *spirit* ya tangu awali kwamba mawazo ya wajumbe juu ya jambo hili la ukanda wa *EEZ* ichukuliwe na serikali ili kuzingatiwa kwa pamoja. Kwa hivyo, nilitaka nitowe maelekezo hayo kwamba haitakuwa sahihi kutoa hukumu yoyote hapa, hakuna hoja ya hukumu iliyokuja kwa mtu yeyote dhidi ya mtu yeyote, tunakwenda juu ya hoja ya *EEZ*. Mhe. Jussa Ladhu karibu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kufanya majumuisho mafupi juu ya hoja ya kujadili hili jambo la dharura ambalo niliwasilisha muda mfupi uliopita.

Mhe. Spika, kwanza nirejee kukushukuru tena kwa kuruhusu kufanyika kwa mjadala huu. Mara nyingi tumekuwa tukisema kwamba kadiri siku zinavyokwenda ndivyo tunavyoona umahiri wako, umakini wako, hekima na busara zako. Lakini zaidi Mhe. Spika, kukipa heshima chombo hiki ambacho kinastahiki ya kuruhusu mijadala ya wazi, ya kidemokrasia kabisa ambayo inakifanya chombo hiki kifanye wajibu wake uliotajwa ndani ya katiba yetu.

Baada ya kukushukuru Mhe. Spika, kwa kuruhusu hoja hii. Naomba pia niruhusu niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wanane wa Baraza lako ambao wamechangia hoja yangu binafsi, naomba niwatambuwe. Wa kwanza kabisa ni;

1. Mhe. Hamza Hassan Juma.
2. Mhe. Omar Ali Shehe.
3. Mhe. Hija Hassan Hija.
4. Mhe. Asha Bakari Makame.
5. Mhe. Ali Mzee Ali, *Professor* katika Baraza hili la Wawakilishi ambaye ameuthibitisha U-*professor* wake tena leo.

6. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa.
7. Mhe. Rashid Seif Suleiman na mwisho lakini si akali
8. Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba nia yangu ilikuwa ni njema ya kuisaidia nchi yangu au yetu. Kwa kweli sikukusudia kuleta hoja hii, ili kumsulubu mtu. Kwa hivyo, ndio maana hoja yangu ilijikita zaidi katika yale ambayo niliona kama nilivyoomba juzi kwamba yataisaidia serikali kupitia Baraza la Mapinduzi litakapokaa kwa ajili ya kuyatafakari, ili hatua hii iliyochukuliwa isije kutuletea athari sisi kama nchi ya Zanzibar pamoja na watu wake tunawawakilishi hapa.

Mhe. Spika, sasa niende moja kwa moja katika baadhi ya hoja ambazo zimetolewa hapa. Mhe. Hamza Hassan Juma alijikita zaidi juu ya suala la uwajibikaji, ambalo nataka nilisema kwa pamoja limejitokeza kwa Waheshimiwa Wajumbe wengi.

Mhe. Spika, nakubaliana na wewe pale uliposema kwamba hapa hatutoi hukumu. Kwa kweli chombo hiki sidhani kama kina mamlaka ya kupitisha hukumu. Lakini sifikiri kuwa kama alivyoeleza Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba Waheshimiwa Wajumbe walipokuwa wakitoa maoni haya, walikuwa wanatafuta mkosa kwa maana ya suala zima lile la hatua ya kufikisha mapendekezo rasmi katika Umoja wa Kimataifa.

Kwa hivyo, kilichojitokeza zaidi kugusa hisia za Waheshimiwa Wajumbe ni maoni au mchango ama maelezo aliyoyatoa mwenyewe Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaa, Maji na Nishati, ambapo alipolihotubia Baraza juu ya suala hili alisema kwamba, suala hili ikiwa serikali ni waziri basi yeye waziri analijua, lakini ikiwa Serikali ni Baraza la Mapinduzi haijui na bila ya shaka hakuliambia. *(Makofi)).*

Sasa Waheshimiwa Wajumbe *concern* yao ipo hapa, kwamba tukiwa na waziri ambaye haiheshimu *doctrine* ya *collective responsibility*, yaani uwajibikaji kwa pamoja kama alivyokiri mwenyewe kwa mujibu wa maelezo yake kwamba hakuwaambia wenzake, yaani Baraza la Mapinduzi. Katika Matakwa ya Ibara ya 43 kifungu kidogo cha 5 cha Katiba ya Zanzibar, basi hapo bila ya shaka Waheshimiwa Wajumbe walikuwa na haki ya kutoa hisia zao kama ambavyo walivyozieleza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka kuachia kiti chako kwa ajili ya kuliamua hilo, ambalo limetolewa na Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu mimi sina mamlaka nalo. Lakini kama mtoa hoja ikiwa kiti chako hakina pingamizi nalo na mimi sina

pingamizi ya kujumuishwa katika jumla ya mapendekezo ambayo nimeyatoa hapa, ambayo pia nilipata nafasi ya kukufikishia. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe, kidogo hili nataka niliweke sawa, kwa sababu nadhani si sahihi kidogo na Mhe. Mwanasheria Mkuu ameligusa, alisema kwamba tusipochukua hatua hapa, basi tunaweza kutumia ibara ya 37 ambayo inazungumzia Kumshtaki Rais.

Nadhani hili niliweke sawa Mhe. Spika, nafikiri mwenzangu kidogo alichukuliwa zaidi na ile kuumwa na nchi na kufika mbali. Mhe. Spika, ibara hii inazungumzia Kumshtaki Rais ikiwa amevunja Katiba si katika masuala kama haya. Lakini zile hoja zake nyengine naziafiki katika kutoa hisia zake. Kama nilivyosema Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Asha Bakari Makame wote wamekazia hapo.

Lakini zaidi naomba niende katika mchango ya Mhe. Ali Mzee Ali. Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Mjumbe yeye ni mtu mzima wetu humu ndani na tunamwita *Professor* si kwa maana ya kumvika kilemba cha ukoka, lakini ni kutokana na uzoefu pamoja na umahiri wake, amezungumza mambo ya msingi kabisa Mhe. Spika.

Kwanza amependekeza na hili naomba kwa hekima zao ulikubali tuliongeze katika mapendekezo ya hoja. Kwa hivyo, amependekeza kwamba tuongeze azimio au katika hizi hoja tulizoziomba, hoja ya kutaka Baraza la Mapinduzi pia lisimamie yale Maazimio Matatu ambayo yaliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 8 Aprili, 2009.

Mhe. Spika, hapa moja kwa moja nikuombe kwa ruhusa yako pamoja na Waheshimiwa Wajumbe waridhie, kwamba katika maazimio yale tuongeze Azimio la Kulitaka Baraza la Mapinduzi Lisimamie Utekelezaji wa Matakwa ya Wazanzibari ambayo Yalipitishwa na Chombo chao cha Baraza la Wawakilishi tarehe 8 Aprili, 2009 kuhusu suala la Mafuta, Gesi Asilia pamoja na Ukanda wa Bahari Kuu (*Excusive Economic Zone*) kuwa chini ya Usimamizi na Umiliki wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Mjumbe amesisitiza juu ya nguvu za chombo hiki akinukuu hotuba wakati lilipokuwa likizinduliwa Baraza hili, kwamba “hii ni Ngome ya Wananchi” pia alisema katika hotuba hiyo pale iliposemwa kwamba “sauti ya wananchi kwa chombo hiki ina nguvu kuliko sauti ya serikali”. Suala hilo ni la msingi kabisa.

Mhe. Spika, nampongeza kwa hayo na kama nilivyosema lile pendekezo lake ningefurahi kama tungelijumuisha.

Wengine Mhe. Spika, wamejikita katika uwajibikaji kama vile Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mhe. Rashid Seif Suleiman, lakini mbali ya kusisitiza suala la uwajibikaji pia amelizungumzia suala la kuongeza Azimio la Kutaka Nafasi ya Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano lirejeshwe. Mhe. Spika, kwa maoni yangu mimi suala la muungano na matatizo, kwa sababu mimi siziiti kero, limekuwa kubwa mno kiasi ambacho kwa sasa tukisema tupitishe azimio la kuzungumzia hiki kimoja tutakuja kupata tabu. Kwa hivyo, nadhani hivi sasa wanahisia juu ya mambo mengi, ambapo wanaisubiri kwa hamu Tume ya Katiba kwa ajili ya kueleza hisia zao.

Sasa nafikiri maoni haya tungesubiri na si katika suala la Rais pengine tunaweza kusema kwamba tumefika pahala hatuhitaji Muungano wa Katiba tunahitaji Muungano wa Mkataba yako duniani. Kwa mfano, *European Union* si Muungano wa Katiba ni Muungano wa Mkataba na ndio maana unaruhusu *flexibility* kubwa.

Kutokana na hali hiyo, inaweza kufika pahala wazanzibari wakasema aa! Hata haya Mamlaka ya *Sovereignty* kila mtu arudi kwake. Kwa hivyo, ikawa hatuhitaji tena Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, nasema kwamba hayo yasubiri mjadala wa katiba utakapofika, basi wananchi watayatolewa maoni tena nadhani wazanzibari wako makini sana katika kulinda mamlaka yako pengine kuliko hata baadhi yetu tuliomo katika chombo hiki.

Mhe. Spika, nimalizie kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu ambaye ni rafiki yangu mpenzi kabisa. Kwanza aliniambia madhumuni yangu ilikuwa ni kutanabahisha, ni kweli na ndio maana bado nimebakia hapo. *(Makofi)*

Lakini nataka nimwambie Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba katika mtu ambaye Wazanzibari wanamheshimu sana, kwa sababu ya kumjua kuwa anao msimamo wa kutetea na kulinda Zanzibar pamoja na maslahi yake basi mmoja ni yeye. Kwa kweli kauli zake humu Barazani, michango yake kabla katika mikutano na makongamano mbali mbali pamoja na maandishi yake mbali mbali aliyoandika yanathibitisha hilo. *(Makofi)*

Sasa nafikiri nimdokolee kwamba wengine wanakuwa na wasi wasi tokea alipoingia kwenye chombo hiki kidogo mara nyengine Mhe. Spika, labda ile *tone* ya *Officialdom* inamfanya ayapoozo baadhi ya mambo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nashukuru sana katika muuongozo wako uliniambia nijikite sana katika suala la *Excusive Economic Zone* na ninajikita huko. Baraza hili tarehe 8 Aprili, 2009 lilipitisha Azimio, ambalo Mhe. Spika ukilisoma kwa makini halikuzungumzia katika suala la *Excusive Economic Zone* suala la mafuta na gesi tu, haidhuru lilikuja katika mughtadha huo.

Mhe. Spika, nilinukuu pale ulipokuwa ukiwahoji Waheshimiwa Wajumbe kwa ajili ya kufunga mjadala ule, basi naomba nirejee tena kwa ufupi tu. Wakati ulipokuwa ukisahihisha ulisema na ninaomba kunukuu.

"Kwa hivyo, pendekezo hili lisahihishwe na inavyoonekana kufuatana na michango ya Waheshimiwa Wajumbe, kwamba eneo hili pia liwe katika mikono ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar". *(Makofi)*

Sasa kule juu Azimio la Msingi ambalo limekataliwa lilikuwa likisema kwamba "Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwahoji wale wanaokubaliana na eneo la *EEZ* sehemu ya Bahari Kuu, serikali inashauri kwamba Waheshimiwa Wajumbe wakubali kuwa suala liende kwa mashirikiano ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Tanzania".

Kwa hivyo, hata kama limekuja katika suala la mafuta, lakini lilikuwa na upana wake. Mhe. Spika, nadhani tusijaribu sasa kulibadilisha na ndio maana sisi tulipoona Serikali ya Jamhuri ya Muungano imepeleka pendekezo au andiko lile hata kama itakuwa imewashirikisha baadhi ya watendaji wa Zanzibar, basi bado hiyo haijahalalisha kufuta Azimio la Baraza hili tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ndio maana nasema amezungumzia kuwa kuna masuala ya muda mimi bahati mbaya sikuyaona. Lakini bila ya shaka serikali itakapokuja kutujibu basi itatujibu na masuala haya pia.

Lakini alipozungumza Mhe. Mwanasheria Mkuu pengine ni mapema mno kusema Serikali ya Jamhuri ya Muungano imekiuka Azimio la Baraza. Mhe. Spika, nasema kwamba huu muhali wa Wazanzibari tuondoshe Mhe. Spika, kwa sababu huku mara nyengine kutaka tuonekane watu wema sisi kwa uungwana wetu pamoja na jinsi tulivyolelewa kwa hivyo maneno ya kuudhi tuyaache, basi ndipo kule upande wa pili tunavyotafsirika kwamba ni udhaifu Mhe. Spika.*(Makofi)*

Kwa kweli Azimio liko wazi ambalo nimelisoma hapa. Sasa kitendo cha Serikali ya Jamhuri ya Muungano kabla suala hili halijamaliza ku-*resolved* kupitia katiba mpya kupeleka ombi hili. Mhe. Spika, ni kwenda kinyume na Azimio la Baraza hili na wala tusitafune maneno katika hilo Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama nilivyosema utaratibu sahihi kwa uzoefu wangu mdogo na ninashukuru na wala sijawahi kuwa katika serikali. Lakini nadhani kwa uoni wangu mdogo kama palikuwa kuna haja kuwa muda hauwahi na pengine tunaweza kuathirika sote, basi ilikuwa ni vyema Serikali ya Jamhuri ya Muungano iwasiliane na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Baraza la Mapinduzi ilete hoja katika Baraza hili, kwa ajili ya kutaka idhini ya Baraza ibadilishe Azimio lake. Hayo yote Mhe. Spika, hayakufanyika. Kwa hivyo, Mhe. Spika mimi katika hayo natofautiana na rafiki yangu Mhe. Mwanasheria Mkuu. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, nimalizie kwa sababu sitaki kuchukua muda wako zaidi. Suala moja ambalo limejitokeza hapa na Waheshimiwa Wajumbe wengi wameligusia na sio katika suala hili tu Mhe. Spika ni kwamba Waheshimiwa Wajumbe wameonesha *concern* zao kuhusu jinsi utendaji wa serikali unavyokwenda.

Vile vile wengine wamempa ushauri mzee wetu ambaye ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwamba sasa anapaswa masuala haya ayaangalie kwa ukaribu kuhusu utendaji wa baadhi ya mawaziri wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tukienda namna hii basi kuna hatari siku tutakuja kuona kwamba tayari timeshajifunga katika mikataba huko na tunakuja kutanabahi hatuwezi kutoka tena. Sasa ukifika wakati huo ndipo utakapokuja ule msingi wa uwajibikaji wa pamoja, kwamba sasa atakayewajibika ikifika hatua hiyo itakuwa si tena waziri mmoja mmoja, isipokuwa itakuwa ni serikali nzima. Mhe. Spika, hatudhani kama tunapaswa tufike huko. *(Makofi)*

Kwa hivyo, niungane na wenzangu waliotoa wito huu kumuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kidogo awe mkali katika utendaji wa serikali, ili mawaziri wajue kwamba kuna mtu ambaye anawasimamia tena anawachunga. Mhe. Spika, kama tulivyoelezwa katika Uislamu ni kwamba sote ni wachungaji na kila mchunga ataulizwa juu ya alichokichunga. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wote waliochangia hoja hii kwa hisia zao walizozionesha na mimi nazitambua, kwa sababu na mimi ni kama wao ninazo hisia kama hizo, kwani nadhani wote hawajaongozwa hapa na dhana yoyote ya kutaka kumsakama au kumuonya mtu. Lakini wanaongozwa na hisia za uzalendo na mapenzi kwa nchi yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba nikushukuru tena. Hivyo, naomba sasa yale mapendekezo niliyoyatoa bila ya shaka kwa utaratibu wako na yale yaliongezwa na Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri utatumia utaratibu wako wa kuwahoji Waheshimiwa Wajumbe, kwa ajili ya kupata kauli pamoja na maamuzi ya chombo hiki, ambacho ni Ngome ya Wazanzibari na Sauti ya Wazanzibari. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa majumuisho hayo.

Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwamba masuala haya yakazingatiwe na serikali na baadaye kutuletea taarifa kama tulivyokubaliana mwanzo, ikichanganya pamoja na lile suala la kuiomba serikali isimamie yale Maazimio ambayo yalikuwepo kama ni pendekezo la ziada wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, suala hili tunawapelekea serikali kwa ajili ya kulizingatia na baadaye kutuletea taarifa.

Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni mmefanyakazi kubwa kwa hii leo na muda uliobaki ni mdogo sana. Kwa hivyo, nataka tusitishe shughuli zetu, ili kumpa nafasi Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora jioni, kwa ajili ya kuja kuwasilisha Mswada wa Kuanzisha Mamlaka ya Kupambana na Rushwa pamoja na Uhujumu Uchumi.

Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana kwa mashirikiano makubwa mnayotoa kwangu pamoja na wasaidizi wangu, ili kufanya shughuli zetu kwa ufanisi mkubwa.

Sasa naomba kuchukua nafasi hii kuahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 6:50 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Kazi Zake, Uwezo Wake na Mambo Mengineyo Yanayohusiana na Hayo

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)
(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima na Afya Njema na kuweza kufika hapa kwa ajili ya kufanikisha majukumu yetu tuliyopangiwa.

Mhe. Naibu Spika, sina budi kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii adhimu leo ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rusha na Uhujumu Uchumi Zanzibar, nashukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Baraza lako Tukufu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kwa michango yao muhimu sana katika kuufanya Mswada wetu uwe mzuri kama unavyoonekana. Naomba kumshukuru kwa dhati kabisa Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Ali Abdalla Ali, mwakilishi wa wananchi jimbo la Mfenesini, Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hiyo. Michanyo ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri iliyotupatia imeonesha nia zao njema katika harakati za kuzuia rushwa hapa Zanzibar. Nawashukuruni sana, ahsanteni sana. Mhe. Naibu Spika, baada ya shukurani hizo sasa naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya kuanzi Mamlaka ya Kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar kazi zake, uwezo wake na mambo mengine yanayohusiano nayo katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu uliwasilishwa katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu na ukachangiwa na kutolewa maoni ili uwe bora zaidi. Ambapo marekebisho yaliyofanywa serikali imeyazingatia ipasavyo. Michango hiyo hasa ililenga zaidi katika marekebisho ya lugha na kupendekeza baadhi ya vijifungu vya baadhi ya vifungu ambavyo viandikwe tena na vifutwe. Mambo ambayo yametekelezwa kwa juhudi kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yao naomba kuvitaja baadhi ya vijifungu hivyo, kujifungu cha 4 cha kifungu cha 24 kimefutwa na kuandikwa upya. Kijifungu cha 5(a) na (b) na kijifungu cha 6 cha kifungu cha 33.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya Mswada huu ni kutunga sheria itakayoanzisha mamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar. Sheria itakayoanzisha mamlaka ambayo itakuwa ni taasisi inayojitegemea yenye mamlaka ya kupokea na kuchunguza vitendo vyote vinavyoshukiwa kuwa ni vya rushwa.

Mhe. Naibu Spika, kutungwa kwa Mswada huu kunatokana na dhamira ya serikali katika kupambana na rushwa ikiwa ni utekelezaji wa sera za CCM kwa kipindi cha mwaka 2010/2020 na Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2010, Sura ya 7 Ibara ya 165 (c) pamoja na mikataba mbali mbali ya kikanda na ya kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuwepo kwa sheria inayopendekezwa katika Mswada huu, masuala ya rushwa kwa Zanzibar yalikuwa yakishughulikiwa na jeshi la Polisi kupitia kitengo chake cha kuzuia rushwa yaani *(Anti Corruption Squad).* katika kitengo hiki mkazo zaidi ulikuwa ni kukamata watendaji wa makosa ya rushwa kuliko kuzuia vitendo hivyo. Vile vile polisi hawakuwa na jukumu la ufilisi wa mali zilizopatikana kwa njia ya rushwa. Hivyo ili kuimarisha vita dhini ya rusha Serikali imeamua kuanzisha sheria itakayosimamiwa na chombo kinachojitegemea na chenye jukumu sio tu kuchukunguza makosa ya rushwa bali pia kuelimisha wananchi kuhusu matatizo ya madhara na athari za rushwa katika jamii.

Mhe. Naibu Spika,

Sehemu ya Kwanza: Masharti ya utangulizi ikiwa ni jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika. Sheria inayopendekezwa pamoja na kutoa tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika ndani ya sheria hii.

Sehemu ya Pili: Inahusu kuanzishwa kwa Mamlaka. Sehemu hii inaelezea kuanzishwa kwa mamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar. Watendaji wake na sifa zao, hesabu, ukaguzi na utayarishaji wa ripoti ya mwaka.

Sehemu ya Tatu: Inazungumzia Mamlaka ya Mkurugenzi Mkuu na uwezo maalum wa kufanya uchunguzi.

Sehemu ya Nne: Inahusu uchunguzi, mali ya mtu anayeshukiwa kufanya kosa la rushwa, kutoa taarifa, kumbukumbu za mali, kuzuia hati ya kusafiria, kukamata mtu, kutoa maelezo yatakayoathiri uchunguzi na mashataka kwa makosa chini ya sheria hii.

Sehemu ya Tano: Inahusu makosa ya rushwa katika uwakala, kishawishi katika kutoa ushauri, kumdanganya muajiri, mgongano wa maslahi, kujinufaisha kutokana na uteuzi wa mdhamini, rushwa katika Zabuni, kukwepa kodi, kufanya magendo, usafirishaji wa fedha haramu, usafirishaji wa dawa

haram, kughushi bidhaa au fedha, matumizi mabaya ya ofisi, kushughulikia mali ya mtuhumiwa, rushwa katika uchaguzi, kutoa rushwa kwa afisa wa kigeni, rushwa ya ngono, faini ya ziada ya lazima na adhabu ya jumla.

Sehemu ya Sita: Inahusu fidia na ahueni manufaa yasiyo halali, fidia nyengineyo, fidia baada ya kupatikana na hatia, kutaifishwa kwa mali isiyo na maelezo na amri ya kuzuia mali inayotuhumiwa.

Sehemu ya Saba: Inaelezea masharti yanayohusu ushahidi kama vile isiyokuwa na maelezo, thamani ya mali, uwazo wa kuagiza uchunguzi na makosa kusikilizwa na Mahakama Kuu.

Sehemu ya Nane: Inaelezea kuhusu kusimamishwa kazi kwa kosa la rushwa au kuhujumu uchumi. Kutangwa kwa waliotiwa hatiani, kinga kwa watoa taarifa, ushirikiano na mamlaka nyengine, kosa lilotokea nje ya Zanzibar, kanuni na kufutwa kwa sehemu ya 10 na 41 ya sheria ya makosa ya jinai Nam. 6 ya mwaka 2004.

Mhe. Naibu Spika, ni matumini yangu kuwa Waheshimiwa Wajumbe wamepata muda wa kusoma kwa makini Mswada huu pamoja na marekebisho yaliyofanywa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na watauchangia ipasavyo na hatimaye kuupitisha ili tuweze kukabiliana na vitendo vyote vya rushwa na uhujumu uchumi katika nchi yetu.
Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitoleaw Ijadiliwe)

Mhe. Panya Ali Abdalla Mhe. (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa jioni hii ya kuweza kuwasilisha hotuba ya Mwenyekiti wa Katiba ya Sheria, Utawala ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar Kazi zake, Uwezo Wake na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote, naomba kuchukuwa fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujalia neema ya uhai pamoja na afya njema miongoni mwetu na kutuwezesha kukutana jioni hii ya leo ili

niwasilishe rasmi mchango wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Kazi zake, Uwezo wake na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada huu muhimu

Mhe. Naibu Spika, aidha, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuhakikisha wizara hii inafikia malengo yaliyowekwa ikiwa ni pamoja na kuandaa na hatimae kuweza kuwasilisha mswada huu kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ili kuipa fursa Kamati yetu kutoa mapendekezo yake kabla ya kuwasilishwa mbele ya Baraza letu tukufu kama Kanuni za Baraza la Wawakilishi zinavyoelekeza.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mtovu wa fadhila nisipowapongeza watendaji wa wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu kwa mashirikiano yao ya dhati waliyotupatia muda wote tulipokuwa tunajadili na kuuchambua Mswada huo. Pia namshukuru kwa dhati kabisa Mwanasheria wa Serikali kwa ufafanuzi wake mzuri alioutoa kwa Kamati. Kwa ujumla wamefanya kazi nzuri na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inazithamini juhudi zao hizo.
Mhe. Naibu Spika, kama kawaida yao Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na wao hawakuwa nyuma katika kutoa michango yao ili kuimarisha zaidi Mswada huu muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.
Mhe. Naibu Spika, naomba kuwatambua Wajumbe hawa kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	-	Mjumbe
6.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	-	Mjumbe
7.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Mjumbe
8.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	-	Katibu
9.	Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	-	Katibu

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kutoa maoni ya Kamati kuhusiana na Mswada ulio mbele yetu, naomba niishauri Afisi ya Baraza la Wawakilishi kuziwezesha Kamati zake za Kudumu kukutana na Wadau mbali mbali kuhusiana na Mswada husika kila serikali au Mjumbe anapowasilisha Mswada ili kupata maoni yao, kwani kama tunavyojua kuwa kitu chochote kikijadiliwa au

kuchambuliwa na zaidi ya mkono mmoja kuna uwezekano mkubwa wa kuibuka mengi ambayo yatakuwa chachu katika kuimarisha utekelezaji bora wa kitu husika, kama Wahenga wanavyosema *'kwenye wengi kuna mengi'*.

Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi na ushauri huo napenda sasa niende moja kwa moja kwenye Mswada.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya Mswada huu ni kutunga sheria itakayoanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Kazi zake, Uwezo wake na mambo mengine yanayohusiana nayo.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa masuala ya Rushwa Zanzibar yanashughulikiwa na Jeshi la Polisi kupitia Kitengo chake cha *Anti-corruption squad*. Isipokuwa Kitengo hiki kinakamata zaidi watendaji wa makosa ya rushwa kuliko kuzuia vitendo hivyo. Hivyo, kupitishwa kwa Mswada huu wa Sheria kutaiwezesha Serikali kuanzisha chombo kinachojitegemea na chenye jukumu siyo tu kuchunguza makosa ya Rushwa, bali pia kuelimisha wananchi kuhusu matatizo na madhara na athari za Rushwa katika jamii pamoja na majukumu mengine kama yanavyoonekana kwenye Mswada husika.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, tunaipongeza serikali kwa kuweka ndani ya Mswada huu adhabu mbali mbali za kinidhamu kwa mtu yeyote atakayefanya kosa la rushwa au kuhujumu uchumi kulingana na uzito wa makosa yenyewe. Hatua hii inaonesha ni jinsi gani nchi yetu inavyofuata misingi ya Utawala Bora.

Mhe. Naibu Spika, tulipendekeza kufanyiwa marekebisho baadhi ya maneno yaliotokana na makosa ya kiuchapaji. Baadhi ya maneno hayo ni; katika ukurasa wa 311 wa Mswada kifungu cha 2(2) mstari wa tatu kutoka juu neno la kwanza 'uweo' limependekezwa lisomeke 'uwezo', ukurasa wa 313 kifungu cha 11 mstari wa kwanza kutoka juu neno "utaolekezwa" limependekezwa lisomeke "utaoelekezwa" na marekebisho mengine mengi kama yanavyoonekana kwenye waraka wetu wa Mapendekezo ya Marekebisho ya Kamati.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu ilipendekeza pia kuongezwe maneno kwenye baadhi ya vifungu ili kuweka mtiririko mzuri wa maneno. Baadhi ya vifungu hivyo vilivyopendekezwa kurekebishwa ni; kwenye tafsiri ya neno "tendo la rushwa" kwenye aya ya (b) tumependekeza yaongezwe maneno "la rushwa" baina ya neno "tendo" na "lililotokea", kifungu cha 22(1)(b) maneno 'nini kilichopelekea' yasomeke 'sababu iliyopelekea' nakadhalika.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hayo, tumependekeza pia kufanyiwa marekebisho baadhi ya vifungu ambavyo maneno yake yanatofautiana baina ya

Mswada wa Kiswahili na Kiingereza. Kwa mfano;- Kifungu cha 18(2)(d) tumependekeza yaongezea maneno “katika vyombo vya habari” baina ya neno “vipindi” na “vitakavyoelimisha”, Kifungu cha 23(5) maneno ‘imepata msamaha au upendeleo wa kutotolewa’ tumependekeza yasomeke “imezuiwa au haikuruhusiwa kutolewa”. Aidha maneno “upendeleo au msamaha huo” yasomeke “zuio au ruhusa hiyo”.

Ili kuokoa muda wako Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waangalie mapendekezo mengine kama haya kwenye waraka wa Kamati.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imependekeza baadhi ya vifungu kuwekwa kiwango cha mwisho cha adhabu ili kuzisaidia Mahkama wakati wa utoaji wa hukumu kutoa adhabu kulingana na kosa lenyewe.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu ilichukua muda mrefu katika kujadili na hatimaye kupendekeza kiwango cha adhabu kwa makosa mbali mbali yaliyokuwemo ndani ya Mswada huu wa Sheria. Hii ni kutokana na kuwa hakuna Sera maalum ya Adhabu inayotumika. Kwa msingi huo, tunaiomba Serikali kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuandaa Sera ya Adhabu *‘Punishment Policy’* ili kupata muongozo juu ya masuala husika.

Mhe. Naibu Spika, ili kuzuia vitendo vya udanganyifu tumependekeza kifungu cha 20(2) yaongezwe maneno “na muhuri wa Mamlaka” baada ya neno ‘Mkuu’. Kwa muhtasari hayo ndio maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Naibu Spika, napenda sasa niwashukuru tena Wajumbe wa Baraza hili kwa kunisikiliza kwa makini, na pia nikushukuru wewe kwa mara nyengine kwa kuniruhusu kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mwisho napenda kutamka bayana kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Raisi, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa asilimia mia (100%) na nawaomba Wajumbe wenzangu wote wa Baraza wauchangie na hatimaye kuupitisha Mswada huu muhimu kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi leo kunipa nafasi ya mtu wa mwanzo ni mtu ambaye mwenye barka katika nchi hii kuweza kuchangia Mswada huu wa Rusha na Wahujumu uchumi.

Nashukuru Wawakilishi wenzangu wa back benchar kwa kazi nzito waliyoifanya leo asubuhi na Ishallah Mwenyezi Mungu awabariki waendelee na msimamo huo huo. Tunaamini wapo wengine na tutaendelea nao.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ametuletea Mswada huu, mimi naamini kwa lengo zuri. Lakini Mheshimiwa ningeomba tujuiulize tayari tumeshajitakatisha halafu ndio tunauleta Mswada huu. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, wasi wasi wangu mimi ni padogo sana. Mara nyingi sana tunavyotunga sheria basi anayeumia ni mtu wa chini kabisa. Ambalo hili suala mimi naliogopa kwa kuwa tayari nataka nijitayarishe kwenda Makka, sasa naogopa sana kuwaumiza watu wa chini kutokana na kupitisha Miswada ambayo haiwaangalii watu wa juu, inawaangalia watu wa chini.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu una jina kubwa, una jina la rushwa, una jina la kuhujumu uchumi. Tukubaliane kwamba rushwa ipo, uhujumu uchumi upo na Mwanasheria wetu atanikubalia mwanafunzi wake nitakayomwambia kuwa ni kesi nyingi sana zipo hizo. Hebu tujiulize Mhe. Naibu Spika, kuna kesi hizi za madai ya kawaida tu, bado hazijahukumiwa na zipo nyingi tu, watu wanakwenda wakirudi. Leo niulize hizi za rushwa ndio kabisa. Nafikiria huko nyuma ilikuwepo sheria hii ya rushwa ipo? Nimejaribu kutafuta hansard lakini sijapata kuiyona. Mwanasheria hebu naomba baadaye uje unielimishe, kwamba Serikali ilitumia kigezo cha aina gani hata kuwepo na sheria ya rushwa na ikawa inafanya kazi. Kilikuwepo kikosi cha *interrupcion* kilikuwepo hicho na ndio kilichokuwa kinahangaika na masuala ya rushwa.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa kwanza 310, kuna kifungu cha sheria hiyo ambayo kama ilivyoonesha hapa kwamba sheria hii itajulikana ni kama sheria ya kuzuia rushwa. Mheshimiwa mimi sina tatizo nacho hata kidogo kifungu hichi. Lakini utekelezaji wake hapa mimi ndio ninapopata mashaka. Tukishuka chini kidogo hapa kuna mamlaka ya kuzuia rushwa. Wenzetu Bara wanaita Takukuru kwa nini na sisi tusitafuta jina tukakipa, tukaeleza bayana, tukataja jina ambalo lingelingana vizuri kama la wenzetu, tukaondoa hili neno Mamlaka, kidogo mimi inanitia wasi wasi. Mimi ningeomba tutafute jina lililokuwa zuri ambalo linakwenda na wakati kwa mawazo yangu mimi. Ikatambulikana Zanzibar wanacho kitu hicho rasmin sana. Wenzetu sasa hivi Takukuru inajulikana na imeonesha macheche yake.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mamlaka hii ndio naiita kiwoga kwa sababu sijafurahika nalo hili neno, lakini kwa kuwa limeshaletwa basi nitaliangalia na wajumbe wenzangu vipi watapolipa nguvu, aidha kuliondoa au kuliweka atajua mwenyewe Waziri katika kuja kutoa hoja zake, lakini nitalitumia hivyo. Wenzetu Takukuru hawaangalii mkubwa wala mdogo, wanafanya kazi zao

vizuri. Tumesikia kwenye uchaguzi, kwenye mambo ya kuhujumu uchumi, kwenye mambo mbali mbali. Lakini mimi wasi wasi wangu hapa najiuliza kweli hii mamlaka itakuwa na uwezo huo. Itakuwa na upeo huo, japo sheria tumeshampa kweli itafanya kazi? Hapo nashindwa kupata jibu, lakini Mheshimiwa wangu waziri atakuja kunisaidia na kuweza kunipa jibu lilokuwa zuri sana.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 311, rushwa maana yake ni. Mheshimiwa fasaha hasa ya rushwa kusema ukweli tunaizungumza lakini hasa hatujaitaja. Rushwa ina maeneo mengi sana, ina tafsiri nyingi sana. Rushwa sio kutoa pesa tu, kuna mambo ambayo unaweza ukayafanya lakini tafsiri yake ikawa rushwa. Kwa mfano, kiongozi ukalitumia jeshi la Polisi na kudhalilisha watu wa chini, tayari hiyo rushwa.

Mhe. Naibu Spika, nasema haya kwa masikitiko sana. Leo bahati mbaya asubuhi sikuja hapa nilikuwepo katika zoezi hilo la kunifanya mimi leo niwe mtu wa mwanzo wa kuweza kuchangia. Nikawa na wasi wasi na kuhusu Mswada huu. Hili Mhe. Waziri nataka nikwambie, lakini madhali keshaingia Mhe. Abubakari naweza nikalipeleka kwake au angelikuwepo Mhe. Mohammed Aboud na yeye ningemwambia kwa upande wake na wewe nakwambia kwa upande wako.

Mheshimiwa viongozi tunalitumia jeshi la Polisi kinyume na taratibu na Polisi wakishakupewa lile tatizo wanalifanya na wao wanaisahau ile sheria kwa kuwa nani, mkubwa fulani kasema. Mheshimiwa hatufiki hivyo. Mheshimiwa nina kituo hangu cha Mahonda naomba mnipelekee salamu kwa Kamishna Waziri wa Mambo ya Ndani, *IGP* mwenyewe, nasema ngazi ya uongozi wa juu, nikisema uongozi wa juu, kuanzia Mkuu wa Mkoa wa Polisi na wa Wilaya na wa chini wake, hawa wote hawafai, wanadhalilisha wananchi. Mimi mwanzo nilikuwa katika mdau mkubwa sana wa Polisi jamii. Mara nyingi nilitetea sana polisi Jamii inatusaidia, nilisema sana kwa uchungu kwa sababu niliona kazi zake.

Mpaka leo tunaona Polisi jamii inavyofanya kazi, wanachukiwa mpaka kwenye vile vituo vya Polisi. Lakini kwa matukio waliyowafanyia wananchi wangu wa jimbo la Kitope nitasema Polisi Jamii sina imani nayo kabisa kwani wananchi wanakwenda kukamata wahalifu kwa kutafuta haki yao wenyewe katika njia ya kilimo, anapewa amri polisi kawakamate wale si rushwa kitu gani, polisi hawaulizi masikini ya Mungu hajui kama yule mwekezaji halali aliyekuwa na kile kiwanda au kutokuwa halali. Mimi nilikuwepo katika katika Kamati ya Ufuatiliaji na mkasema kwamba yule si halali kwa sababu halipi kodi, si rushwa hiyo? Mhe. Naibu Spika, hapa ndipo niliposhangaa polisi wale kuwa hawaangalii hali halisi mimi ndio hapa nikasema Mheshimiwa hii sheria

naogopa mimi kama nilivyosema mimi lazima niende Makka, lakini nitakwenda vipi Makka wakati bado tunadhalilisha jamii.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyokwambia kwamba rushwa ina tafsiri nyingi, viongozi wametumia Jeshi la Polisi kwa kwenda kuwadhalilisha wananchi kwa matakwa yao wenyewe, hiyo tayari ni rushwa. Mhe. Naibu Spika, ungekuwepo wewe leo Mahakamani basi ungelia, mimi nimelia machozi kabisa Mahakamani wallahi laadhimu, haya ni matatizo makubwa sana. Na matatizo haya tunayoyafanya ni sisi viongozi jamani hii itakwisha lini, kila siku tunawadhalilisha wananchi.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Hakimu katumia kifungu kinachosema kuwa ni haki yake mtu kupewa dhamana, wallahi nilishukuru sana tumbo lote lilijaa tena maana yake lilikonda halafu likajaa, taabani nafsi yangu naona leo wale wanakwenda rumande tu. Lakini Hakimu alitumia tafsiri hii ya kifungu cha kuwa hawa wanayo haki yakupewa dhamana, nilisema *alhamdulilah*, lakini ilikuwa ishajengwa mazingira wale wa Kitope wa kalale.

Mhe. Naibu Spika, Mkuu wa Kituo kafika Mahakamani mapema Kituo cha Mahonda kwenda kusema kwa shindikizo kwamba nimemuona kwa jicho langu, Meja mzima anakwenda Mahakamani anakwenda kufanya nini, kwa kuweka shindikizo wale watu lazima wadidimizwe wapelekwe rumande. Kwa haki yao wenyewe, ardhi yao wenyewe inakwenda kuwatesa, hapana kwa mtu mgeni hiyo naomba mheshimiwa tuione tafsiri ya rushwa. Mhe. Naibu Spika, naomba Kamishna hili alisikie na akitaka niridhike na polisi jamii kwa upande wa Jimbo la Kitope wale watu wawaondowe mara moja.

Mhe. Naibu Spika, juzi tu kuna mwananchi wangu baba yake amepondwa na gari wallahi mpaka leo polisi hawajafuatilia mpaka amekufa tumekwenda kumzika juzi na mwenye gari ameachiwa ati wananiambia nendeni Bima, kweli hivyo ndio sheria inavyosema hivyo.

Mhe. Naibu Spika, isitoshe kuna mtu ameuwa watu wawili kwa siku moja na bado leo anakwenda huko mitaani anaringa, hiyo kama si rushwa ni kitu gani na mtu hana hata leseni, wako huko Mkoa wa Kaskazini. Mimi kawaida huwa sisemi kitu cha uongo siku zote nasema kitu cha ukweli, ameuwa watu wawili mpaka leo *file* halijuilikani wapi lilipo, nambie kama si rushwa ni kitu gani? Halafu leo Mhe. Mshimba niseme niunge mkono sheria hii mimi sikubaliani nayo siungi mkono hata kidogo kwa sababu najua mnamuumiza yule mnyonge.

Mhe. Naibu Spika, ukiwa na pesa katika nchi hii ndio mwenye sheria kabisa wala usijali wewe ukiwa na pesa zako fanya unavyotaka mwenyewe utatoa pesa tu. Mhe. Naibu Spika, hii hali ambayo ya Mkoa wetu wa Kaskazini

isitoshe baya zaidi kuna mzungu kwenye hoteli alikutwa na mwanamke wake, basi askari akamuwekea *hands up* akachukua *Euro*.

Mhe. Naibu Spika, baya zaidi mbona halikufanyiwa kazi na polisi, hiyo si rushwa nayo na mpaka leo huyo jamaa hata hakusimamishwa kazi yupo. Mhe. Naibu Spika, mimi nashangaa tunakwenda kuwaonea wale masikini ya Mungu wakulima kwa kuwa nini ati wamepata amri kutoka juu, amri hiyo kutoka juu ni kwa Mungu. Suala hilo linasikitisha sana kwa ukweli kwani hapa Zanzibar hatujawa na mazingira mazuri sheria hii ipo kwa wanyonge tu, jamani tukubaliane je kwa mkubwa hakuna sheria.

Mhe. Naibu Spika, ingekuwa sheria hii kwa mnyonge ipo basi watu wale wasingepelekwa Mahakamani hata kidogo. Kwa sababu alichokifanya yeye kenda kalima pale pahali hapana mua ni bonde safi kabisa kwa kuwa mwaka jana walilima walipata mpunga mwingi na mwaka juzi walilima vile vile, sasa Mkubwa kaona choyo akasema na sisi ndio tunapataka hapa hapa.

Mhe. Naibu Spika, ndio nikasema kwamba hiyo ndio dhana yenyewe inayokuja nayo tuiangalie hiyo ni rushwa hayo ndio katika misingi ya kutumia madaraka kinyume na utaratibu wa sheria. Mhe. Naibu Spika, leo nataka uniachie tu nizungumzie neno rushwa linalohujumu uchumi, maana yake leo asubuhi nilikuwa sipo kwa hiyo kiu yangu yote nitaitoa hapa hapa.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru hivi karibuni kulindwa tume ya uchunguzi wa bonde lile, mimi nawashukuru sana viongozi wangu walifanya kazi vizuri sana na wakaangalia katika maeneo mengi sana. Mhe. Naibu Spika, leo mimi nimefanya sensa baada ya kutoa kule nikapita kwenye vianzio ambapo kwa mujibu wa sheria zinatakiwa zilipwe ikawa yule mwekezaji hajaleta. Kwa hivyo, nimewaambia askari kwanza Shirika la Umeme wanadai milioni 56, katika mle katika mkataba alipewa miezi 48 wa kujiandaa tu halafu ametia saini tarehe 14 Julai, 2005 na mpaka leo mwanasheria atanisaidia. Na tunapofunga mikataba ninavyoelewa mimi ni kwamba kwanza aliambiwa alipe kodi zote ambazo zinalipwa katika nchi, halafu unatakiwa ukifika muda fulani uanze kufanya ile *product* yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, hapa mimi ndipo ninapojiuliza serikali yangu tunangojea nini. Kwa kweli mimi sikusoma sheria basi ninajua sheria kwamba yule mtu ameshavunja mkataba, halafu leo mtu anakwenda kushtaki Mahakamani hivyo anamshtaki nani? Hapo ndipo polisi wanaponisumbua akili yangu kwamba hawafuatii yale mambo wakiambiwa tu na bwana fulani kakamate, wao watakuja kukamata tu, lakini hawaangalii mtu huyu tunamkamata kwa sheria gani. Mhe. Naibu Spika, wewe kwanza unayetoa agizo hilo kweli umehalalika kwenye bonde lile na chakusikitisha zaidi yule yule mwekezaji ametoa ruhusa

mabonde mengi kwamba wananchi walime, isipokuwa bonde hilo tu la 18 ndilo liloekwa maalum kwa viongozi ambalo hilo ndilo waliokuwa wakilima wenyewe wananchi.

Mhe. Naibu Spika, hiyo kama sio rushwa ni kitu gani, sheria hii ikipitishwa na Rais akitia saini mwambie aje mimi nitamuonesha kawakamateni sasa, nitakwambieni kila kitu kawakamateni hao waliotoa amri hiyo. Sisi tukishakusema hapa tunampelekea mwenyewe Dk. Shein akishapale kutia saini ndio sheria inafanya kazi. Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa tayari nitakupeleka nikuoneshe ni huyu na huyu.

Mhe. Naibu Spika, katika sheria yako hii kuna watu ambao watatiwa kwenye sheria, lakini kuna watu ambao watakuwa hawana sheria. Je, hawa kwa mfano wahujumu uchumi watachunguzwa na kumbe yule hakuwa na makosa kachomewa tu kwa kuwa bwana mkubwa ndio hivyo. Kwa hivyo, huyu je haki yake itarejeshwa sikuona mimi humu au mfanyakazi atarudishwa kazini kwa sababu ana ujuzi. Mhe. Naibu Spika, kuna wafanyakazi wengi wamesharudishwa makazini. Kuna mmoja mpaka leo jamaa yangu kutoka Pemba yumo kwenye wizara ya Babu yangu Mhe. Juma Duni Haji mpaka leo hajarudishwa kazini na haki yake hajapewa na kesi ameshashindwa. Mhe. Naibu Spika, ndio mimi nikasema hii sheria jamani inamlenga mnyonge.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna mwengine huko huko Pemba kwa Mkuu wa Mkoa naye alitiwa makosani lakini bahati nzuri ameshinda kwenye Mahakama hajarejeshwa kazini mpaka leo na haki yake hajapewa. Halafu leo tunaleta mswada huu viongozi tuwe makini sana tufikirieni jamani hiki sio kitu cha masihara hata kidogo, sheria ni sheria. Mimi ninavyosema ni kweli yuko mfanyakazi wa Wizara ya Afya mpaka leo hajapewa mafao yake ati kwa kuwa pesa ni nyingi, lakini si mlimfukuza na mkatia kwenye makosa na akaa nje kwa muda wa miaka mingi tu. Mhe. Naibu Spika, naiambiwa Wizara ya Fedha ipeleke pesa kule Wizara ya Afya wapewe haki yao hao wanaodai.

Mhe. Naibu Spika, na huu ndio wasi wasi wangu kwamba mswada huu utamtia makosani mdogo, lakini hatimae akisha kesi humlipi pesa zake, halafu mimi Mshimba niunge mkono, sikubaliani nalo suala hili hata siku moja. Mhe. Naibu Spika, mimi nitaunga mkono pale penye haki. Mhe. Naibu Spika, mimi nimeona ili kuuweka vizuri huu mswada wetu basi tuangalie na zile kasoro zake ambazo moja ni hilo nilolisema, kwamba nimesema humu kuwa mtu anaposhinda katika kesi zake basi mamlaka iweze kumrudishia mtu haki yake kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, twende katika ukurasa huo huo wa 311 Nam. 3 (1) inaanzisha mamlaka hiyo. Mhe. Naibu Spika, sisi tuna *PAC* hapa ni watu wa

ukweli na uwazi, wenzetu Kenya wanapokwenda kufanya kazi katika mawizara wanakuwa wanachukuwa polisi. Kwa hivyo, naomba hii mamlaka yako iwe karibu na *PAC* akigunduliwa mtu basi atiwe pingu pale pale hakuna msalie Mtume hapo. Hiyo mamlaka itakayopita hapa basi iwe karibu sana na *PAC* vyengine vyovyote Mhe. Naibu Spika, basi tutajidanganya tu kwa sababu *PAC* kama katika bajeti walitueleza mambo mengi sana waliyaona mle kwenye mawizara lakini hakuna sheria yoyote ambayo mpaka sasa hivi tuliyosia waliotoa ripoti yao watu wa *PAC* na watu wakaweza kukamatwa. Mhe. Naibu Spika, hilo nalo ni tatizo lakini ili mamlaka yake iende vizuri ni lazima *PAC* wawe karibu nao.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa leo nimejitahidi sana nataka nimalizie, katika mazungumzo yangu mheshimiwa ili kwa kutengeneza vizuri ni kwamba hawa majaji wetu hebu tuwaone hasa tuanzie Mahakama ya mwanzo. Mhe. Naibu Spika, Mahakama ya Wilaya wenzetu wanapata pesa nyingi tu karibu kama milioni 2 na zaidi, lakini hawa Mahakama ya mwanzo Mhe. Naibu Spika, wanapata fedha kidogo.

Kwa hivyo, katika kulinda hii rushwa isiwemo humu Mhe. Waziri wangu wa Sheria waoneni na hawa Mahakama ya mwanzo ili na wao tuwawezeshe haya mambo ya kuwapa 200,000 umepitwa na wakati sasa hii, mimi nataka na wao wanufaike katika haya mafungu mazuri. Kwa hivyo, nalo hilo Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria sasa hivi Mahakama ni nzuri kwa sasa hivi kwani wanapata pesa nzuri kwa hiyo sio rahisi Jaji kwenda kumshawishi sasa hivi, hilo mimi nakubaliana nalo. Mhe. Naibu Spika, lakini huyu Mahakama ya mwanzo hakupata fedha hizo hata kidogo kama kapata nyingi labda 300,000, hivyo ili mazingira yawe mazuri na wao tuwapandishe katika *level* inayostahiki ili tuwawezeshe vizuri. Kwa hivyo, tuwawezeshe ili wafike pahala napo kidogo wajisikie vizuri ili rushwa yetu tuanze kuitengeneza.

Mhe. Naibu Spika, hiyo ndio hali ambayo nitasema kwamba tuangalie kwa jicho la huruma Mahakama ya mwanzo ili kuweza na wao wajisikie katika hali ambayo nzuri. Hicho ndio kilio ambacho nimeona niwasemee ndugu zangu hawa ili waheshimiwa wote mliokuwepo hapa waweze kuongezewa mafao hayo.

Mhe. Naibu Spika, kituo changu cha Mahonda bado kingali kinadhalilisha watu, mheshimiwa anisikie vizuri Kamishna wetu wa hapa Zanzibar ni mtu mzuri sana, lakini na hili aendelee kunisikiliza naomba kuanzia *RPC, OCD*, Mkuu wa Kituo hawatufai tunaomba hili na salamu zangu mzipeleke kwa IGP au kwa Waziri wa Mambo ya Ndani na nina ushahidi tosha wa kusema hili, na wananchi hakisikia hao wameondoshwa katika Mikoa yetu basi watafurahi sana watu jinsi kutokana na matatizo wanayoyapata. Kwa hivyo, hapo mimi

wakiniondoshea watu hao ndio nitaunga mkono polisi jamii tena nitaipigia debe kwa nguvu tu.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, wananchi wangu wa Jimbo la Kitope wameniambia hivi, japo siku moja waziri mmoja alinisemea na leo nitataka tena anisemee namshukuru sana mimi kwa hilo. Mhe. Naibu Spika, kila ninakopita Mshimba ndiye nani na mimi siku zote nasema pale panapo haki simuogopi mtu yeyote nitaelezea ukweli ulivyo mpaka kufa kwangu. Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo namshukuru sana Mhe. Waziri yule kanipigia debe zuri sana leo namwambia nawazungumzia wananchi wa Kitope wameniambia mswada huu nisiunge mkono kwa sababu yakuwa wamedhalilishwa leo.

Mhe. Naibu Spika, naendelea tena kusema mswada huu siuungi mkono. Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kitope kwa sababu wamedhalilishwa leo na mapolisi ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwanza kukupongeza nashukuru kwa kukalia nafasi hii jioni hii ukiwa ndio muongozaji wa kikao hiki. Mhe. Naibu Spika, kwa hakika mswada huu Wazanzibari walikuwa wakiusubiri kwa muda mrefu kwa sababu ni mswada ambao tunategemea kwamba utakomboa uchumi na rasilimali ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nataka niipongeze sana Kamati ya Katiba na Sheria ambayo wewe ndiye unayoiongoza. Mhe. Naibu Spika, ukiangalia ukubwa wa mswada huu na jinsi kamati walivyorekebisha ni mara tatu ya mswada huu kwa hivyo chini yako Mwenyekiti wa Kamati hii nikupongeze sana kwa umakini wenu na najua ni kwa sababu ya uzoefu na utaalamu wenu mlionao wa kisheria.

Mhe. Naibu Spika, kwanza marekebisho ambayo kamati wameyafanya nimeshindwa kuyamaliza lakini naunga mkono yote nikiamini kwamba kamati ina watu makini na nidhahiri kwamba wanakusudia kuutengeneza mswada huu kwa maslahi ya umma. Mhe. Naibu Spika, mswada huu ni muhimu sana na ni muhimu kwa sababu kama utarekebishwa ipasavyo utaendelea kuokoa sana uchumi na mali ya Zanzibar. Kwa sababu tukubaliane kwamba bila ya kuwepo kwa sheria hii rushwa wajanja na wale watu ambao kuwa wanapenda sana kucheza *deal* watakuwa wanachukua nafasi kubwa ya kuhujumu uchumi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa najiuliza kipi kingeanza mwanzo kati ya mswada huu na mswada wa maadili ya uongozi wa kutangaza mali zetu wazi wazi. Mimi nilifikiria na pengine humu ndani ya mswada huu Mhe. Waziri angeweza akaazilisha kwamba kabla ya kwenda kwenye rushwa basi tungeanza kutangaza mali zetu, ili Wazanzibari wakajua kwamba mali zetu ambazo

tunazo ni halali na hazitokani na mikono ya rushwa. Lakini kama hilo bado na kama hili halimo ndani ya sheria hii basi namuomba Mhe. Waziri naomba sana uzingatie ili kile kiongozi aliyekamata nafasi hapa ndani ya serikali yetu hii tukiwemo sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, basi tuwe wazi tutangaze mali zetu ili Wazanzibari wanyonge watupime kwamba kweli na sisi tulikuwa viongozi kwa ajili ya maslahi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa misingi hiyo sasa mimi nianze kuzungumzia kifungu cha 4 cha uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka hii. Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono kabisa kwamba Mhe. Rais tumpe jukumu hili la kuteuwa Mkurugenzi Mkuu, tumpe jukumu hilo kwa sababu ya misingi yote ya Katiba lakini isiishie hapa.

Mhe. Naibu Spika, inawezekana siku moja tukapata Rais ambaye si muadilifu, nashukuru kwamba tunapata Marais waadilifu sana. Lakini ikiwezekana siku moja ikatokezea tukapata Rais ambaye asiyekuwa muadilifu na ambaye tumempa jukumu hili la kuteuwa Mkurugenzi yeye mwenyewe akawa ni mla rushwa. Kwa hivyo, mimi nashauri kwamba baada ya Mhe. Rais kumteuwa Mkurugenzi huyu lazima Baraza la Wawakilishi liridhie uteuzi huu ili baadae ikitokezea kwamba viongozi wetu wakubwa wanakula rushwa na mkurugenzi huyu akaamuwa kuwalinda basi tuweze kuwa na nguvu ya kumuondoa madarakani.

Mhe. Naibu Spika, wako Marais duniani hapa wamekuwa ni wala rushwa wakubwa. Kwa hivyo, si jambo la kushangaza kwamba inawezakana siku moja Zanzibar tukapata kiongozi huyu ambaye ni mpenda rushwa. Kwa hivyo, tukimuachia madaraka haya ya kuteuwa Mkurugenzi Mkuu bila ya Baraza lako tukufu kuidhinisha uteuzi wake basi ni tatizo kubwa. Kwa hivyo, naomba madaraka haya tumuachie Mhe. Rais amteuwa lakini Baraza letu liridhie ili hatimae baadae iwe rahisi kumuondoa madarakani iwapo atalinda viongozi wakuu wa serikali hii.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kwenye kifungu hicho kifungu cha 7 tumeambiwa kwamba kuna sifa za Mkurugenzi, sifa za Mkurugenzi tumeambiwa ni mtu ambaye atakuwa angalau na *degree* moja.

Mimi nasema kwamba sasa umefika wakati wakuwathamini wenzetu waliosoma, kwa hivyo napendekeza hapa kwamba Mkurugenzi Mkuu tuondoshe angalau shahada ya kwanza na tuweke shahada ya pili. Kwa nini? Kwa sababu tukiwachukua hao wa shahada ya kwanza tu maana yake tunawaacha shahada ya pili na ya tatu wakiwa hawana kazi. Kwa hivyo, sheria hii nashauri kwamba kifungu tumteuwe Mkurugenzi wa mamlaka angalau shahada ya pili nikiamini kwamba Wazanzibari shahada ya pili wapo, shahada

ya tatu wapo na hawana kazi yoyote. Mhe. Naibu Spika, hivyo hivyo Naibu Mkurugenzi angalau yeye tumpe shahada hiyo kwanza ili tuweze kuweka tofauti.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka nilizungumzie ni kifungu cha 9 (b) mapato ya vyanzo vya fedha za mamlaka, ni kwamba ni ruzuku misaada ya kifedha na mambo mengine. Mhe. Naibu Spika, mimi natoa wasi wasi kwamba tukiruhusu kwamba mamlaka ya rushwa ipokee ruzuku, ipokee misaada ni dhahiri kwamba tunawatafutia chaka wale wahalifu wa uchumi kuuwa uchumi wetu. Kwa nini? Kwa sababu mswada ukitolewa unaweza ukatafsiriwa kwa jina jengine ukaitwa takrima, zawadi au hidaya.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi ushauri wangu ni kwamba tuangalie lugha nyengine lakini tusiwape mwanya mamlaka kupokea ruzuku za misaada hata kwa watu binafsi. Mhe. Naibu Spika, inawezekana kuwa ni chanzo cha kuwafanya wenzetu hawa wapokee rushwa na walindwe wale watu wa rushwa kwa ajili ya kuhujumu uchumi wetu. Mhe. Naibu Spika, naendelea kusema kwamba mswada huu iwapo kweli tuna dhamira ya kulinda rasilimali za uchumi wetu, humu mna kifungu kinasema kwamba mtu ambaye atatoa rushwa ya ngono adhabu yake ni milioni tatu au kifungo.

Mhe. Naibu Spika, mtu aliyekomaa kwa adhabu ya ngono haoni tatu kumuhonga ghorofa, watu wanahonga ghorofa aje ashindwe kuja kutoa milioni tatu kwa ajili ya kujilinda. Kwa hivyo, adhabu ya huyu mtu ambaye kuwa amedai rushwa ya ngono isiwe milioni tatu, na kifungu hiki kiondoshwe. Mimi nasema adhabu yake iwe ni milioni 50 na miaka isipungue 15.

Mhe. Naibu Spika, kuna utafiti usio rasmi kwamba baadhi ya nchi huwezi kupata ajira kwa masikini ikiwa hukudaiwa rushwa ya ngono. Kwa hivyo, tukitoa mwanya kwamba mdai rushwa ya ngono atoe milioni tatu, nadhani hii si adhabu adaiwe milioni 50 na kukimkamata afungwe miaka 15 ili akome kufanya tendo hili.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya umakini wa mswada huu niseme tu kwamba mamlaka inayohusika ya kulinda uchumi wetu na maadili ya uongozi basi iwe makini na ijue kwamba tumeiweka kwa ajili ya kulinda uchumi wetu na sio vyenginevyo.

Mhe. Naibu Spika, rushwa ina uwanja mpana, kwa hivyo kila tendo ambalo rushwa imekataza Wazanzibari wanategemea kwamba litawekwa wazi na wahusika watatajwa kila pale ambapo wanastahiki kutajwa. Hatuwezi kutunga sheria ambayo itakuwa inakwenda kisiri.

Kwa hivyo, ni matumaini yangu kwamba sheria hii ikipita kila mtu ambaye amedai au amepokea rushwa ni vyema kuwekwa wazi ili Wazanzibari wajue kwamba huyu ni adui kama walivyo maadui wengine wa malaria duniani.

Mimi nishauri tu Mhe. Naibu Spika kwamba, Mhe. Waziri wakati atakapomaliza mswada huu na Mhe. Rais akishatia saini na hata pale katika utungaji wa kanuni basi nimuombe sana afanye uadilifu, awe wazi na aweke kanuni ambazo zinakusudia kuokoa uchumi wetu, vyenginevyo kanuni ikiwa legelege basi wahalifu wa rushwa wanaweza wakapenya na hatimaye mswada huu ukawa hauna maana yoyote.

Nimalizie kwa kusema tu kwamba, kuna haja bila ya kuona aibu kila kiongozi muadilifu ataje mali yake vipi ameipata ili Wazanzibari wanyonge waridhike kwamba kweli viongozi wao wako kwa ajili yao na nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri akinijibu maswali yangu akinijibu kwa ufasaha na hasa la Mkurugenzi wa Mamlaka basi nitaunga mkono mswada huu nakushukuru sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuzungumza machache kuhusu mswada huu wa kuanzishwa kwa Mamlaka ya Rushwa na Kuhujumu Uchumi.

Kabla sijaingia kwenye mswada kulikuwa na mambo mawili nilikuwa nataka kuuliza, tulipofanya semina hii kwenye Mwezi Mosi Ramadhani iliyopita kulikuwa na jambo fulani lilifanyika pale la ziada, sasa mantiki yake sikuiona katika mswada huu. Kulikuwa na kitu cha nyongeza ya maadili ya kazi. Sasa namuomba Mhe. Waziri aje atueleze mchanganyo ule ulikuwa na faida gani siku ile ya semina ya leo ikawa haimo kuhusu maadili ya kazi.

Suala la pili ni kwamba, katika kuondoa tashwishi za kupendeleana katika kazi kuna tathmini ya mfanyakazi ambayo kikawaida huwa inafanywa kila mwaka (*job appraisal*). Sasa siku ile tuliyofanya semina ni moja kati ya jambo lililozungumzwa sana, lakini vile vile sikuliona kupatikana katika mswada huu. Sasa namuuliza Mhe. Waziri yale mambo mawili yalikwenda wapi?

Kwa sababu gani nikayataja hapa, Mhe. Naibu Spika, makosa mengi duniani yakiwemo haya ya rushwa na kuhujumu uchumi yanategemea sana na ile nchi, ile namna yanavyofanyika yanategemea na ile nchi yanayofanyika. Hili hili neno rushwa, rushwa inaweza ikatolewa Zanzibar pengine ni tofauti na rushwa inayotolewa katika nchi za ulaya, haidhuru ni ile ile rushwa. Kwa hivyo, ule utamaduni wa pale pahali na watu mazowea yao unapelekea kupatikana kwa rushwa za aina fulani ambazo si rahisi kwa mtu mwengine kuzitambua.

Sasa moja katika rushwa ambazo zinapita katika maofisi ya serikali ni kupandishana vyeo. Hii mimi nilishukuru sana siku ile ya semina kwamba ilionekana kuwa kuna haja ya kuweka misingi ya maadili ya kazi ili kuwazuwia watu wengine wasitumie nafasi zao kwa kuwahujumu watu wengine katika kazi na matokeo yake uchumi ukahujumika. Kwa sababu tunaweza tukawahujumu watu katika kazi lakini ni watengenezaji wazuri wa uchumi wa nchi, lakini kwa sababu wewe humpendelei kwa wakati ule au kiongozi wa juu hampendelei kwa wakati ule akamtafutia majanga na majungu matokeo yake akafaitika.

Kwa hivyo, kinadhatia ya juu juu utaona kama kwamba shughuli zinakwenda, lakini kindani kuna kuhujumiana humo ndani kwa ndani na nchi inazidi kudidimia. Kwa hivyo, mimi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri kwa nini mambo haya mawili hayakupewa uzito katika mswada huu ambayo kwa Zanzibar yapo kwa aina fulani. Hata kama mtu ana uwezo, ana kipaji cha elimu, ana kipaji cha uendeshaji lakini kama hajulikani na mtu fulani, kama hana uso uliokuwa unachongeka kidogo ananyimwa fursa. Hilo la kwanza Mhe. Naibu Spika.

La pili Mhe. Naibu Spika, napenda nipongeze wizara hii pamoja na waziri wake pamoja na mambo yote, lakini bado wakaona ipo haja ya kuleta mswada huu. Mimi nathamini sana kauli aliyoitoa ambaye sasa ndiye Mwanasheria wetu wakati ule nafikiri alikuwa *DPP* alisema bora tuanze kuliko kuambiwa hakuna kitu. Na mimi nakubaliana naye ni Baraza hili hili zinaletwa hizi wakati tushajua makosa yaliyomo kwa wakati huo mambo gani yanatatiza tutakuja kurekebisha kama tulivyoanza kurekebisha juzi katika miswada mingine, lakini hivi tulivyoanza ni hatua moja mbele.

Kwa hivyo, natoa pongezi na shukurani zangu kwa Mhe. Waziri na watendaji wote kwa kuona kwamba muda huu watuletee mswada huu. Pia naipongeza Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi yao nzito waliyoifanya katika kuupitia huu mswada na wakatoa mapendekezo yao waliyotoa.

Mhe. Spika, mimi kwanza nakuja katika kifungu Nam. 4 cha Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu. Hii mamlaka Mhe. Naibu Spika, kidogo ingechukuliwa kwamba ni tofauti na chombo cha kiserikali moja kwa moja. Kwa sababu mamlaka hii kazi yake inafanana fanana kidogo na hizi kazi tunazozifanya sisi Baraza la Wawakilishi, kuwafuatilia mienendo zaidi ya viongozi na watu wengine katika nchi. Sasa haya mambo ya uteuzi wake ungelifanywa tofauti kidogo, mimi sikubaliani na utezi uliowekwa hapa kirahisi namna hii.

Katika kifungu 4(1) pameandikwa kwamba, ‘kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ambaye atateuliwa na rais’ halafu chini huku kwenye 7(a) wakasema, ‘Mzanzibari mwenye taaluma angalau ya shahada ya kwanza ya sheria, uzoefu usipungua kipindi cha miaka saba’.

Sawa lakini hapakutajwa umri hapa, mimi nadhani *degree* ya kwanza hivi sasa mtu anaweza akaipata kwenye miaka 20 na baada ya miaka saba kwa 27 tayari ameshakuwa na uzoefu wa miaka saba huyo, ndio awe Mkurugenzi wa Mamlaka kama hii ya Kupambana na Rushwa kijana wa miaka 27? Naona hapa pana mashaka kidogo.

Mimi nafikiria kwamba kama ambavyo anawekwa rais na umri wa kiongozi kama huyu wa kupambana na rushwa basi na umri wake utizamwe hivyo hivyo, asiyepungua miaka 40, haiwezekani kuchukua kijana tu wa miaka 27 kwa sababu ana *degree* ya sheria na uzoefu wa miaka saba ukamwambia huyo ndiye Mkurugenzi wa kuzuia rushwa, yeye mwenyewe atapokea rushwa kuliko hao wengine nakuhakikishieni, kwa sababu umri wake unamruhusu kufanya mambo kama hayo hajatulia bado katika *brain* yake. Kwa hivyo, kiongozi kama huyu lazima apangiwe umri awe angalau kesa *settle* katika harakati zake, lakini kumchukua kijana wa miaka 27 au 30 ukamwambia wewe ndiye Mkurugenzi wa Mamlaka kwa kweli hapa tutakuwa tunacheza.

Nashukuru kwamba kifungu Nam. 7 kimemtaja kuwa ni Mzanzibari, naunganisha na yale maneno ya mwanzo kwamba rushwa wakati mwingi inategemeana na utamaduni uliko katika nchi mbali mbali. Lakini mimi nataka nimuombe Mhe. Waziri afikirie tena baadhi ya mambo ambayo bado ziwe sifa za huyu. Mimi niliongeza vifungu vitatu hapa naomba Mhe. Waziri akavitizame.

Kwanza tulisema kwamba mtu huyu ambaye atakuwa na sifa hiyo atateuliwa na rais mwenye umri usiopungua miaka 40, Mzanzibari mwenye elimu hiyo hapo iliyotajwa, lakini awe anaheshimika katika jamii, hatuwezi kuwa na kiongozi katika mamlaka kama hii ikawa jamii haimuheshimu. Leo anaonekana katika *club* hii, kesho hii, keshokutwa unasikia keshapata kesi hii, hiyo haiwezekani lazima awe anaheshimika katika jamii.

Lakini kwa sababu yeye anataka kuzuia rushwa awe yeye mwenyewe keshajizuiya angalau ana pahala pa kukaa, hatuwezi kumchukua mtu hata nyumba hana ya kukaa tukampa dhamana kama hiyo, atatafuta rushwa kwanza apate ghorofa yake. Kwa hivyo, nasema awe makazi ya kudumu hapa Zanzibar, inawezekana ni mtu mzuri lakini ana *jump* vile vile.

Lakini la mwisho napenda niungane na Mhe. Hija Hassan ambaye amezungumza ingawa mimi sikutaja neno alilolitaja yeye, lakini nimesema awe amethibitishwa na Baraza la Wawakilishi, kwa sababu ni kazi ya uaminifu mkubwa, kazi ya fitna kubwa, anaweza akaiparaganya nchi mara moja au akakaa tu ikawa wengine wanashtakiwi wengine hawashtakiwi, wengine wanaonekana wala rushwa na wengine wanaokula rushwa kweli kweli hawaonekani.

Sasa nasema tatizo letu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba hatutaki kufanya mabadiliko katika taratibu zetu za kiuongozi, unaposema tu athibitishwe na Baraza la Wawakilishi kuna watu washajitwika mikono hapa, lahaula anatuletea nini tena huyo, hivi hatutokwenda. Kwa sababu kuthibitishwa na chombo kama hiki ndio yule kiongozi unampa ule uzito wa kuona kwamba kakabidhiwa dhamana na kwa sababu Baraza la Wawakilishi ni chombo cha usimamiaji wa serikali ndipo atakapojua yeye kwamba aa mimi sikuteuliwa na rais tu, lakini ninawajibika kwa chombo kilichonithibitisha.

Nadhani nchi za wenzetu ndivyo zinavyofanya, kuna baadhi ya vyeo Mhe. Rais hupewa akateuwa moja kwa moja, lakini kuna baadhi ya vyeo hupewa nafasi ya kuteuwa jina halafu kukawa na *session* maalum ya bunge akenda akaulizwa maswali akajieleza na bunge likamthibitisha au lisimthibitishe.

Kama nilivyosema mwanzo hiki chombo kinawachunguza wote wale wa *executive*, wale wa Baraza, wa Mahkama, ni chombo kinachochunguza wote. Sasa lazima apate uthibitisho huyu Mkurugenzi wa Baraza la Wawakilishi.

Mimi binafsi kama mambo mawili katika hayo hayatokubalika basi nitapiga mguu, nitampigia buti Mhe. Waziri mpaka ipigwe kura nitakubali kushindwa kwa kura. Umri usiopungua miaka 40 na kwamba amethibitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, hali hiyo hiyo yende kwa Naibu Mkurugenzi sina haja ya kuyarudia. Isipokuwa katika kifungu Nam. 6(1) kile kinasomeka ‘Rais anaweza kumteuwa’, mimi nasema kisomeke ‘Rais atamteuwa’ kwa sababu hakuna mtu anayefanya kazi peke yake, rais awajibike hasa kuteuwa Naibu Mkurugenzi, ikiwa atateuwa yeye vile vile basi rais ateuwe, alazimike yaani katika Kiingereza ‘me’ isomeke ‘*shall’. The president shall appoint the Depute Director.* Kwa sababu akija rais akisema huyu anatosha pengine ndio keshamuweka mwenzake mambo yataharibika. Kwa hivyo, nasema kifungu kisomeke Rais atateuwa Naibu Mkurugenzi na sio anaweza kuteuwa, lakini mambo niliyoyataja kwa Mkurugenzi yawe hayo hayo kwa Naibu Mkurugenzi.

Mhe. Naibu Spika, na hapo tunaweza kusema pia kwamba wasitoke familia moja, Rais atateuwa Naibu Mkurugenzi ambao hawatokani familia moja na Mkurugenzi, lazima tuweke vipengele ambavyo vitawazuwia viongozi kutumia madaraka bila ya kufanya hivyo tutakuja kuzongana humu humu kisheria, Mkurugenzi anaweza kumteuwa mjomba wake lakini naibu hawezi tena atateuwa mwengine. Haya mambo ya kuoneana haya ndio yanayotepelekea tukafika hapa, kwa sababu mtu anaachiwa kuteuwa mtu anayetaka sasa anateuwa mjomba wake, kwa sababu kuna nafasi za wanawake na shangazi pia na mama mdogo, lakini tusiweke *loop hole*.

Kifungu Nam. 8 Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika kifungu nambari 6 hapa tunapendekeza kwamba isomeke 'Mamlaka itateuwa au kuajiri', sio kwamba inaweza. Kwa sababu katika kufanya kazi zake lazima ipate na *team* ya kufanya kazi. Kwa hivyo, wakati ikitokezea ilazimike kufanya hivyo sio wakati wanaotaka.

Mhe. Naibu Spika, kifungu Nam. 9 kina wasi wasi kidogo. Fedha za mamlaka hii haziwezi kuwa ruzuku na misaada, mamlaka nyingi wanaweza wakapata fedha hizi, lakini mamlaka hii nakubaliana na wenzangu waliochangia kwamba kifungu cha (b) kifutwe kabisa. Fedha za mamlaka hii zitokane na lile fungu lililopitishwa na Baraza la Wawakilishi moja kwa moja, ikiwa zinatosha zitatumika, hazitoshi litaletwa tena haba katika Baraza kuweza kurekebishwa. Kwa sababu tukianzisha hii nani atakuwa na ufuatiliaji kwamba viongozi wale au mamlaka ile haikupokea rushwa katika kupata ile ruzuku, itakuwa tunaweka mamlakama ya kuondoa rushwa lakini tunakubaliana na rushwa hatujafanya kitu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo kuhusu vifungu sasa nasema mimi kwamba sisi hapa katika serikali au hapa Zanzibar kuna mambo manne makubwa ambayo rushwa yake ndio hujuma yake ya uchumi inakwenda sambamba.

Kwanza uuzwaji wa majengo ya serikali. Mimi nilibahatika kuwa mmoja kati ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi niliyekaa vipindi viwili katika Kamati ya Fedha na Uchumi, haya majibu tunayopewa hapa na baadhi ya mawaziri wanatufikiria kwamba sisi hatujui kitu, hili ndio tatizo. Thamani ya majengo ya Mji Mkongwe ni kubwa mno kuliko inavyotajwa humu katika Baraza na wanaotwambia hivyo ni hao hao katika Wizara ya Fedha, wako watu maalu waliosomea kutathmini majengo, jengo halina maana ya matofali na paa lake, lakini pahala lilipo, historia yake na mambo yake mengine lina thamani tofauti. Sasa haya mambo ya kuja kuparaganya majibu ya kiovyo ovyo humu yana mashaka.

Kwa hivyo, uuzwaji wa majengo ya kiserikali ni eneo moja wapo kubwa la kuangaliwa katika kitengo hiki, kama haijaangaliwa basi tutakidharau mapema sana.

La pili, ukodishwaji au uuzwaji wa ardhi. Kisiwa hicho hapo, mimi si mwenyeji sana hapa cha Changu, hiyo bei iliyokodishwa utaweka mikono kichwani. Kisiwa kizima kinakodishwa kwa bei chee. Hilo la pili.

La tatu, mikataba ya serikali inasua sua sana, mikataba inayotiwa kwenye kampuni au kwenye shughuli nyengine za ununuzi na mambo mengineyo inasua sua sua sana. Haya ni maeneo ambayo lazima yatizamwe kweli kweli kwa sababu yanafanya kazi zote mbili, rushwa inakuwepo lakini na uhujumu wa uchumi unakuwepo.

Leo Mhe. Naibu Spika, tuna jengo kule Pemba na wewe umeliona ardhi haitumiki wala jengo halitumiki linakaa kama dudu tu hakuna aliyepata faida. Pemba haikunufaika, Serikali haikunufaika, wala Wizara ya Fedha iliyojenga haikunufaika, hakijulikani kifanyike nini na mpaka leo hakuna jibu kila mmoja anamtupia mpira mwenzake. Yote ni nini, mikataba.

Mhe. Naibu pika, ndani ya hii mikataba na manunuzi zogo lote hili watu hukimbilia asilimia kumi ya *commission*. Si vibaya Zanzibar kufikiria kwamba kuwe na mfuko maalum wa asilimia kumi zinazopatikana kwa mikataba ziende kuingia katika fedha za kuwasomeshea vijana wetu. Tuwatazame hao wakurugenzi na wakubwa wengine watakimbilia kusaini hiyo mikataba. Ikiwa Baraza hili litapitisha kwamba ile asilimia kumi ya *commission* inayopatikana kwenye mikataba iwe na mfuko maalum wa kuwasomesha vijana wetu na kuzichangia zile skuli zilizokuwa hazijaezekwa maana wizara inashindwa.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa kweli unakusudia kuondoa rushwa tuletee mswada huo tutaupitisha kwa nusu saa tu unakwenda zake. Asilimia kumi ya *commission* Zanzibar inakwenda katika mfuko maalum wa kuimarisha elimu Zanzibar utazame. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tukiwa *serious* huu mswada ni mzuri, yapo mambo yatakayokuwa yana kasoro yatarekebishwa mbele, yapo mambo ambayo yatakuwa yenye kuongeza, yapo mambo yatakuwa ya kuchunguzwa. Lakini kama tunavyosema kwamba tuuanze kwanza wanasheria wetu wapo, wataalam wetu wapo watatuongoza na sisi tutaangalia wapi tunapokwama. Baada ya hayo ikiwa Mhe. Waziri atakuja na kauli nzuri basi tutaupitisha mswada.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia jioni hii. Mhe. Naibu Spika, mimi nitakwenda moja kwa moja katika kifungu cha 46 kinachohusu wafanyabiashara naomba kunukuu.

Kifungu cha 46:

> "Mtu atakayeficha bidhaa kwa madhumuni ya kuzuia au kupunguza usambazaji au kueneza bidhaa ili kujitengenezea bei ya bidhaa hiyo kwa maslahi au faida yake atakuwa ametenda kosa la kuhujumu uchumi chini ya sheria hii."

Mhe. Naibu Spika, desturi yetu Wazanzibari kutokana na ukarimu wetu tunavyoishi mimi naweza kuwa na ghala akaja akatokea mtu tu yupo Dar es Salaam au Mombasa na mzigo wake ukapitia hapa nikaweza kuuhifadhi katika ghala lile. Itabidi kuja kuingia kwenye kosa kwa sababu ya wafanyabiashara tu wenyewe kwa wenyewe kuja kuchomeana.

Hichi kifungu Mhe. Naibu Spika, tukiangalie kwa makini vyenginevyo kuwapunguza wafanyabiashara kuja kuwekeza hapa. La si hivyo, tutakuja kutafuta mchawi. Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi kiangaliwe upya kwa sababu kinaweza kutumika vibaya.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije kifungu cha 56 naomba nikinukuu. "Mtu yeyote ambaye kwa nia ya kuathiri utaratibu wa upigaji kura wakati wa uchaguzi wowote atampa rushwa mtu mwenigne yeyote ama moja kwa moja au vyenginevyo kwa lengo la kumshawishi mtu huyo au mtu mwengine yeyote kupiga kura au kuacha kupiga kura atakuwa ametenda kosa." Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi kiangaliwe kwa makini sana.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 56 kinahitaji kiangaliwe upya kwa sababu kinatofautisha vitu viwili rushwa na sadaka. Kwa mfano, unaweza kumpa mtu shilingi elfu moja jimboni ukaambiwa umeshampa rushwa, wakati hali za wazee wetu tunazijua, skuli mbovu mabanda yanavuja, mtoto sare ya skuli katia viraka. Sasa umekwenda jimboni umekuta wazee unataka kuwasaidia kuwapa shilingi elfu tatu ukaambiwa tayari umeshafanya kosa la rushwa. Mhe. Naibu Spika, halikadhalika kifungu hichi kitawaumiza sana wanyonge watajikuta wanaingia katika hatia bila ya hatia.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 61 kinazungumzia adhabu kwa mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya rushwa lakini adhabu hii imependekezwa kuwa faini isiyopungua shilingi milioni moja au kifungo cha miaka miwili. Mhe. Naibu Spika, adhabu hii ni kubwa. Kwa mfano, mtu aliyepokea rushwa ya shilingi elfu tano haiwezekani adhabu hiyo sawa sawa na mtu aliyepokeza shilingi milioni kumi.

Mhe. Naibu Spika, rushwa ni tatizo katika jamii lakini lazima tutofautishe baina ya sadaka na rushwa. Wengi wasiokuwa na hatia kwa kupokea sadaka ya ahsante kutokana na Wazanzibari kuwa na moyo wa kumcha Mwenyezi Mungu.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 58 naomba kunukuu. "Mtu yeyote mwenye mamlaka ambaye atatumia madaraka yake kudai au kuomba ngono kwa mtu yeyote kama sharti la kutoa ajira, kupandisha cheo, kumpatia haki, upendeleo au huduma maalum atakuwa amefanya kosa na atakapopatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kifungo kisichopungua miaka miwili au adhabu zote mbili kifungo na faini."

Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi cha 58 kimewalenga moja kwa moja wanaume, ni vizuri kifungu hicho kingesomeka kwa wanawake vile vile. Mwanamke anaweza kutumia madaraka yake ya kudai au kuomba ngono akipatikana na hatia atakuwa ni mkosa. Kuna wanawake humu wanapandishwa vyeo ni mtihani Mhe. Naibu Spika. Aidha, adhabu hii ipendekezwe faini ya shilingi milioni tatu au adhabu ya kifungo miaka miwili jela kuliko adhabu iliyopendekezwa watu watakaopatikana kwa njia hii ya kuhujumu uchumi. Mhe. Naibu Spika, haiwezekani mtu huyo aambiwe amehujumu uchumi.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 76 naomba kunukuu. "Mtu aliyepatikana na hatia kwa kosa la rushwa au kuhujumu chini ya sheria hii atakuwa na sifa za kuchaguliwa au kuteuliwa kama ofisa kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia tarehe aliyotiwa hatiani." Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi kinapaswa kuangaliwa kwa makini ili haki iweze kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa sheria hii haijazungumzia suala la viongozi kutangaza mali wanapoingia madarakani na wanapomaliza madaraka yao. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kwa mara nyengine tena kusimama hapa leo hii mara hii nikiwa nami natoa mchango wangu kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu Uchumi Zanzibar, Kazi zake, Uwezo wake na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii lakini pia niseme kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo maoni yetu kwa kiasi kikubwa tumeyaleta hapa kupitia waraka huu ambao umewasilishwa wa mapendekezo ya marekebisho katika maeneo mbali mbali.

Lakini utakumbuka Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa wewe ndio mwenyekiti wangu katika kamati hii kwamba yalikuwepo maeneo kama mawili ambayo nilisema nitayatolea maoni yangu hapa kwa sababu tulikuwa na mawazo tofauti katika kamati. Lakini nadhani pia yapo maeneo ambayo tayari tumekubaliana katika marekebisho ningependa kuyatilia nguvu tu ili wajumbe waelewe zaidi msingi wa mswada huu. Lakini kabla ya kuingia huko Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nianze kwa kuipongeza serikali na kumpongeza Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Haji Omar Kheir kwa kuchukua juhudi za kuhakikisha mswada huu unafika mbele ya Baraza hili.
Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya wajumbe wameeleza hisia zao kwamba labda wakati haujafika na kwamba labda utaishia kuwakomoa maofisa wa ngazi za chini na wananchi wa kawaida. Mhe. Naibu Spika, mimi siamini hivyo. Kwa sababu kama alivyozungumza kaka yangu Mhe. Rashid Seif Suleiman mara nyingi tunaambiwa kwamba kama kuna tatizo katika jamii tukingoja binaadamu wawe tayari kwa suala hilo kawaida ya binaadamu hawi tayari, lakini ni sheria inayomfanya akawa tayari, ni kanuni inayomfanya akawa tayari.

Mhe. Naibu Spika, tusiende mbali, sisi sote ni waja wa Mungu ingelikuwa tungengojwa mpaka tuweze kutimiza yale masharti tuliyowekewa ndani ya vitabu vyetu kwa waislam kuran tukufu basi nadhani kuran isingeshuka maish. Maana binaadamu mpaka itamalizika dunia kuna mambo tumekatazwa katika kuran hatutakuwa tayari nayo kwa sababu tu nafsi haitaki na ndio msingi wa kuwepo sheria. Sheria zinawekwa ili kutuweka sawa, kutupa muongozo, kujenga misingi ambayo kama jamii tunapaswa kwenda nayo pamoja. Yale ambayo kwa mmoja mmoja hatuwezi kuyatekeleza kama jamii inatuwekea utaratibu ndivyo ilivyo katika dini zetu na katika nchi zetu kama wananchi ndio wanaotuongoza.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naipongeza serikali kwa hatua hii kwa sababu nasema tukingoja tuwe tayari hatutakuwa tayari, tutakuwa tayari kupitia utekelezaji wa sheria hii, tunaweza pengine tukapambana na changamoto hapa na pale lakini ndio kawaida na maumbile ya binaadamu.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, niwakumbushe wajumbe wako bahati nzuri Baraza hili limeundwa na wajumbe wanaotoka katika vyama viwili tu vya siasa, Chama cha Wananchi (CUF) na Chama cha Mapinduzi ambavyo vyama hivi sasa vinaunda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa.

Niwakumbushe katika ilani za uchaguzi za vyama vyetu vyote viwili tuliahidi tukishinda kila upande ulisema kwamba utahakikisha unaleta Sheria ya Kupambana na Rushwa. Kwa hivyo, nilidhani sisi tungepongeza kwa sababu

sote tumefungika na ilani ile kwamba leo vyama vyetu vinatekeleza ilani tuliyokuwa tumeingia katika uchaguzi na kwenda kuiombea kura kwa watu.

Mhe. Naibu Spika, pia pamoja na kuwa Baraza hili asubuhi tumeliona likiamua kuwaka moto linawaka moto kweli kweli wajumbe wako, lakini hiyo isiwe na maana kwamba serikali inapofanya jambo zuri tukawa hatupongezi, vyenginevyo tutawavunja moyo wenzetu vile vile ambao tumewakabidhi dhamana ya kuongoza nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme katika utangulizi huu kwamba yapo mambo ambayo serikali inafanya vizuri na inaonesha mwelekeo mwema. Mhe. Naibu Spika, kipindi cha karibuni hapa serikali imeweka hadharani ripoti ya uchunguzi kuhusiana na tukio la ajali ya meli ya *MV Spice Islanders* ambalo ni moja katika misingi ya utawala bora vitu kama vile kuwekwa wazi. Lakini sio tu kama wameweka wazi, imeweka wazi na hapo hapo ikachukua hatua na kuanza kutekeleza mapendekezo ambayo yametolewa na tume ile ya uchunguzi.

Mhe. Naibu Spika, nawapa pole wenzetu pengine humu ndani wameathirika lakini naamini sheria itahakikisha kwamba wanapata haki na wanatendewa haki. Lakini huko nisiende mimi nasema jumla tu, kile kitendo cha kuiweka hadharani ripoti ile, kitendo cha kuanza kutengeneza mapendekezo yake na ukitazama ripoti ya tume ile inaonesha kwamba Zanzibar tumeonesha mfano.

Mhe. Naibu Spika, jana gazeti la Mwananchi tahariri yake ilikuwa ni kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa hatua ile ambayo imesema haijawahi kutokea katika historia ya Tanzania. Lakini pia kuna makala kaandika mwandishi mwengine ndani ya gazeti lile lile akiwaambia TAKUKURU na wengine nendeni mkajifunze Zanzibar kutokana na yaliyotokea kutokana na ripoti ile. Sasa nasema Mhe. Naibu Spika, yapo mambo ambayo yanatuashiria kwamba tunakwenda kuzuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika hili pia nisisitize tena kwamba watu wameonesha wasi wasi kwamba sheria hii inaweza kuishia kuwabana labda wananchi na pengine ikawafaa viongozi. Lakini mimi ninachokiona katika sheria kwa ujumla maeneo mengi tuseme imeweka uwiano mzuri na nitatoa mfano.

Mhe. Naibu Spika, sheria hii kifungu cha 44 kinafanya kwamba ni kosa na kuweka adhabu kwa ukwepaji wa kulipa kodi. Lakini ungesema mnatuonea sisi kwamba hatulipi kodi lakini je, wanaotumia vibaya kodi. Mswada huu wa sheria kifungu cha 42 na 43 vinazungumzia kutumia vibaya mali. Kwa hivyo, ikiwa sheria hii itasimamiwa maana yake ni kwamba watabanwa watu walipe kodi lakini wanaokusanya kodi watabanwa watumie vizuri kodi za wananchi.

Lakini hapo hapo Mhe. Naibu Spika, niseme kuna baadhi ya wenzetu wameonesha kwamba hii sheria haikukamilishwa kwa sababu haina maadili ya viongozi kutangaza mali. Mimi nadhani Mhe. Waziri alitwambia nyuma kwamba serikali imeamua kuja na sheria mbili tofauti juu ya masuala haya. Kwa hivyo, nadhani tusifanye papara. Lakini mimi niseme moja kwa Mhe. Waziri na hili nakubaliana na wajumbe wenzangu waliokuwa wamechangia kwamba kuwa na sheria nzuri ni hatua moja na utekelezaji wa sheria ni hatua ya pili. Zanzibar tunakuwa mara nyingi tunasifiwa sana kwa kuwa na sheria nzuri lakini ugumu unakuja katika utekelezaji.

Kwa sababu tunakuwa na sheria nyingi nzuri karibuni moja nilipoliandika suala hili na kutaka maoni ya wananchi huko alisema kwamba haoni faida ya sheria hii mpiga kura wangu. Akasema mbona hakuonekani utashi wa kupambana na hiyo rushwa. Katika hoja yake akasema hivi kuna *traffic* wangapi ambao kazi yao kukaa majiani na kungoja watu wawabambikizie kesi ili wapate chochote wao, au hata kama hawana kesi au kama zipo zififirishwe lakini mradi yeye apate chochote. Hawa pia wanataka sheria ya kupambana na rushwa ndio waweze kupambana nayo. Kwa hivyo, alisema hoja yake ni kwamba kwa sababu wale wanaachiwa hakuna haja ya sheria hii kwanza tuanze na haya ambayo sheria zake zipo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nikasema hapana, ni kweli tuna changamoto katika utekelezaji lakini hiyo isitufanye kwamba tusitunge sheria. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nasema waziri alione hilo kwamba kuna *challenge* katika utekelezaji wa sheria hii.

Sasa Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nije katika mswada wenyewe. Mhe. Naibu Spika, nilisema kuna maeneo naomba nianze hayo katika kamati utakumbuka nilisema nina maoni tofauti na niliheshimu demokrasia kwamba ndani ya kamati wajumbe wengi walikuwa na mawazo tofauti na mimi lakini nikasema nitayazungumza Barazani kwa sababu pia hapa ninayo haki hiyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika kifungu cha 4 cha mswada huu, lakini pia nikiunganishe na kifungu cha (4)(1) na 6(1). Mhe. Naibu Spika, bahati nzuri ninayotaka kuyazungumza yameshachangiwa na baadhi ya wajumbe wenzangu, kwa hivyo nimefurahi kwamba kumbe ninao wenzangu ambao na wao wana mtazamo kama wangu. Mhe. Naibu Spika, nilipendekeza na hapa naliomba Baraza lako nilishawishi likubali kwamba vifungu hivi tuvifanyie marekebisho isiwe tu kwamba "Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais." Lakini nimalizie na atathibitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, hivyo hivyo, ikiwa kutateuliwa Naibu Mkurugenzi Mkuu basi na yeye pia athibitishwe na Baraza. Kwa sababu kama alivyojenga hoja vizuri kabisa Mhe. Rashid Seif Suleiman, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar itakuwa ni tofauti na vyombo vyengine vya serikali. Kwa hivyo, tumezoea kwamba Rais anateua Wakuu wa Taasisi mbali mbali lakini taasisi hii dhamana zake ni kubwa na nzito. Katika majukumu yake ni kuitazama serikali kwa ujumla wake pengine pamoja na huyo Rais mwenyewe.
Sasa nilidhani kwa uzito wa taasisi hii yule mkuu wake ingependeza sana kwamba mamlaka hizi mbili, kwa maana Mamlaka ya Utendaji inayowakilishwa na Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utendaji wa Shughuli za Serikali zikashirikishwa.

Sasa sipendekezi kwamba tumnyang'anye Rais madaraka ya kuteua lakini nasema baada ya kuteua basi Baraza hili lipewe nafasi ya kuthibitisha uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu. Tulipolizungumza hili Mhe. Naibu Spika, katika kamati inaonekana kulikuwa kuna hoja kwamba katiba yetu ina kipingamizi. Mimi siamini hivyo Mhe. Naibu Spika. Palitajwa ibara ya 51 ya katiba yetu naomba ninukuu.

Ibara ya 51:

> "Madaraka ya Serikali ya Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Rais. Kwa mujibu wa katiba hii anaweza kuyatekeleza yeye mwenyewe moja kwa moja au kuwapa viongozi walio chini yake kutekeleza madaraka hayo. Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika kifungu hichi hayazuii sheria kukabidhi madaraka ya kutekeleza kazi kwa chombo chochote cha umma kwa mtu mwengine yeyote ambaye si Rais wa Zanzibar."

Mhe. Naibu Spika, naomba tutazame sana hapo inapoanza ifahamike. Kwa maoni yangu Mhe. Naibu Spika, kifungu hichi kinatupa madaraka tukipendekeza na tukikubaliana hivyo kwamba uteuzi wa Rais kwa nafasi kama hii kuthibitishwa na chombo hichi haikizuii.

Lakini pia palizuka hoja katiba hii katika Baraza la Wawakilishi haitaji kazi hiyo. Lakini Mhe. Naibu Spika, si lazima kwamba kila tunachokifanya katika Baraza hili kiwe kimetajwa *exclusively* katika katiba. Ziko shughuli nyengine zinafanywa ambazo hazikutaja *exclusively* lakini zimefafanuliwa zaidi katika kanuni kwa sababu sheria hii imetoa nafasi hiyo. Kwa hivyo, tukikubaliana humu kupitia kifungu hichi tukatoa madaraka hayo kwa chombo hichi kuthibitisha tutarekebisha saa ngapi tutakuwa na utaratibu wa kuthibitisha uteuzi kama huu unaofanywa na Mhe. Rais. Huu Mhe. Naibu Spika, ni

utaratibu wa kisasa katika mambo kama haya badala ya madaraka kuyaweka zaidi katika sehemu moja.

Lakini Mhe. Naibu Spika, ukitazama namna ya mamlaka hizi tatu zilizoelezwa humu madaraka yake katika kifungu cha 5A (2) kinasema: "Mamlaka ya Utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma ni Baraza la Wawakilishi na Mamlaka ya Kutekeleza Utoaji Haki ni Mahakama."
Kwa hivyo, utaona Baraza la Wawakilishi halikutafsiriwa kwamba kazi zake ni kutunga sheria tu kama tulivyozoea kuliita, lakini linafafanua kwamba ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma na katika utekelezaji wa shughuli hizo ni pamoja na kuthibitisha uteuzi wa nafasi kama hii. Mhe. Naibu Spika, mimi sioni kama tutakuwa tunavunja katiba yetu.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa napendekeza kwamba hili tulitazame tena katika vifungu hivi vya 4 na 6. Namuomba sana Mhe. Waziri na watendaji walitafakari ili tuifanye sheria hii iwe nzuri zaidi na Zanzibar iendelee kuwa mfano kwa wengine katika vitu kama hivi. Kwa mara nyengine tunaweza kuwa tunachelewa kuanzisha lakini tukianzisha tunaonesha sisi mfano wa kufanya kitu kizuri zaidi kuliko hata wale waliotutangulia.

Hapo hapo Mhe. Naibu Spika, nikizungumzie kifungu chengine ambacho nilisema nitakitolea maoni hapa na hivi pia ni vifungu viwili ambavyo vinafanana, kifungu cha 14(8) na kifungu cha 13(2) cha mswada. Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 14(8) kinazungumzia kwamba ikibidi kushtaki baada ya uchunguzi mamlaka hii lazima ipate ruhusa ya Mkurugenzi wa Mashtaka, ama Mkurugenzi wa Mashtaka ashtakiwe mwenyewe au ikibidi basi Mkurugenzi Mkuu anaweza lakini kwa ruhusa ya Mkurugenzi wa Mashtaka."

Mhe. Naibu Spika, ukikisoma kifungu hichi kinasema "Kwa ruhusa ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkurugenzi wa Mkuu au mtu aliyeruhusiwa na Mkurugenzi Mkuu atakuwa na mamlaka ya kuendesha mashtaka kwa makosa ya rushwa au uhujumu uchumi chini ya sheria hii. Ndio maana hivyo hivyo, kile nilichokitaja mwanzo kifungu cha 13(2) ukitazama kinasema "Mkurugenzi Mkuu anaweza kupeleka taarifa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kuhusiana na kosa ambalo ameligundua katika uchunguzi wake chini ya kijifungu cha kwanza cha kifungu hichi."

Sasa Mhe. Naibu Spika, nilipendekeza na hapa naomba tena kulishawishi Baraza lione kwamba mimi kwa maoni yangu tungeliweka nafasi kwa mamlaka kupitia Mkurugenzi wake Mkuu au Afisa mwengine ambaye atakuwa amemuidhinisha. Moja kwa moja ikiona kwamba kuna haja ya yeye

mwenyewe au chombo chake kuendesha mashtaka basi tungefanya kazi hiyo bila ya kuomba ruhusa na kuipata kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Nasema hivyo Mhe. Naibu Spika, mara nyengine tukitazama hivi huwa tunatazama mtu gani yupo katika ile Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka lakini tukitunga sheria hatutazami hivyo. Kwa sababu leo anaweza kuwa mtu fulani tukamuona ni muadilifu na tunamuamini hatujui kesho atakuja mtu gani katika nafasi kama hiyo.

Mhe. Naibu Spika, nalitoa hili kwa sababu nasema tukitunga sheria tutazame na uzoefu wa watu wengine. Mhe. Naibu Spika, tusiende mbali tutazame kando ya pili tu ya bahari hapa kwa wenzetu Tanzania Bara au kama alivyosahihisha Mhe. Rashid Seif Suleiman leo Tanganyika.Mhe.

Naibu Spika, wenzetu wanayo TAKUKURU yaani Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Wao kama sisi tunavyopendekeza humu taasisi ile haikupewa madaraka ya kushtaki wenyewe lakini mpaka ipitie kwa *DPP* au ipewe ruhusa. Walipokuwa wakijadili marekebisho ya sheria ile ilipokuwa inabadilishwa kutoka kwa iliyokuwa TAKURU kuwa TAKUKURU. Wabunge nakumbuka mimi walitoa hoja kama hii tunayoizungumza sisi leo hapa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, uzoefu umeonesha kwamba kuna kesi nyingi katika kipindi cha miaka kama miwili au mitatu iliyopita ambazo TAKUKURU ilizifanyia uchunguzi, ikaridhika kwamba kuna kesi za kujibu kuhusiana na kesi za kujibu kuhusiana na makosa ya rushwa au ufisadi. Lakini baada ya mafaili kupitishwa kwa DPP basi yamekwama mpaka leo.

Hoja ni kwamba DPP hajaridhika, matokeo yake kuna kurushiana mpira. Ilikuwa akihojiwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU ndugu Edward Osea, anasema keshamaliza kazi anamsubiri DPP, akenda kuhojiwa DPP anasema bado uchunguzi uliofanyika haujatosheleza. Kwa hivyo, kuna kama kurushiana mpira.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nasema katika kuondosha mambo kama hayo kutoweza kutokea hapa kwetu, nadhani ni vizuri tukatoa nafasi katika mswada huu au sheria hii kwamba Mkurugenzi Mkuu na Mamlaka yake wakiona kwamba wana kesi ya kutosha ya kuweza kuipitisha mahakamani bila kupitia kwa Mkurugenzi wa Mashtaka waweze kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nisahihishe kitu moja kidogo tu, sio kitu kikubwa. Tulirekebisha katika kamati, lakini naona bahati mbaya tulipopitia hapa katika waraka wa kamati yetu kimesahauliwa. Kifungu cha 20(2)

ambacho katika marekebisho huu waraka wa marekebisho ya kamati unayapata katika ukurasa wa sita hapa. Kilikuwa kinasomeka kwamba;

Kifungu cha 20(2)

> "Hati ya utambulisho iliyotolewa na mahakama lazima itiwe sahihi na Mkurugenzi Mkuu".

Sasa baada ya marekebisho wameongeza yale maneno tuliyoongeza kuwa isomeke;
"Mkurugenzi Mkuu na muhuri wa Mamlaka". Lakini palikuwa na neno tulilirekebisha wamelisahau. Tulisema sio sahihi ni saini. Sasa naomba na hili kidogo makatibu wetu nafikiri liliwapitikia tulirekebishe na tutofautishe. Hivi karibuni kwa bahati nzuri wataalamu wa Kiswahili walitutofautishia vizuri, baina ya sahihi na saini. Nadhani tulichokikusudia hapa ni saini sio sahihi.

Mhe. Naibu Spika, naomba niruhusu kwa uchache kuingia ndani ya mswada, sio tena kuzungumzia marekebisho, lakini kuna baadhi ya vitu nataka kuvitilia mkazo tu na kuvitilia nguvu ambavyo vimetajwa katika sheria.

Mhe. Naibu Spika, wajumbe hapa wamezungumza na hapa nazungumza haya kwa kuipongeza serikali na wizara katika kuandaa mswada huu na pengine Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa mchango wake mkubwa iliyotoa kwa kuyaweka makosa yaliyotajwa ambayo yanaitafuna sana jamii yetu.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 41 kinazungumzia rushwa katika zabuni na kama kuna jambo katika nchi yetu linaonekana linatutafuna kweli kweli ni rushwa katika zabuni. Mhe. Naibu Spika, ukifuatilia katika Baraza hili hili mijada mingi hapa ambayo wajumbe wako wameiibua inahusu wasi wasi na kuwepo kwa harufu ya rushwa katika zabuni, pametajwa suala la ukodishwa wa kisiwa cha Changuu, tulilipitia kelele hapa na kamati yako ilikuja na maelezo, kamati kwa maana kamati ya Baraza la Wawakilishi, kuhusiana na suala la ukodishwaji wa kumbi katika hoteli ya bwawani. Tulizungumzia hapa mtambo wa *digital* wa televisheni kuja kwa jina la mtu binafsi wa Wizara ya Fedha. Pia tulizungumzia hapa kuuzwa kwa majengo ya serikali na tulizungumzia mambo mengi sana Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nasema nafurahi kwamba sasa inatambuliwa kwamba ni kosa kuwepo kwa rushwa katika zabuni na kuwekwa adhabu kali. Ni matumaini yangu kuwa hii itatusaidia kuziba mianyo hii.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, napenda kuzungumzia kifungu cha 42(1)(d) na kifungu cha 44. Kama nilivyosema haya nayatilia mkazo tu sina marekebisho,

kifungu hiki kinazungumzia makosa kwa kukwepa kulipa kodi. Mhe. Naibu Spika, hili katika utekelezaji namuomba Mhe. Waziri atakapokuwa keshakamilisha kuunda mamlaka hii. Moja eneo la kulitizama ni mahoteli ya kitalii katika nchi yetu. Kuna manun'guniko makubwa ya watu kwamba kama kuna eneo ambalo lina ukwepaji mkubwa wa kodi basi ni mahoteli.

Mhe. Naibu Spika, nilipata kuona nyaraka fulani kuna hoteli moja sitaki niitaje tena wala haiko mbali na mji hapa ina hoteli hapa Zanzibar na ina hoteli Dar es Salaam, wanaomba misamaha ya kodi kwa Zanzibar na wanaleta bidhaa ambazo ukitizama ule wingi wake tu unajua kwamba zile bidhaa ni lazima uwe na hoteli kama zile tano au sita kwa Zanzibar na sio kwa hoteli moja, lakini Zanzibar inakuwa ndio mlango wa kupitia kukwepa kulipa kodi, halafu zinachukuliwa. Bidhaa hizo zinasafirishwa Mhe. Naibu Spika, wala hazipiti katika bandari ya kawaida. Kuna bandari yanakuja maboti yanachukua moja kwa moja katika hoteli yanavuka bahari yanakwenda katika hoteli yake iliyokuwepo Dar es Salaam vinateremshwa, hivyo tunakwepa kulipa kodi kwa kuptia mlango wa Zanzibar. Kwa hivyo, nasema suala hili tulitizame sana.

Hata katika mahoteli haya yanayolaza wageni, kodi ambazo wanapaswa walipe, utakuta tunazikamua zaidi hizi hoteli za hapa mjini, tena tunawabana zaidi hawa wa ndani, lakini kule kwa wawakezaji wa kigeni kwenye mahoteli yale umekuwa ni mchezo kawaida na mimi naamini kwamba kuna fedha nyingi sana kwa sekta za utalii, basi ingekuwa tunasimamia vizuri hata hayo mapungufu mengi ya Dk. Sira kila wakati kubanwa kuhusu suala la ICU lingemalizika kwa sababu angepata fedha za kutosha kabisa kutokana na kodi inayokusanywa kutokana na mahoteli. Kwa hivyo nasema suala hili la kulipa kodi litiliwe mkazo.

Mhe. Naibu Spika, pia mswada huu uzuri wake huko katika kuweka hayo makosa ambayo yanaitwa ya uhujumu uchumi. Mimi Mhe. Naibu Spika, sioni huruma na wale waliozungumza kwamba tuna utamaduni wetu maghala kuweza kutumika kwa vitu hivi ama vile. Mimi nasema napongeza haya makosa yaliyoidhinishwa katika kifungu cha 46 na 47 ambacho kuna kuficha bidhaa na kingine kufanya taratibu ambazo zinakwenda kinyume na ushindani wa soko.

Mhe. Naibu Spika, wanaoumia mfanyabishara akifanya mambo haya ni mwananchi wa kawaida. Hasa katika bidhaa za chakula. Kwa sababu wafanyabiashara wa chakula wanajua kwamba mtu hawezi kukaa akaishi bila ya kula, kwa hivyo chakula ni lazima utakihitaji tu. Sasa kwa sababu hiyo wanajua kwamba hata akiongeza kodi vipi, mtu hana njia nyengine, ni lazima analihitaji pembe ili aweze kuishi.

Sasa wengine kwa tamaa zao binafsi wanaamua kuficha bidhaa kwa wakati fulani ili zionekane bidhaa zimeadimika ili wapate kupandisha bei, yapo haya. Hata Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko analijua hili, kwa sababu kajaribu mara kadhaa, lakini mara nyengine jitihada zake zinakwamishwa. Kwa hivyo, mimi napongeza sana kwa makosa haya kuwekwa na ninamuomba yeyote atakayekuja kusimamia malalamiko haya basi ayatazame kwa ukaribu sana, kwa sababu haya yanawagusa watu moja kwa moja, maskini za Mungu wanatizama kupata mlo wao wa siku.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 52 kinazungumzia kudanganya kima cha fedha. Jambo hili ni tatizo kubwa hasa katika mahoteli. Ndio maana asubuhi niliuliza swali hapa kuhusu wanaotumia dola kwa Zanzibar katika kulipia huduma mbali mbali. Kumekuwa na utaratibu hapa kama ukilipa kwa dola, basi unapotaka kurejeshewa pesa zako zilizobakia basi kuna *rent* tofauti ulizozoweka katika soko ukenda katika *bureau de change* na *rent* ukenda katika mahoteli, kwa nini iwe hivyo wakati sarafu ni ile ile moja. Kwa hivyo, nafurahi kwamba sheria hii imeweka kifungu cha kuweka kwamba ni kosa kwa mtu kudanganya kima cha fedha. Nadhani na hilo pia litaangaliwa kwa ukaribu, ili Zanzibar isionekane kama ni pahala ambapo mtu anaweza kuja kufanya anavyotaka tu, tuondokane na utaratibu huo.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 53 kinazungumzia matumizi mabaya ya *Office*, hili nalo ni muhimu sana. Kwa bahati nzuri Mhe. Naibu Spika, hili limeanza kuguswa na katiba yetu, lakini ilikuwa haijafanya kuwa ni kosa, kwa sababu katiba haiweki makosa. Lakini ukitizama kifungu cha 69(4)(a) na(b) katika miko ya uongozi pale katiba yetu inafafanua, kwa hivyo nafurahi kwamba sasa haya yanafanywa kuwa ni kosa kwa kupitia sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, ukitizama kifungu cha 69(4)(a) na(b) kinasema;

> “ni mwiko kwa kiongozi kutumia madaraka aliopewa kwa ajili ya manufaa yake binafsi au kwa upendeleo au kwa namna yoyote ambayo ni kinyume na lengo lililokusudiwa kwa madaraka hayo”.

(b) inasema;

> “ni mwiko kwa kiongozi kupokea kipato cha kificho”, sio kificho Spika wetu, “au rushwa au kushiriki katika mambo yoyote ya magendo”.

Kwa hivyo, mambo haya yametajwa katika katiba sasa yameingizwa katika sheria hii, ni matumainio yetu kama nilivyosema isije ikaonekana kuwa sheria imekusudia kwa watu wengine, lakini kwa sisi ambao tuna dhamana ya uongozi. Maana Mhe. Naibu Spika, watumiaji wa madaraka vibaya ni sisi

wenye dhamana na dhamana nyengine katika utendaji wa serikali. Kwa hivyo, nasema ni muhimu likatizamwa sana.

Pia Mhe. Naibu Spika, mimi napongeza kifungu cha 56 kuhusu rushwa katika uchaguzi. Tusilivike nguo nyengine hili kwa sababu tunaona litatugusa sisi, kwa sababu sisi ndio tunaokwenda katika uchaguzi. Kuna mjumbe mmoja kachangia hapa kasema kuna rushwa na sadaka. Mhe. Naibu Spika, tafsiri yake iko wazi, sadaka unatoa kwa kutegemea kitu kwa Mwenyezi Mungu na rushwa unatoa unayempa rushwa akupe kitu, tofauti yake iko wazi kabisa. Kwa hivyo, nasema tusijaribu kulikataa hili, haya yapo tuone vipi utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kuna bahati mbaya wenzetu Bara wamepitisha ile sheria ya gharama za uchaguzi, lakini mpaka leo inawashinda kutekeleza kwa sababu wameizonga mno, lakini hili lipo wazi kabisa. Mimi nasema tulisimamie kwa sababu tunaweza kujenga mazingira mazuri ya nchi yetu katika masuala haya ya siasa na hili pia tulitazame kwa upana wake.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kuzungumzia kifungu cha 66 na kifungu cha 68(1). Hivi vinakwenda hatua moja zaidi katika suala la kuwa na mali ambayo huna maelezo nayo, kumiliki mali pengine zaidi ya kipato chako na ukitaka kutoa maelezo huna maelezo. Kifungu cha 66 kinatoa uwezo wa kutaifisha mali hiyo ikiwa umeshindwa kuitolea maelezo na kifungu cha 68(1) kinazungumzia kuwa mali kama ile inaweza kutumika kama ni ushahidi katika kesi dhidi yako.

Mhe. Naibu Spika, mimi napongeza sana suala hili, kwa sababu kama nilivyosema kama mali umeipata kihalali, basi huwezi ukashindwa kutoa maelezo ya kuipata mali hiyo. Mhe. Naibu Spika, suala hili wananchi wengi wanalalamikia hasa tabaka letu la wanasiasa. Wanasema inakuwaje mtu kabla ya kupata nafasi ya uongozi ya utumishi fulani wanamuona alikuwa anaishi maisha ya kawaida, pengine ana kijumba chake na kigari chake kimoja. Lakini ghfla akapata nafasi unakuta minara ya majumba inasimama kila siku, yanazungumzwa haya. Ukitizama kwa mshahara huu ambao tunaambiwa ni siri usisemwe hapa, hautoshelezi kujenga majumba hayo halafu bado ukaishi maisha unayoishi. Lakini bado imekuwa tunaishi nayo.

Kwa hivyo, nasema nimefurahi kuona vifungu hivyo vimeingizwa na naamini kwamba Mamlaka ikiyasimamia vizuri na ikimpata msimamizi mzuri kama Mkurugenzi Mkuu, basi naamini kwamba tutaweza kuonesha mfano katika masuala mazima ya utendaji katika kazi zetu za kila siku na ndio maana Mhe. Naibu Spika, nikarudia tena kwamba msingi wa mamlaka haya utakuwa ni nani Mkurugenzi Mkuu wake. Nadhani kama nilivyosema, kwa sababu mamlaka haya yatakuwa ni tofauti na vyombo vyengine vya serikali narudia kupendekeza kwamba tusiridhike tu kwamba ateuliwe na Rais, lakini tuseme

pia athibitishwe na chombo hiki ili apate uhalali mkubwa zaidi na apate nguvu kubwa zaidi ya kusimamia sheria.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, niseme pamoja na marekebisho hayo ambayo naamini rafiki yangu Mhe. Waziri, Mhe. Haji Omar Kheir atayakubali na yale mengine ambayo nimemsaidia kwa sababu yamekuja katika kamati yangu kuyatolea ufafanuzi, naamini kabisa kwamba tutakuwa na sheria nzuri. Mimi nasema kwamba Mhe. Waziri akikubali mapendekezo hayo na ushauri huo, basi sheria hii mimi nitaiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu uliopo mbele yetu. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima wa afya na kuweza kufika katika shughuli zetu za kawaida katika Baraza hili.

Pili, naishukuru serikali kwa uwamuzi wake wa kuuleta mswada huu na umefika katika wakati muafaka ambapo katika nchi yetu kuna matatizo mengi hasa yanayohusiana na masuala ya rushwa. Mhe. Naibu Spika, naishukuru kamati ya katiba na sheria kwa kuisaidia serikali katika kutoa ufafanuzi mbali mbali na marekebisho ya awali.

Mhe. Naibu Spika, suala la rushwa katika jamii yetu ni tatizo kubwa sana. Kuna wakati marehemu Mwalimu Nyerere aliwahi kusema rushwa ipo mpaka Ikulu. Kwa hivyo, tukiangalia maana ya rushwa ni nini, basi tukitoka sasa hivi tukianza kutembea mpaka Mnazi Mmoja tu hapo tutakuta matendo ya rushwa yanatendeka, yaani imekuwa kama ni utamaduni wa watu, watu wanaona suala la rushwa ni utamaduni na wala watu hawajui hii rushwa ni nini.

Kwa hivyo, kabla ya kwenda katika mswada naiomba serikali kwa kupitia Wizara hii ya Nchi Afisi ya Ris Utumishi wa Umma na Utawala Bora, watu kwanza wapewe elimu kuhusiana na suala la rushwa. Kama sheria hii ikipita kesho tu basi naona tutakuwa na mahabusu wengi sana na watuhumiwa ambao watapelekwa mahakamani kwa suala la rushwa. Kwa hivyo, elimu ni kitu cha msingi sana katika suala hili.

Mhe. Naibu Spika, mimi naanza kwenda moja kwa moja katika vifungu, naangalia kifungu nambari 4 ambacho kinatoa uwezo kwa Rais kumteuwa kiongozi au Mkurugenzi ambaye anahusika na taasisi hii ya kudhibiti rushwa pamoja na uhujumu uchumi. Nakubaliana na maoni ya Waheshimiwa Wajumbe wenzangu ambao wametangulia kama kina Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Hija Hassan na wengineo kwamba baada ya uteuzi huu basi pia ni vizuri

kwamba wakapata kuthibitishwa katika Baraza hili. Hii sio kutokana na umuhimu wa mtu huyu, lakini pia umuhimu wa sheria hii uzito wake ulivyo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile naangalia kifungu cha 57(2) kinazungumzia kutoa rushwa kwa raia wa kigeni. Mimi kwa mawazo yangu kuanzia hapa katika kifungu cha 57(2), adhabu zote ambazo zinahusiana na masuala ya rushwa basi hapa ndio tuanze kutoa adhabu katika hii sheria, milioni 10 kwa raia wa kigeni na kifungo cha miaka 7. Rushwa ni adui wa haki, pahala popote ambapo rushwa itasimama basi hapo hapana maendeleo yoyote ya kisiasa, kiuchumi na masuala ya kijamii. Kwa hivyo miaka 7 hapa ilikuwa adhabu ya rushwa ndio ianze na hii milioni 10 nayo ndio ianze hapa. Sasa tutafute milioni 10 ya raia wa kigeni na mambo mengine.

Mhe. Spika, kifungu cha 61 kinazungumzia adhabu ya jumla Shs. 5,000/= na miaka 2. Hebu jamani tuangalieni miaka 2 kila siku tunashuhudia katika mahakama zetu, mtu anaiba nazi moja anafungwa miaka 2, lakini mtu anatenda kosa la rushwa tunaweka kuanzia miaka 2. Kwa hivyo, hapa tutilie uzito zaidi juu ya suala hili, adhabu kali ndizo zitakazotusaidia katika kukomesha matendo ya rushwa.

Vile vile katika kifungu cha 62 kinazungumzia kulipa fidia, pengine mtu kama atakuwa ametenda kosa hilo au amemsababishia madhara mtu basi alipe fidia, fidia ambayo inatakiwa ile ile kwa mujibu wa mswada huu na kifungu hiki. Sasa mtu tumemsababishia madhara makubwa pengine usumbufu, lakini badala yake tena tunakuja kumrejeshea kitu kile kile, sheria hapa ya kifungu hiki itakuwa bado haijatusaidia sana. Kwa hivyo, mtu anaweza akafanya kosa, lakini baadae akarudisha kile kitu chengine tu, kwa hivyo hapa naona hapana athari kubwa.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, tukiangalia kifungu hiki cha 58 kinachozungumzia masuala ya rushwa, ikiwemo rushwa ya ngono na adhabu iliyotolewa hapa nayo tuiangalie ni ndogo sana. Kwa sababu rushwa ya ngono tukiangalia katika sheria nyengine za adhabu, tunaikuta iko katika masuala ya ubakaji, katika ubakaji hapa kuna miaka mpaka 30. Sasa hapa kuna tofauti gani baina ya kumbaka mtu. Mimi naona tukitoa tafsiri ya kubaka basi katika sheria hii na kifungu hiki hapa tunapata kosa la ubakaji nalo limo humu humu, lakini katika sheria nyengine adhabu yake mpaka miaka 30 jela hapa.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano mtu anakwenda kutafuta kazi, anakwenda kutaka huduma yake mwenyewe anadaiwa rushwa. Kwa hivyo, hapa tutizame kosa hili la kudai rushwa ya ngono na adhabu iliyowekwa, lakini pia tuangalie katika sheria ile inayohusiana na masuala ya ubakaji kwamba adhabu kule ni

kubwa sana. Mimi hasa katika sheria hii naangalia zaidi katika masuala ya adhabu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo mimi niseme tu kwamba naunga mkono hoja hii, kutokana na umuhimu wa mswada huu katika nchi yetu ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa wakati huu wa magharibi haya kuweza kupata fursa iliyohuru kuchangia mada hii iliopo mbele yetu. Mhe. Naibu Spika, mara nyingi nchi yetu imekuwa ni wapokeaji wa maazimio kutoka aidha mataifa tofauti ya kikanda au mataifa makubwa ya kutekeleza baadhi ya maazimio. Mara nyingi hii inatuathiri sana kwa sababu mazingira na uwezo inakuwa ni tofauti ukilinganisha sehemu moja na sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Spika, ninachokifahamu ni kwamba sisi hapa Zanzibar kwa makusudi na sisi tuna nia ya kupambana na rushwa na tulianzisha *anticorruption group* hii ilikuwa iko chini ya polisi. Sasa kwanza mimi huwa najiuliza, kwa nini tuanzishe *executive* nyengine wakati kitengo kilichokuwa kinashughulikia mambo haya kipo. Kama ingelikuwa kitengo hiki kina mapungufu fulani, basi tungekiwezesha kitengo hiki kikawa na uwezo wa kisheria ili kikaendelea na kazi zake kama kawaida. Lakini huu mpango wa kusema leo tunataka *executive* nyengine maana yake tunaingiza pesa nyengine katika kitengo ambacho labda tungeepuka kufanya hivyo kama tungekitumia kitengo chetu kilichopo.

Mhe. Naibu Spika, tatizo kubwa liliopo labda ni kuwa kitengo hiki cha polisi kiko chini ya Muungano, labda ingekuwa ni kasoro kwetu kwamba kisingeweza kufanya kazi zake sawa sawa hapa Zanzibar. Lakini hivi sasa tuna *department* kama ya DPP, labda tungeitumia kwa kufanya hivyo na tusingekwenda moja kwa moja tu katika kuanzisha vitengo vipya ambavyo mimi nahisi utendaji wake ni mbovu.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tunavyo vitengo kama vya KMKM na malengo yake makubwa ni kupambana na magendo. Lakini katika miaka iliyopita tulikuwa tunashuhudia wenyewe, tumeipa kazi idara hii ya kupambana na magendo, lakini mahesabu yanatuonesha kwamba karafuu nyingi zilielekea nchi jirani ya Kenya na wao walishindwa kufanyakazi kama hii, sasa leo tunaanzisha kitengo chengine na jamii yetu sio rahisi kwamba mtu mmoja akatowe taarifa kwamba fulani amefanya kosa fulani la rushwa au kosa jengine. Kwa hivyo, utekelezaji sifikirii kama tutafikia malengo kama hayo tunayoyakusudia. Sasa mambo ya kuanzisha vitu kama hivi bila ya kuwa na utekelezaji mzuri yatatupotezea fedha nyingi sana.

Kwa hivyo, mimi ningependa tukakaa tukaangalia kama ingekuwa kitengo hiki kina mapungufu ya kisheria, basi hizi idara zetu tulizonazo tungezipa uwezo wa kisheria zikaendelea na kazi hizi bila ya kuleta muhimili mwengine kama huu tunaotaka kuuanzisha.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo, nataka niingie katika vifungu. Kuna kifungu cha 14(2)(a), hapa tumeelezwa kwamba atakaekuwa amefanya kosa. Kwa mfano mtu amesema uongo basi mtu huyo atakuwa ameingia katika kosa na adhabu yake pengine ni faini ya shilingi kuanzia milioni 1 mpaka milioni 100. Sasa mtu kama kasema uongo aje aambiwe atowe milioni 90, basi mheshimiwa tunampa fursa hata huyo ambaye atakuwa ana hukumu yeye labda kutumia upenyo huu kupata na yeye hiyo rushwa. Nafikiri tungeangalia vizuri zaidi. Je, kweli hapa pana uwiano upo.

Mhe. Naibu Spika, jengine ukiangalia katika kifungu cha 14 hiki kidogo kinakwenda kasoro na kifungu cha 15 ambacho kimetaja kosa hilo hilo, lakini yeye amekwenda moja kwa moja, amesema yeye huyo atapata adhabu yake ni milioni 1 tu sio zaidi ya hiyo. Sasa sijui huu uongo unakuwa wa aina gani mpaka huyu huku anapata adhabu kubwa kuliko huu uongo wa kifungu cha 14 ambao labda adhabu yake imekuwa ni kubwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, pia nataka niseme kidogo kuhusu kifungu cha 14(2)(a) kuna kauli inayosema kwamba kujibu hoja, huyu atakuwa amefanya kosa na kosa hili limechanganywa pamoja na mtu ambaye amesema uongo na adhabu yao imewekwa sawa sawa. Mimi nafikiri kosa la kuwa mtu hakujibu hoja, inaelekea pengine mtu huyo hilo swali alililoulizwa halifahamu, hivyo adhabu zake zingekuwa ni makosa mawili tofauti. Aliyekuwa hakujibu hoja adhabu yake ni hii na huyu ambaye kasema uongo pia na yeye akawa na adhabu yake nyengine. Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache naomba nimalizie hapo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kusema machache sana katika jambo hili ambalo liko katika ukumbi kwa wakati huu.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwanza nianze kwa kuipongeza sana serikali na hasa Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kutekeleza ahadi yake ya kuleta sheria hii mbele ya Baraza letu. Nakumbuka Mhe. Rais wakati anazindua Baraza hili. Moja kati ya mambo mengi aliyoyaahidi ni kuhakikisha kwamba ndani ya kipindi kifupi serikali yake itawasilisha mswada wa sheria hii na leo hii sote ni mashuhuda kwamba ndani ya kipindi hiki cha mwaka mmoja Mhe. Rais ameweza kukamilisha ahadi hiyo. Kwa hivyo, tunashukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais aliyasema yale au ameharakisha suala hili kutokana na ukweli wa athari ya suala hili la rushwa. Kwa kweli suala la rushwa ni la kitaifa na kimataifa, kwa sababu rushwa ina athari mbaya sana kwa uchumi wa nchi yoyote ile, kwani uchumi huathirika sana kwa vitendo vya rushwa. Lakini si uchumi tu, rushwa ni adui mkubwa wa haki, wananchi wengi masikini ambao ni wanyonge hukosa haki zao kwa sababu ya vitendo hivi vya rushwa.
Mhe. Naibu Spika, ukiyachanganya mambo yote mawili utaona kwamba kushamiri au kuwepo kwa rushwa hatimaye huzaliwa kitu ambacho kinachoitwa kukosekana kwa utawala bora katika nchi.

Kwa hivyo, kutokuwepo kwa rushwa maana yake kwa kweli ni kuimarisha kwa uchumi wa nchi, pia kupatikana haki kwa wananchi, lakini kupatikana kwa vitu hivyo tafsiri yake ni kuimarika kwa utawala bora katika nchi. Kwa hivyo, nasema kwamba naishukuru serikali pamoja na Mhe. Rais kwa kutimiza ahadi yake kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, kama ilivyoelezwa katika mswada kwamba madhumuni makubwa ya sheria hii ni kutokana na *convections* ambazo Tanzania imeridhia za Kimataifa. Kwa kuwa Tanzania imeridhia ndio hatimaye Baraza likaleta sheria hii.

Sasa naomba niseme kwa vyovyote vile kadri ambavyo Tanzania itafanya kama kuna sheria kama Katiba yetu inavyoeleza kwenye kifungu cha 132 cha Katiba yetu ya Zanzibar, Mhe. Naibu Spika naomba kunukuu.

Kifungu cha 132(1) cha Katiba ya Zanzibar kinaeleza hivi:-

(1). “Hakuna sheria yoyote itakayopitishwa na Bunge la Muungano ambayo itatumika Zanzibar mpaka sheria hiyo iwe ni kwa ajili ya mambo ya Muungano tu na ipitishwe kulingana na maelekezo yalio chini ya vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano”.

(2). “Sheria kama hiyo lazima ipelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi na Waziri anayehusika”.

Kwa kweli kwa kipindi kirefu kumekuwa na tatizo hili kwamba, kumekuwa na sheria ambazo hazihusiani na mambo ya Muungano na ambazo hutakiwa zifanyekazi Zanzibar bila ya sheria hizo bila ya kuridhiwa na Baraza letu. Mhe. Naibu Spika, kwa kipindi kirefu tumekuwa tukilipigia kelele sana suala hilo.

Kwa hivyo, hiyo nakumbushia tu, kwamba kwa sheria hizo pamoja na mikataba kama hii ya kimataifa, ambayo imeridhiwa na Tanzania, basi kwa vyovyote vile na sisi Zanzibar tuletewe, ili angalau sisi kama Baraza tuweze kuweka baraka zetu.

Mhe. Naibu Spika, suala la kuwa na sheria nzuri ni kitu cha msingi sana, kwa sababu tunaweza kuwa na sheria tu kwa kufuata mkumbo, lakini tunaweza kuwa sheria ambayo haikidhi yale mahitaji pamoja na matakwa ambayo tumeyakusudia. Kwa hiyo, sheria hii kwa kiasi kikubwa kwa mujibu tulivyoichambua tumeona ime-*cover* eneo ambalo tunalihitaji. Lakini kama alivyosema Mhe. Rashid Seif Suleiman kwamba mambo haya lazima yaangalie na mazingira ya nchi au sehemu inayohusika.

Kwa mfano, aina za rushwa hizi zinatofautiana baina ya jamii moja na nyengine, pia nchi moja na nyengine, yaani rushwa inayofanyika katika nchi iliyoendelea ni tofauti sana na nchi zetu za kimasikini. Kwa maana hiyo, ni vyema mambo haya yakazingatia hali hiyo na kwa kiasi kikubwa tunasema mswada huu umezingatia mambo hayo, tunashukuru sana kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, nadhani siku zote wanaofanya rushwa katika mazingira yetu ni sisi viongozi pamoja na watendaji katika sekta mbali mbali. Kwa hivyo, bila ya kuangalia sheria katika maeneo hayo muhimu, sheria tutakuwa nayo, lakini bado haitokuwa *effective*.

Kwa kweli niungane na wenzangu wote waliotangulia kueleza kwamba, kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kitendo cha rushwa kuonekana na kazi ngumu sana, lakini yanayotokana na rushwa ni rahisi kuonekana, lakini kitendo kinapotokea ni tabu sana kuweza kukibaini.

Kwa hivyo, kwa kuwa mara nyingi hutokea katika maeneo ya kwetu sisi viongozi pamoja na watendaji hasa katika Sekta ya Umma, basi wale walioanzisha utaratibu wa kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi ni suala la msingi sana. Mhe. Naibu Spika, nasema tena kwamba sisi viongozi pamoja na watendaji wa serikali, ndio sehemu kubwa katika eneo hili. Kutokana na hali hiyo, naomba niungane na wenzangu kwamba kuwepo na utaratibu maalum ama ndani ya sheria itamkwe wazi wazi au kwa namna yoyote, lakini suala hili ni la msingi sana. Katika sheria kadri nilivyoangalia sijui pengine nime-*overlook*, lakini kwa vyovyote vile kitu hiki ni muhimu sana kuwepo na utaratibu wa Maadili ya Viongozi hasa kutangaza mali zao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano haiwezekani mtu ameajiriwa ndani ya kipindi cha mwaka mmoja au miwili, lakini akamiliki utajiri ambao hawezi kuelezea na wala hilo haliwezekani.

Kwa hiyo, naomba nisisitize hapo, kwamba kuwa na utaratibu kwa vyovyote vile utaratibu huo usiachane mbali na upitishwaji wa sheria hii katika Baraza letu, yaani usipishane iwe ni vitu vinavyokwenda sambamba. Kwa kweli viongozi kuwe na maadili fulani ambayo yatawafanya waweze kutangaza mali zao kwa umma kila kipindi ambacho tutakubaliana. *(Makofi)*

Jengine naomba nikubaliane na wenzangu kwamba kuhusu suala la uteuzi wa Mkurugenzi. Mhe. Naibu Spika, lazima tufike pahala Zanzibar kwa kweli jambo linalowezekana kutekelezeka japo kuwa wenzetu hawajafanya, lakini kama upo uwezekano basi tufanye sisi na Zanzibar huo ndio ustaarabu wetu.

Kwa kweli mambo mengi ya kimaendeleo yanayotokea hivi sasa katika ukanda huu tulionao yalianza hapa Zanzibar. Kwa hivyo, sisi tusiwe watu wa kukopia tu, lakini wakati mwengine tukopiwe sisi kwa mambo mazuri. Kwa maana hiyo, kila ambalo ni zuri ambalo tunaliweza kulifanya basi tulifanye, ili wenzetu nao waige Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ule utamaduni wa kumuachia Rais kuteua baadhi ya watendaji na kuwa ndio basi, mimi nadhani utaratibu huo umeshapitwa na wakati.

Kwa kuanzia basi ni vyema tukaanza hapa kwa uteuzi huu wa Mkurugenzi wa Kamisheni hii, ikiwezekana Rais kama ilivyo sheria apewe mamlaka hayo ateue, lakini kuthibitishwa kwake lazima tuje kumthibitishe Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, utaratibu huo uendelee na hata watendaji wengine muhimu, kwa sababu wapo watendaji muhimu ambao lazima kutahitajika Baraza hili wapate ridhaa zetu.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na muda ulivyo, basi naomba nisisitize suala hilo na kumalizia katika hili kwamba uteuzi wa Mkurugenzi Rais awe na mamlaka ya kumteua, lakini na Baraza la Wawakilishi liwe na mamlaka ya kumthibitisha.

Nakushuuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ingawa ni ndogo tu kama kawaida yangu. Kwanza niseme kwamba rushwa ni adui wa haki.

Kwa kweli rushwa ni tatizo linalosumbua nchi nyingi duniani, hii ndio sababu inayozifanya nchi kwa nyakati tofauti na kutokana tofauti za kiuchumi, kisiasa, kijamii pamoja na kiutamaduni.

Kupambana na Rushwa. Nchini Tanzania chimbuko la mapambano dhidi ya rushwa lilianzia mwaka 1930, pale Mtawala wa Kikoloni wa Kiingereza alipotumia Kanuni ya Adhabu ya India kuwaadhibu watumishi wa serikali waliopatikana na hatia ya rushwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa maneno hayo nianze kuchangia mswada huu.

Kwanza niende kwenye kifungu cha 13(h) na 18(d) ambavyo vinaelezea kuhusu masuala ya elimu, naomba kunukuu.

Kifungu cha 13(h) cha Mswada kinaelezea hivi:-

> "Kuelimisha wananchi juu ya hatari ya rushwa na makosa ya kuhujumu uchumi na kuomba kuungwa mkono na jamii katika kupiga vita makosa ya rushwa na kuhujumu uchumi".

Kwa kweli hii ni sawa kwamba tunahitaji tutoe elimu kwenda vijijini, kuandaa makongamano pamoja na semina mbali mbali. Lakini naona mbali ya kifungu hiki pia kuna kifungu cha 18(d) ambacho kinafanana na maelezo ya kifungu cha 13(h). Kwa hivyo, nadhani kama kuna mgongano wa hivi vifungu.

Vile vile kifungu cha 17(2) naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 17(2) cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Mkurugenzi Mkuu angalau kila baada ya miaka miwili anatakiwa kuteua mtu au taasisi yenye sifa kufanya tathmini ya utendaji kazi, ili kujua kama viwango vya utendaji kazi vimefikiwa na kama viwango hivyo vinatosheleza".

Mhe. Naibu Spika, wasi wasi wangu hapa Mhe. Waziri ni kwamba mtu hawezi kuchagua wimbo au kusema anaweza kumchagua mtu yeye mwenyewe wa kumtathmini kazi yake.

Kwa hivyo, ni vyema kuwe na chombo chengine ambacho kitamtafuta huyo mtu ambaye atatathmini kazi ya huyo mhusika.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye kifungu cha 24 naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 24(7) cha mswada kinaelezea hivi:-

> "Kwa madhumuni ya kifungu hiki "kumbukumbu" inajumuisha vitabu, taarifa za marejesho, hesabu za benki na hesabu nyengine, ripoti, nyaraka za kisheria au za biashara na mawasiliano mengine, isipokuwa mawasiliano binafsi".

Mhe. Naibu Spika, hapa nasema kwamba sijafahamu vizuri, lakini atakapokuja kufanya majumuisho Mhe. Waziri atanisaidia.

Vile vile kifungu chengine cha 25 naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 25 cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Mkurugenzi Mkuu au mtu mwengine yeyote aliyeruhusiwa na Mkurugenzi Mkuu, anaweza kwa hati au bila ya hati, kuingia katika eneo lolote na kufanya upekuzi wa nyaraka, mali au kitu chochote ambacho kinashukiwa kuwa kimo ndani yake au ndani ya eneo na ambacho hakikuwasilishwa na mtu kwa mujibu wa masharti ya sehemu hii".

Sasa kama mtu anakwenda awe nayo au asiwe nayo hati, kwa hivyo hapa pia kidogo pamenipa mashaka, basi namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, atakapokuja kufanya majumuisho aweze kunifafanulia zaidi.

Vile vile kwenye kifungu cha 46 cha mswada naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 46 cha mswada kinasema hivi:-

> "Mtu atakayeficha bidhaa kwa madhumuni ya kuzuia au kupunguza usambazaji au kuenea kwa bidhaa hiyo, ili kujitengenezea bei bidhaa hiyo kwa maslahi au faida yake, atakuwa ametenda kosa la kuhujumu uchumi chini ya Sheria hii".

Mhe. Naibu Spika, ni kweli hapa nchini yapo matatizo haya ambayo na hasa wanaofanya biashara ya mafuta ya *petrol* mara nyingi. Kwa mfano, wanaposikia tu kuwa bei zimepanda, basi mafuta yale ambayo yako kwenye *stock* yanapandishwa bei. Kwa hivyo, sheria hii naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Kifungu cha 47 cha mswada naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 47 cha mswada kinaeleza hivi:-

> "Mtu yeyote ambaye atafanya au ataacha kufanya jambo kinyume na ushindani wa soko au njama kwa madhumuni ya kuzuia ushindani wa soko la bidhaa na huduma, atakuwa ametenda kosa la kuhujumu uchumi chini ya Sheria hii".

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, muda umemaliza, kwa hivyo malizia.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Naibu Spika, namalizia, kwa hayo machache naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nawashukuru wachangiaji wote waliopata muda hivi jioni. Lakini bado mjadala utaendelea kesho asubuhi na mategemeo yetu jioni tumwite Mhe. Waziri kwa ajili ya kufanya majumuisho na kupitisha. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe wakazidi kuangalia mswada, ili tupate wachangiaji kesho baada ya kipindi cha maswali na majibu.

Baada ya hayo naahirisha kikao chetu hiki hadi kesho siku ya Jumanne tarehe 24/01/2012 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 24/01/2012 saa 3:00 asubuhi)